

3 NOVEMBA, 2022

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Tatu – Tarehe 3 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tilia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA
BUNGE:**

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu; leo kabla sijamuita hapa mbele kwa kutumia kanuni yetu ya 44 ambayo inahahu sualiliano na shughuli na lenye maslahi kwa umma kwa muda usiozidi dakika kumi, iku fuatiwa na maswali ya Wabunge kwa dakika ishirini kuhusu taarifa yake au masuala mengine yoyote ya Serikali.

Kwa hiyo, tutamia hii Fasili ya 4, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa taarifa ya mambo ambayo atatueleza hapa, halafu baada ya hiyo taarifa yake maswali kwa siku ya leo yatakuwa yanahusu taarifa hiyo. Kama itahitaji ufanuzi wowote na kama kutakuwa hakuna ufanuzi unaohitajika Mheshimiwa Waziri Mkuu atafanya kazi hiyo moja tu ya kutueleza kile ambacho anacho. (Makof)

Kwa hivyo nimuite Mhesimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aje atueleze taarifa aliyonayo. Karibu Mheshimiwa. (Makof)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu katika mfululizo wa vikao vya Bunge siku ya Alhamisi imekuwa ikitengwa maalum kwa ajili ya kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa lengo la kupata mrejesho kutoka kwenye Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kisera yenyе maslahi mapana kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Alhamis ya leo itatumika tofauti kidogo na pengine ilivyozoleka. Leo badala ya kusimama hapa na kupokea hoja ya maswali ya papo kwa papo toka Wabunge wenzangu, nitaomba uridhie nitumie fursa hii kutolea ufanuzi masuala kadhaa ambayo si tu yameibua mjadala mionganini mwa Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge lako Tukufu lakini pia yamebeba maslahi makubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni kauli ya Serikali kuhusu kuzuka kwa moto katika hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro. Vilevile nitatoa kauli ya Serikali kuhusu

utekelezaji wa zoezi linaloendelea nchini la utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, kihusu moto katika hifadhi ya Kilimanjaro, tarehe 21 Oktoba, 2022 majira ya saa mbili na nusu usiku ililipotiwa taarifa kuzuka kwa moto katika bonde la Karanga lilipo ndani ya hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (*KINAPA*). Serikali inaendelea kuchunguza chanzo cha moto huo ili kuchukua hatua stahiki. Jitihada za udhibiti wa moto zimefanyika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali hadi leo tarehe 03 Novemba, 2022. Zoezi la uzimaji unaendelea vema na moto umedhibitiwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo korofi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zoezi la uzimaji moto linaendelea vizuri kwa mafanikio makubwa pamoja na kuwa na changamoto kadhaa ikiwemo upepo mkali ambao ulikuwa mara kwa mara unababilisha mwelekeo, uwepo wa miinuko mikali na makorongo makubwa, mrundikano wa mboji ambao uhifadhi moto kwa muda mrefu na uoto wa mimea ya asili aina ya erica ambayo inashika moto kwa urahisi na hivyo kusababisha moto kusambaa kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau wote ambao wamekuwa bega kwa bega na Serikali katika kuhakikisha kuwa moto unadhibitiwa. Ninatoa shukrani za pekee kabisa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, kwa kutoa helkopta mbili, na askari 878 kuongeza nguvu katika zoezi la uzimaji moto ambao umedhibitiwa kwenye maeneo mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa zoezi la uzimaji moto kwenye Bonde la Karanga linaendelea matukio mengine ya moto yaliyobainika ndani ya hifadhi ya Kilimanjaro, ni

3 NOVEMBA, 2022

kwenye msitu wa asili katika eneo la Ubetu – Samanga Wilayani Rombo, na eneo la Mandara Wilaya ya Marangu. Moto huo ulidhibitiwa na kuzimwa na vikosi vyetu vya jeshi la ulinzi Tanzania TPDF, askari wa Jeshi la Uhifadhi, Jeshi la Akiba Mgambo, kutoka Wilaya za Rombo na Longido na Jeshi la Polisi kutoka Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, tuko hili limesababisha hasara hofu na kuteketea kwa kilomita za mraba 33 za uoto wa asili, uharibifu wa madhali ya ukanda wa juu wa hifadhi na kuteketeza viumbe mbalimbali. Hata hivyo, kutoka na jitihada za Serikali na wadau tumeweza kuokoa maeneo muhimu ya utalii kwa kupanda mlima ambayo yamebaki salama na hivyo shughuli ya utalii kuendelea kama kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya moto inayojitokeza kwenye maeneo ya hifadhi ikiwemo Mlima Kilimanjaro, ninaiielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kushirikiana kwa karibu na TANAPA pamoja na KINAPA, katika kuhakikisha kuwa;

- (i) Kinaundwa kitengo ndani ya TANAPA na KINAPA cha kukabiliana majanga au maafa yanayotokea ndani ya hifadhi;
- (ii) Kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia ya kisasa hususani katika tahadhari utambuzi na uzimaji moto; na
- (iii) Kuimarisha shughuli za doria na uokoaji wa kushirikisha jamii na wadau.

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, muitikio wa wananchi na wadau wengine katika kuzima moto ulikuwa mkubwa na wengi walifanya kazi kwa ari kubwa na kuhakikisha zoezi la kuzima moto linaisha salama bila kuleta madhara kwa watalii au miundombinu ya shirika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, natoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, pia shukrani za dhati kwa viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, majeshi yetu, TANAPA, KINAPA, taasisi nyingine za Serikali pamoja na zisizokuwa za Serikali ikiwemo pia Skauti, UVCCM, wananchi wa vijiji kutoka Wilaya za Rombo, Siha, Moshi Mjini na Vijijini pamoja na wadau wote walioshikiri kikamilifu katika uzimaji wa moto. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, itaendelea kuboresha uwezo wa kupambana na majanga kwa kuimarisha kitengo cha maafa, mifumo ya kisheria na kitaasisi na kutoa mafunzo ya pamoja kwa vyombo mbalimbali. Wakati wote Serikali itahakikisha upatikanaji wa vifaa vya tahadhari, uokozi na utoaji huduma mapema kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utambuzi wa mifungo kwa kutumia hereni za kielektroniki. Eneo la pili ambalo ninalitolea kauli leo ni zoezi linaoendelea nchini la utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki. Itakumbukwa kuwa mwezi Oktoba, 2021 Serikali ilianza kufanya utambuzi wa mifungo kwa kutumia hereni za kielektroni na kuisajili kwenye mfumo wa utambuzi ili kurahisisha ufuatiliaji wa mifugo na mazo yake.

Mheshimiwa Spika, hereni hizo zinaonesha utambulisho wa utaifa wa mfugo wenyewe, zikifuatiwa na

namba za mkoa, mfugo unakotoka, namba za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mfugo ulipo pamoja na namba zinaonesha taarifa ya mfugo na mfugaji. Namba hizo utolewa na Serikali na taarifa hizo za mfugo na mfugaji hutunzwa kwenye barcode ambazo hupatikana kielektroniki duniani kote.

Mheshimiwa Spika, zoezi la utambuzi wa mifugo ni utekelezaji wa takwa la kisheria kulingana na sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo wa mwaka 2021 na kanuni zake za mwaka 2011. Naomba nirudie, usajili na ufuatiliaji mifugo ya mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011. Hivyo, kukamilika kwa zoezi hilo kunawezesha ufuatiliaji wa mifugo yetu nchini kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo kurasimisha umiliki wa mifugo kwa mfugaji mwenyewe na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, sambamba na kuhamahama kwa mifugo kusikozingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, manufaa mengine ya zoezi hili ni kuimarisha kosafu ya mifugo, kuongeza thamani ya mifugo, kuongeza thamani ya mifugo kwenye masoko, kuwezesha matumizi ya bima na upatikanaji wa mikopo kwa wafugaji, upatikanaji kwa urahisi wa mifugo iliyopotea au kuibiwa na kufanikisha sensa ya mifugo kwa ajili ya kuiwezesha Serikali na wadau wengine kupanga mipango ya miundombinu, malisho na huduma nyingine za malisho na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki ulipaswa kukamilika tarehe 31 Okotba, 2022. Hata hivyo, tangu kuanza utekelezaji wa kanuni husika mwaka 2021 hadi kufikia tarehe hiyo idadi ya mifugo iliyotambuliwa na kusajiliwa ni 5,068,616 tu, sawa na asilimia 11 ya lengo la kutambua mifugo milioni

3 NOVEMBA, 2022

arobaini na tano mia tisa na ishirini. Kufuatia hali hiyo, Serikali ilitoka kwa umma kuhusu hatua iliyofikiwa na kuongeza muda wa utambuzi wa mifugo kwa hiari kuwa tarehe 31 Desemba, 2022, na baada ya hapo ingechukua hatua za kisheria kwa wafugaji ambao mifugo yao haitakuwa na hereni.

Mheshimiwa Spika, bei elekezi ya kuweka hereni za kielektroniki kwa mnyama mmoja ni shilingi 1,750 kwa ng'ombe na punda, shilingi 1,000 kwa mbuzi na kondo. Gharama hizi zimekuwa zikilalamikiwa na wafugaji kuwa ni kubwa tofauti na uhalisia na kwamba zoezi hilo linaendesha kibiashara badala ya kihuduma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesikia hoja za wafugaji, kuhusu mapungufu ya kanuni, usimamizi wake na utekelezaji wake na gharama kubwa ya uwekaji hereni za kielektroniki na inaona kuna haja ya kufanya upya tathmini ya zoezi hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Serikali imeamua kusitisha utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki kwa kipindi cha miezi mitatu mpaka tarehe 31 Januari, 2023 wakati ikiendelea na tathmini ambayo itawezesha kutoa mwongozo wa namna bora zaidi ya kutekeleza zoezi hilo kwa mafanikio. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, inathamini sana sekta ya mifugo katika kukuza uchumi wa nchi na wafugaji wenyewe. Serikali imefanya juhudii kubwa kuibadili sekta hii kwa kufungua soko la nyama katika nchi mbalimbali, kuondoa tozo, kero na kuweka ruzuku kwenye dawa za kuogesha mifugo na ujenzi wa

mabwawa na malambo. Hivyo, ninatoa wito kwa wafugaji wote nchini kufuga kisasa ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa nyama na mazao mengine ya wanyama kwa ajili ya masoko na uchakataji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie nafasi hii kuziagiza Wizara za Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wdau wa sekta ya mifugo kuhakikisha miradi mikubwa ya maji inayotekelzwa kwenye maeneo yenye shughuli za wafugaji inafanyiwa tathmini ya kupewa kipaumbele cha kutengeneza miundombinu kwa ajili ya mifugo, ikiwemo maeneo ya kunyweshea mifugo badala ya kuacha mifugo Kwenda kwenye mabonde yaliyohifadhiwa ikiwa ni ukiukwaji wa sheria na vyanzo vingine vya maji ambavyo sasa vinapotea kwa kasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

SPIKA: Haya ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge mmesikia taarifa hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ina mambo makuu mawili. Moja, kuhusu moto uliozuka kule Mlima Kilimanjaro na namna ambavyo Serikali imeufanya kazi. Changamoto nyingine alioizungumzia ama taarifa nyingine ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inahusu utambuzi wa mifugo.

Kuna Mbunge yeote mwenye swalí kuhusu taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? Nimeona Wabunge wanne; Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Ally Kassinge, Mheshimiwa Olelekaita na Mheshimiwa Mbunge wa Kalenga. Mheshimiwa Getere umesimama, baadaye. Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini nashukuru kwa kauli ya Serikali ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili la uvalishaji hereni kwa ng'ombe lilianza katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya Nkasi, na ikafikia mahali mpaka kutishwa kwa wafugaji, na mimi Mbunge nikalazimika kwa sababu ilikuwa ni kauli ya Serikali, nikapita kuwahamasisha wafugaji kutii maagizo ya Serikali na wakatoa hiyo fedha ya shilingi 1,750. Leo kuna maeneo ambayo yalikuwa hayajafikiwa; kwa kuwa ni utaratibu mzuri mlileta ninyi upigaji chapa siyo wafugaji, Serikali ilitoa hayo maagizo na wafugaji wakalipa, leo likaja agizo lingine la uvalishaji hereni wametii.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua, kwa kuwa ni nia njema ya Serikali, kwa wale ambao walikuwa tayari wameshalipa hiyo fedha, itakuwaje ili na wao wajione ni sehemu ya wafugaji wengine wa Tanzania?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hatujasitisha malipo, tumesitisha zoezi hili ambalo linalalamikiwa ili kuipa nafasi Serikali kuititia Wizara ya Mifugo kufanya tathmini ya mapungufu ya kanuni iliyowekwa ili kuweza kufanikisha zoezi hili vizuri kwa kushirikisha na wadau. Kama kutakuwa na maamuzi mengine ndani ya Wizara ya kupunguza bei, fedha, itakuwa ni baada ya mjadala huo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa sasa tumesitisha tu zoezi lenyewe kuendelea, kwa sababu tangu sheria imewekwa mwaka 2010 na kanuni zake mwaka 2011, kati ya mifugo milioni 45 ni mifugo milioni tano tu mpaka leo kuanzia mwaka 2011 ndiyo imefanikiwa kufikiwa. Kwa nini? Maana yake kuna tatizo. Kama tungetekeleza inavyotakiwa leo tungefikia angalau nusu ya mifugo yote nchini kuwekwa hereni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumesema tunasitisha kwa muda wa miezi mitatu, ili kuipa nafasi Wizara kukaa ndani ya Wizara yenyewe, kupitia kanuni zao kuona wapi kuna dosari zilizosababisha kutofanikiwa kupata mifugo mingi zaidi, lakini kupitia hayo malalamiko ambayo yanawafanya wafugaji au kukwepa au kutoshiriki vizuri au kuijunganisha vizuri na watendaji walio kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambao ndio wanatakiwa kuwatambua watu wao kila Wilaya ili sasa kuweka mfumo mzuri unaowezesha kufikia hatua nzuri zaidi na kuondoa manung'uniko yanayotokana na utekelezaji ambao unaonekana si mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya januari, sasa hayo mambo yote, maazimio yote yatakayokuwa yamefikiwa, ili waweze kufanya vizuri wakati wa utekelezaji yataanza kuanzia tarehe 1 Februari, 2023. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Jackson Kiswaga ajiandae.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa

Waziri Mkuu. Swali litajikita katika eneo la zoezi la utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba Serikali ilipoanzisha zoezi hili ilikuwa na nia njema kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameieleza lakini sisi wananchi pamoja na hayo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyaeleza tunatambua pia kwamba zoezi hili lingepunguza kwa kiwango kikubwa migogoro ya wafugaji dhidi ya watumiaji wengine wa ardhi, kwa sababu mifugo ingekuwa imetambuliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati Serikali imesitisha zoezi hili ili iweze kufanya tathmini kwa miezi mitatu; nini mkakati wa Serikali wa muda mfupi na wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba uingizaji holela wa mifugo hautoendelea na hautoweza kuathiri na kuleta migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yako matatizo kwenye sekta ya ufugaji ambapo kwa sasa tunaona kuzagaa holela kwa mifugo yetu, lakini pia mifugo mingi kuingizwa kwenye vyanzo vilivyoohifadhiwa kisheria na kusababisha madhara mengine kama ambavyo sasa tumeona vyanzo vingi vinakauka.

Mheshimiwa Spika, kusitisha kwa miezi mitatu kutaiwezesha Wizara sasa kuweka mkakati thabiti kwanza kuhakikisha kwamba wanakutana na wadau na

kuelimisha namna nzuri ya ufugaji kisasa kama alivyotamka kwenye taarifa; na pili, kushirikisha mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kutambua maeneo yote yenye mifugo na mipaka yao ili sasa lengo la kuweka hereni ambapo moja kati ya malengo ya kuweka hereni yaliyokusudiwa ni kuhakikisha kwamba tunapunguza kuhamahama kwa mifugo hii kiholela kutoka eneo moja mpaka eneo lingine, kwa sababu hereni inatambulisha mahali mfugo ulipo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa utaratibu huu tutakuja kujipanga vizuri na kesho kutwa tuna kikao cha Mawaziri wote wenye sekta zinazohusu mifugo, maji, mazingira pamoja na ardhi, pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa hapa Dodoma kuweka mkakati wa kudhibiti hali hiyo. Hiyo ndiyo moja kati ya njia ambayo tumeamua ili tuweze kufikia hatua nzuri ya kuelimisha pia na wafugaji umuhimu wa kufuga. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo mnakumbuka wakati tunaendesa zoezi la wanaohama kwa hiari Ngorongoro, na watu wa Loliondo kupisha lile eneo na kuwaweka mahali pazuri na upimaji wa vijiji vyao, tuliiagiza Wizara itumie vizuri eneo la Msomera kuwa ni eneo la ufugaji kisasa la kimkakati kama pilot area ili wafugaji wengine wapate kujifunza kutoka Msomera.

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara inaendelea na zoezi hilo la kuratibu vizuri pale Msomera, tunataka sasa mfumo huo uhamie kwenye Halmashauri nyingine zote nchini ili ufugaji sasa uwe na tija, wafugaji watambulike, mifugo tuitambue, tuwasaidie kutohama kwa umbali mrefu unaosababisha mifugo kupata shida, kutafuta

malisho na huku Serikali ikijipanga kujenga maeneo ya kunyweshea na majosho. Huo ndiyo mkakati wa Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taarifa hii na wafugaji wote nchi nzima leo, kwa kweli wamepokea taarifa hii vizuri sana. *In fact*, leo nilikuwa najiaanda tutumie Kanuni ya 54 tujadili hili suala kama la dharula. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu umeni-pre-empt. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na hayo, kipindi hiki sasa mvua hakuna, ukame ni mkubwa sana, ng'ombe za wafugaji zinakufa. Nilikuwa naiomba Serikali, wakati mwingine pamoja na mjadala huu, na kweli hii bei ni kubwa sana, tuangalie hata hiyo Januari, wakati mwingine kama mvua itakuwa haijanyesha, kwa kweli kuleta zoezi hilo wakati ng'ombe zinakufa na ukame, kwa kweli litakuwa bado ni suala gumu kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Januari, yes, lakini tuangalie pia msimu wa mvua ili wafugaji hao waone kwamba hata hii mifugo mnayoweka herein, iwe na afya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Naona Mheshimiwa Olelekaita ameamua kutoa ushauri. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, tutamalizia na Mheshimiwa Getere.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, kwa kuwa suala la Mlima Kilimanjaro ni suala nyeti kwa uchumi wa nchi, na ni maeneo muhimu sana ambayo yanatuletea fedha nyingi pamoja na Ngorongoro na Serengeti; na Jeshi la Kujenga Taifa limeonesha uwezo mkubwa katika operesheni mbalimbali katika nchi hii:-

Je, kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuwa hata na kambi ndogo ndogo mbili hata za wanajeshi watano au sita, kuzunguka Mlima Kilimanjaro? Kwa sababu kwenda mbele inawezekana kuna wivu mkubwa unajitokeza kwa sababu ya matangazo makubwa ambayo tunayafanya ya kuleta watalii katika nchi hii.

Swali ni kwamba je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuwa na kambi kambi ndogo ndogo mbili za Jeshi ili kulinda Mlima Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tukio hili moto Mlima Kilimanjaro linajitokeza pia na maeneo mengine na linatokana na baadhi ya watu wasiopenda mema ambao pia hawataki hata uhifadhi, huchoma moto maeneo yote yanayotakiwa kuhifadhiwa kama ambavyo ingekuwa kupitia elimu mbalimbali zinazotolewa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tumeona tatizo hilo na katika kipindi cha muda mrefu tulikuwa hatujapata moto kiwango hicho kwenye Mlima Kilimanjaro, lipo jambo tumejifunza. Ushiriki wa majeshi yetu yote; JWTZ, Jeshi la Mgambo, Jeshi la Polisi, na wananchi pamoja na Skauti na makundi mbalimbali yaliyojitokeza kwenda kuzima moto, tayari baada ya zoezi hilo litakapokamilika, tutakaa chini kufanya tathmini.

Swali lako ambalo limeingia pamoja na ushauri, tutauzingatia ili sasa tuwe na mkakati endelevu kwenye maeneo mengi muhimu ambayo yanaweza kujitokeza tatizo la moto, ikiwemo na kuimarisha Kitengo cha Maafa na hasa kwenye maeneo ya moto. Kuwa na vifaa, kuwa na wataalam ambao pia wanapata mafunzo ya mara kwa mara ili tuweze kukabiliana na majanga haya yanapotokea popote pale.

Mheshimiwa Spika, naomba kupokea pia na ushauri aliutoa Mheshimiwa Kiswaga. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swalii kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kweli kama kuna siku moyo wangu umefarijika, ni leo.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa nalalamika hapa kwamba hivi tunamwamulia nani? Hivi kumbe haya mambo yanawezekana? Ni juzi tu umekaa nasi hapa kwenye *briefing*, tumetoa kilio chetu. Nadhani ni juzi tu, siku mbili kabla, leo Serikali imekaa, Mkuu amekaa na mama, mama kaamua, sasa wafugaji wamejitoa kwenye mnyororo wa kuwa huru sasa, wanaweza kwenda kuuza ng'ombe wao mnadani. Kwa sababu imefikia leo mtu hawezi kwenda mnadani mpaka awe na hereni.

Mheshimiwa Spika, sasa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninachotaka kusema ni kwamba kumbe haya mambo ya kuamua yanawezekana. Sasa nakuja kwenye Wizara ya Mifugo, wafugaji wamekuwa wakitolewa kwenye mapori ya wanyamapori, tunasema sawa tu, tuhifadhi wanyama, ng'ombe wabaki. Wafugaji wana maeneo ya wafugaji ya kutoka Wizara ya Kilimo, yalikuwa yanaitwa *holding ground*. Liko eneo la Mara pale linaitwa *Buhemba Building Ground*, wale waliokuwa wanatunza mifugo kwa kuzalisha ndama, wametoka mwaka 1977, ile kampuni ilikufa, ikawapa wakulima wa vijiji vitatu. Leo Wizara ya Mifugo inataka kuuza eneo kwa mtu. Wizara ya Mifugo inataka kunyang'anya wakulima maeneo yao ya ufgaji kwenda kuyauza kwa mtu, badala ya kwenda kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu wazee wa kule wamekuja naye aliniahidi leo ataonana nao, na Wizara yote iwepo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru. (*Makofii*)

3 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi hilo jambo lilikuwa halina uhusiano kabisa na taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, ndc – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya Kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Venant Daudi Protas.

Na. 40

**Mpango wa kuongeza majengo katika Kituo cha Afya
Itobo – Nzega**

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. JACQUELINE K.
ANDREA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza majengo katika Kituo cha Afya Itobo Wilayani Nzega?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kuongeza majengo katika Kituo cha Afya Itobo kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Shilingi milioni 500 zilipelekwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje, jengo la maabara, kichomea taka, jengo la mama na mtoto, jengo la upasuaji na jengo la kufulia nguo. Ujenzi wa majengo haya upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Venant Daudi Protas, swalii la nyongeza.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Ni kweli majengo yameshaanza kujengwa katika kituo cha Itobo pamoja na kuendeleza; Serikali imekuwa ikiipeleka fedha na kujenga majengo nusu baadhi ya vituo, kikiwemo Kituo cha Igalula, jengo la OPD halijajengwa, Kituo cha Lutete majengo hayajakamilika:-

Je, nini mikakati ya Serikali kupeleka fedha kumalizia vituo vya afya vyote ili wananchi waendelee kupata huduma? Ahsante. (Makofii)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijenga vituo vya afya kwa awamu kwa kupeleka fedha awamu ya kwanza kujenga majengo ya awali na awamu ya pili kumalizia majengo yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kuna baadhi ya vituo vya afya vimepata awamu ya kwanza Shilingi milioni 250, vitapelekewa awamu ya pili Shilingi milioni 250 kutimiza Shilingi milioni 500. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vituo vya afya ambavyo bado havijakamilishwa, fedha itapelekwa awamu ya pili ili kukamilisha majengo yale na vituo vianze kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru wa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pale Kijiji cha Chomachankola, Tarafa ya Choma, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kutupatia fedha kuongeza kwenye Kituo cha Afya cha Choma:-

Je, ni lini sasa Wizara italeta fedha kwa sababu ahadi hii imetolewa toka 2018? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

3 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali iliahidi kupeleka fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Choma, Kijiji cha Chomachankola katika Jimbo la Manonga na ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge amefuatilia kwa karibu sana, na mwaka wa fedha uliopita tulikosa kifungu cha kupelekea fedha ile, lakini nimeongea naye na tumekubaliana katika mwaka wa fedha huu tutahakikisha fedha inapelekwa ili kitu cha afya kianze kujengwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Mwaka 2008 Serikali ilianza ujenzi wa jengo la mama na mtoto kwenye zahanati ya Kijiji cha Msada, Kata ya Msada, lakini mpaka leo ni miaka 14 lipo kwenye renter. Naomba kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha za kumalizia?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweka utaratibu wa kutumia fedha kutoka Serikali Kuu na pia kutumia fedha kutoka mapato ya ndani halmashauri kukamilisha baadhi ya majengo na hususan majengo katika ngazi ya zahanati. Kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, kuhakikisha wanatenga fedha katika asilimia 40 ya miradi ya maendeleo kukamilisha jengo la mama na mtoto katika zahanati ambayo Mheshimiwa Mbunge ametaja. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

MHE. CONDESTER M. SICALWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Je, ni lini Serikali itaboresha kituo cha afya cha Ndalambo ikiwa ni sambamba na kuongeza majengo? Kituo hiki kinahudumia kata zaidi ya tano zilizopo kwenye Tarafa ya Ndalambo. (Makofij)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Jimbo la Mombasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya vituo vya afya ambavyo ujenzi wake ulianza, lakini haujakamilika na inaweka mpango wa kukamilisha vituo vya afya vile havijakamilika ili viweze kutoa huduma za afya kwa wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa

3 NOVEMBA, 2022

Mbunge kwamba kuwa kituo kile kilishaanza ujenzi na hakijakamilika, tutakwenda kukamilisha kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba mpango na dhamira ya Serikali ni kukamilisha kwanza vituo vya afya ambavyo vilianza ujenzi na havijakamilika ili vipate vifaa tiba na kuanza kutoa huduma za afya kabla ya kuendelea kujenga vituo vingine vipyta. Vile vile tutaendelea kujenga zahanati za kimkakati isipokuwa vituo vya afya vipyta mpaka pale tutakapokuwa tumekamilisha ujenzi wa vituo vya vya afya ambavyo tayari vimeshaanza. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Kata ya Mlowa, Kijiji cha Mkolango, wananchi wa Mkolango wamejenga zahanati pamoja na Diwani na Mbunge; na Rais alipokuja tulimweleza jambo hili na aliahidi kwamba sasa atakwenda kumalizia kwa sababu imekwisha, wameshaezeka na kila kitu; na Naibu Waziri na Waziri walikuwepo na ndiyo mlisikia: Sasa je, ni lini mtatuletea fedha ili wananchi wa Mkolango muweze kuwaunga mkono zahanati hii imaliziwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Mlowa, Kijiji hiki cha Mukolango kwa kutoa nguvu zao kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuanza ujenzi wa zahanati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika bajeti ya Serikali ya mwaka huu wa fedha, fedha zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati na tutatoa kipaumbele katika zahanati hii ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya cha Changuge, Tarafa ya Gelango, Wilaya ya Ranya ni moja ya kituo ambacho kimejengwa muda mrefu sana na kwa sasa majengo yake yamechakaa na hata yaliyopo hayatoshelezi kulingana na mahitaji ya tarafa na kata ile. Nataka nijue mpango wa Serikali sasa kuboresha vituo vya afya vile vya zamani ili angalau viendane sasa na kasi na uhitaji wa wananchi wa sasa. Nini mpango wa Serikali katika kuboresha vituo vya afya vya zamani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Jimbo la Ranya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika maeneo mbalimbali kote nchini kuna baadhi ya vituo vya afya na

3 NOVEMBA, 2022

hospitali za halmashauri ambazo ni chakavu, na Serikali imeweka kanzidata kwa kutambua vituo vyatya afya chakavu na itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ukarabati wa vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tuichukue hii hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tufanye tathmini ya kituo hicho cha afya na kuona uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Patric Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 41

Hitaji la Daraja Kata ya Arusha Chini

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Daraja Kata ya Arusha chini litakalouunganisha Vijiji vyatya Muungano, Mikocheni na Chemchem?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 barabara hii imetengewa fedha kiasi cha Shilingi milioni 475.00 kwa ajili ya kuanza kujenga daraja katika Mto Ronga ili kuweza kuunganisha Vijiji vya Muungano, Mikocheni na Chemchem. Mradi huu upo katika hatua za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TARURA itaendelea kuweka katika vipaumbele vyake ujenzi wa barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuhakikisha inaweza kupitika katika kipindi chote cha mwaka.

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, swalil ya nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Barabara ya Getifonga - Mabogini hadi Kahe, iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kujengwa kwa kiwango cha lami na huko ndiko ilikojengwa hospitali ya wilaya: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii?

Mheshimiwa Spika, barabara ya *International School - Kibosho KCU* hadi kwa Raphael imebakiza kilomita nane kukamilika kwa kiwango cha lami: Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hii?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba barabara aliyoitaja mwanzo ya kutoka Getifonga – Mabogini Kahe, ipo katika llani ya Chama Cha Mapinduzi na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hii kwa sasa iko katika usanifu kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami. Usanifu unaofanyika ni wa kilomita 31.25, kwa hiyo, tupo katika hatua nzuri kwenye hiyo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka *International School* – Kibosho - KNCU mpaka kwa Raphael na yenyewe kilomita 8.42 tayari imeshajengwa kwa kiwango cha lami. Kiwango ambacho kimebakia ni kilomita 5.49, kwa hiyo na yenyewe tunatafuta fedha ili tuanze ujenzi kwa kiwango hicho.

SPIKA: Mheshimiwa Idd Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kuuliza ni lini sasa Serikali itajenga daraja linalounganisha Halmashauri ya Msalala, Kijiji cha Namba Tisa na Halmashauri ya Nyang'hwale? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi kubwa ambayo sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumekubaliana kuifanya sasa ni pamoja na kutambua madaraja korofit yote ambayo tunahitaji kuyahudumia sasa ili tuunganishe moja na eneo lingine. Kwa hiyo, hata hili daraja alilotaja Mheshimiwa Mbunge la kuunganisha Halmashauri ya Msalala na Halmashauri ya Nyang'hwale liko katika mpango wetu, hivyo, nimuondoe hofu katika hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swalii la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwanza niipongeze Wizara kuitia TAMISEMI, kupeleka fedha nyingi katika Kata ya Swaya. Naomba kujua kama ni lini watawaongezea ili waweze kujenga daraja linalouanganisha wananchi na hasa wanafunzi kuelekea kwenye Shule ya Sekondari ya Swaya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukipeleka fedha mara kwa mara, uzuri yeye mwenyewe amekuwa ni shuhuda na nimhakikishie tu kwamba sisi tunazingatia maoni ya wananchi na jambo lake tumelipokea. Ahsante sana.

3 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 42

Ujenzi wa Chuo cha Ualimu Masasi

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE aliuliza:-

Je ni lini serikali itajenga Chuo cha Ualimu Masasi baada ya Chuo cha Ualimu Ndwika kuwa shule ya Sekondari ya Wasichana?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge Jimbo la Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilibadili Chuo cha Ualimu Ndwika kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana kutokana na mahitaji ya wakati huo. Kwa sasa Serikali ina vyuo 35 vya Ualimu vyenye uwezo wa kudahili wanachuo 25,054 ambapo hadi sasa jumla ya wanachuo 22,085

wamesajiliwa. Idadi hii ni chini ya uwezo wa vyuo hivyo katika udahili kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeelekeza nguvu katika ukarabati wa vyuo hivyo ili kuweka mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Serikali itaendelea kujenga Vyuo vya Ualimu katika maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji na rasilimali.

SPIKA: Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, swal la nyongeza.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili nyongeza. Swal la kwanza; ni lini basi Serikali itaona umuhimu katika hivyo vyuo ambavyo imepanga kujenga basi kijengwe pale Masasi kwa sababu tayari kilikuwepo na Serikali ilifanya maamuzi ya kukibadilisha chuo na kuwa shule ya sekondari ili pia ihudumie wananchi wa Masasi na wilaya za jirani?

Mheshimiwa Spika, swal la pili; je, ni lini Serikali pia itaona haja ya kufungua matawi vyuo vya elimu ya juu Wilayani Masasi ili kuweza kusaidia watu wa Masasi, lakini pia na watumishi mbalimbali kuweza kuijendeleza kielimu? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambe, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi kwamba Serikali inamiliki vyuo 35 na katika vyuo hivi tuna mahitaji ya wanafunzi zaidi ya 25,000 lakini wanafunzi waliopo kwa sasa ni 22,000. Tafsiri yake hapa ni kwamba, hata hivi vyuo vilivyopo bado vina upungufu mkubwa wa kupata wanafunzi. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanya tathmini ya jambo hili kulingana na mahitaji, kama nilivyozungumza kwenye majibu yangu ya msingi, iwapo kama tutaona kwamba kuna uhitaji wa kujenga chuo, basi Masasi tutaipa kipaumbele katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Mkoa wa Mtwara, bado tuna vyuo vitatu vya ualimu, tuna Chuo pale Mtwara Mjini, tuna vyuo viwili kimoja cha ufundi na kile cha kawaida. Vilevile katika Wilaya ya Newala tuna chuo pale Kitangale ambavyo wanafunzi hawa wote wanaweza wakatumia vyuo hivi kuweza kupata elimu yao katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kama mahitaji yatatokea basi tutaweza kwenda kujenga katika eneo hili Masasi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lake la pili, kuhusiana na masuala ya matawi ya Vyuo Vikuu, naomba nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hivi sasa Serikali inakwenda kujenga katika maeneo mbalimbali matawi ya Vyuo Vikuu. Naomba tu nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu, pale Mtwara tuna matawi ya Chuo Kikuu Huri ana Chuo Kikuu cha Stella Marius, lakini vilevile tuna tawi la Chuo cha TIAA. Vyuo hivi vyote vinaweza vikatumiwa na wenzetu wa Masasi kwa ajili ya kupata mafunzo yao pale. Vilevile Chuo Kikuu chetu cha Dar es Salaam kiko

3 NOVEMBA, 2022

mbioni kufungua tawi katika Mkoa wa Lindi ambapo ni jirani kabisa na Wilaya ya Masasi. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunashukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Dennis Londo.

Na. 43

TFS Kutoa Vibali vya Malisho kwa Wafugaji

MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. INNOCENT E. KALOGERIS aliuliza:-

Je, ni lini TFS itaanza kutoa vibali vya malisho kwa wafugaji kama inavyotoa vibali vya kuvuna mbao na mkaa ili Serikali ipate mapato?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Misitu, Sura ya 323, Kifungu cha 26(n) kinakataza kuingiza au kuchunga mifugo kwenye maeneo ya hifadhi. Aidha, Kanuni za

3 NOVEMBA, 2022

Misitu za mwaka 2004, Kifungu cha 14(4) kimeweka katazo la kutoa vibali vya kuchunga au kulisha mifugo au kufanya shughuli za kilimo kwenye hifadhi za misitu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kuchunga, kulisha mifugo au kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya hifadhi za misitu ni kuvunja sheria. Hivyo, sheria zimebekwa ili kulinda rasilimali zilizomo hifadhini kwa matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa kizazi cha sasa na vijavyo.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni kweli sheria inataka hivyo, lakini kwa kuwa shughuli za kibinadamu zinaendelea kama uvunaji wa mikaa na kuvuna miti katika misitu hiyo ya TFS, je, Serikali hawezi kuona sasa wakati umfefika wa ku-review sheria hiyo ili kwenda na wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tunaona hifadhi nyingi ambazo zinachomwa kwa makusudi katika utaratibu wa kuachia muda majani yaote. Je, Serikali haioni kwamba hata utaratibu huo pia umepitwa na wakati, wakati umefika sasa wa kuruhusu watu kuvuna majani ili kutoa suluhisho ya malisho ya ng'ombe ambao sasa hivi wanahangaika hasa katika maeneo ya wafugaji?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya

nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Kalogeris akiwakilishwa na Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu haya maswali mawili kwa pamoja kwamba ni kwa nini tunafanya usafi kwenye maeneo ya hifadhi hususani kuchoma majani na Mheshimiwa Mbunge amesema badala ya kuchoma hayo majani basi yangetumika kwa ajili ya mifugo. Kiutaalam wa kiuhifadhi, wanashauri endapo kuna na mahitaji ndani ya hifadhi, ikiwemo mbolea, lakini pia kuna calcium ambayo wanaitumia wanyama pori, basi huwa kuna maeneo ambayo yameainishwa ambayo yanatengeneza hiyo calcium kwa kuchomwa jivu, ili wanyamapori waweze kupata calcium waendelee ku-survival kwenye maeneo yao ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo jivu hili huwa linatengeneza mbolea ili iweze kusaidia kuendelea kumea kwenye yale majani ambayo yanatumika kwa ajili ya malisho ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swalii la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa namna ambayo kwa kweli wameweza kudhibiti moto uliokuwa unawaka ndani ya Mlima Kilimanjaro. Katika dhana hiyo hiyo ya kudhibiti, je, Serikali haioni iko haja ya kufanya mabadiliko ya sheria ili wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro waweze kupata service levy kama ilivyo kwenye maeneo mengine yenye mgodi

3 NOVEMBA, 2022

ili kuongeza sense of ownership ya wananchi wanaozunguka kuona mlima ule ni mali yao? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utali, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapokea mawazo yake, lakini bado tunatambua kwamba wananchi wanaozunguka maeneo ya Mlima Kilimanjaro, ni sehemu ya hifadhi na mara nyingi tumekuwa tukihamasisha upandaji wa miti ili kulinda hifadhi hii ili iweze kutunzwa vizuri. Kwa hiyo, tunalipokea hili pia la sheria ili tuweze kuangalia utaratibu mwingine kuhakikisha mlima huu tunautunza vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, Mbunge wa Mwanakwerekwe, sasa aulize swalii lake.

Na. 44

Kutanua Sehemu ya Kusafirisha Abiria wa Zanzibar Bandari ya Dar es Salaam

MHE. HASSAN HAJI KASSIM aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kutanua sehemu ya kusafirishia abiria wanaokwenda Zanzibar katika Bandari ya Dar es Salaam?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia TPA imetenga kiasi cha Sh.1,500,000,000 kwa ajili ya maboresho ya sehemu ya abiria katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa sasa ni manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya maboresho ya eneo la kusafirisha abiria kwenda Zanzibar. Maboresho yatahusisha ukarabati wa miundombinu ya gati la kuhudumia abiria ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria ili kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria, kuweka mkanda wa mizigo (*conveyor belt*), ukarabati wa kingo za gati, maboresho ya sehemu ya abiria mashuhuri (VIP), sakafu na vyoo. Aidha, Mkandarasi anatarajiwa kupatikana na kuanza kazi mwezi wa Desemba, 2022.

SPIKA: Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, swalii la nyongeza.

MHE. HASSAN HAJI KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu ya Serikali. Hata hivyo, kwa kuwa utaratibu uliokuwepo sasa hivi, wa abiria ambao wanasaferi wanausbiria sana nje kabla ya kuingia ndani. Je, ni lini Serikali hii itatoa maelekezo ya wale abiria

3 NOVEMBA, 2022

ambao tayari wana tiketi, wasisimame pale nje, waingie ndani moja kwa moja na kusubiria usafiri ndani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Haji Kassim, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo ama jengo lilipo la kusubiria abiria pale Dar es Salaam Kwenda Zanzibar lina uwezo wa kubeba abiria 150 na jengo ambalo tutajenga litakuwa na uwezo wa kubeba abiria 400.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hatua ambayo Serikali inachukua tunaweza ratiba maalum, mahususi kwa boti zote mbili ambapo boti ya kwanza kama ambavyo iko inaondoka saa moja asubuhi, boti ya pili itaondoka saa tatu na nusu, boti ya tatu itaondoka saa sita, nyingine saa nane mpaka saa kumi na mbili. Kwa abiria wote ambao wanakuwa nje na wana tiketi, hawa ndio wanatakiwa waingie kwenye jengo hili ili kuruhusu wasafiri kuliko mwingine yeyote kwa sababu eneo lile bado ni dogo. Kwa hiyo, ni maelekezo kwa Serikali kwa abiria wote, lakini pia wale wote wanaosimamia eneo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Asia Mwadini Mohamed, swali la nyongeza.

MHE. ASIA MWADINI MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Changamoto hii ambayo inaonekana kwa abiria wetu kwa upande wa

3 NOVEMBA, 2022

Dar es Salaam hali kadhalika changamoto hii imejitokeza sana kwa upande wa Zanzibar. Je, Serikali ina mpango gani wa upanuzi wa Bandari ya Zanzibar ama kujenga bandari mpya ili kupunguza changamoto hii kwa abira wetu?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa suala la Bandari ya Zanzibar ni suala ambalo lipo kwenye Wizara ya Wenzetu kule, tutawasiliana nao ili tuone namna gani ya kupanua ujenzi wa Bandari hii ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 45

Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mifupa – Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Lindi

MHE. TECLA M. UNGELE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupeleka Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na Mifupa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Lindi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Hospitali ya Rufaa ya Lindi ina jumla ya Madaktari Bingwa watano ambao ni Daktari Bingwa wa Upasuaji mmoja, Madaktari Bingwa wa Afya ya Uzazi na Mtoto wawili, Daktari Bingwa wa Mionzi mmoja na Daktari Bingwa wa Dawa za Usingizi mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza idadi ya Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi, Wizara imapelekwa kusoma jumla ya Madaktari saba, ambao Madaktari wawili wanasomea Udaktari Bingwa wa Watoto, Madaktari wawili Ubingwa wa Upasuaji, Daktari mmoja Ubingwa wa Mionzi, Daktari mmoja Ubingwa wa Mifupa na Daktari Bingwa wa Afya ya Uzazi na Watoto mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Serikali inakamilisha taratibu za uhamisho ili kumpeleka Hospitali ya Lindi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Tecla Mohamed, swali la nyongeza.

MHE. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu hayo ya Serikali. Swali la kwanza; kwa kuwa magonjwa yasiyoambukiza ni tatizo kubwa katika Mkoa wa Lindi. Je, ni lini sasa watapeleka *specialist hao wa internal medicine?* (Makofij)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni lini Waziri atakwenda Mkao wa Lindi pale Hospitali ya Sokoine kwenda kuona hali halisi ya ukosefu wa Madaktari hao na kadhia wanayopata wananchi? Ahsante. (Makofij)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalilake la kwanza ni lini Serikali sasa itapeleka Daktari huyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tukae naye pamoja tuwasiliane na Afisa Utumishi na Wizara ya Utumishi tuone ni lini watakamilisha mchakato huo. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, la pili, ameniuliza kwamba ni lini tutakwenda Lindi ili kwenda kuona matatizo yanayoendelea pale. Namuahidi Mheshimiwa Mbunge mara tu tukimaliza Bunge, tutashirikiana na yeye na Mbunge mwagine wa Mkao wa Lindi twende huko. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mariki, swalil la nyongeza.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Hospitali ya Mkao wa Katavi inao upungufu mkubwa sana wa Madaktari Bingwa akiwemo Physician na Daktari Bingwa wa Watoto, pia Mkao mzima Daktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake yupo mmoja tu.

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari Bingwa katika Mkao wa Katavi?

SPIKA: Mheshimiwa, Naibu Waziri wa Afya Majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kwanza hospitali yao ni mpya inayojengwa sasa, lakini ni kweli kwamba siyo tu kwa Mkoa wa Katavi bali upungufu wa Madaktari Bingwa uko karibu nchi nzima, ndiyo maana unaona kuna mkakati unaofanywa kuongeza Madaktari Bingwa. Nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge tuangalie la kufanya. Kwa sababu najua kuna Daktari wa Watoto aliyejukwepo pale alipelekwa Songwe, sasa tutaona ni nini kinafanyika ili kurekebisha hayo yaliyotokea. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swalil ya nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Natambua kwamba kila hospitali ya Wilaya inayo shida ya kupata Madaktari Bingwa na upatikanaji wake kidogo unakuwa ni mgumu. Pia kuna Halmashauri zinakuwa na uwezo wa kusomesha Madaktari Bingwa, mojawapo ikiwa ni hospitali yangu. Sheria ya Utumishi inasema tukimsomesha *at least* afanye Miezi 36 ndiyo aweze kuhamza. Sasa kwa sisi ambao tumepeleka Madaktari wakapata huo Ubingwa, halafu wakarudi ndani ya wiki moja wakahamishwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwenye hili suala la Madaktari Bingwa siyo tu kwa hospitali za

Wilaya hata za Mikoa kuna baadhi ya Mikoa ukimpeleka Daktari Bingwa ana-resign anakwenda sehemu nyingine. Tulichokubaliana ni kwamba kama ni Wilaya au Mkoa ametokea pale Daktari kwenda kusomea Ubingwa, anapewa mkataba maalum wa kufanya kazi na Halmashauri au Mkoa huo kwa muda wa Miaka mitano bila kuhama. Kwa hiyo, hilo likianza kutekelezwa na tumeanza kutekeleza huo mkakati ili kuzuia wasihame tena, hivyo, nafikiri hiyo itasaidia sana. Mheshimiwa Musukuma hebu uje kwangu tuone kilichotokea kwenye eneo lako ili tuone kwa yule mliyemsomesha kama tunaweza kufanya lolote. (Makof)

SPIKA: Mheshimiwa Tunza Malapo swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi Sokoine ni sawa kabisa na tatizo lililopo katika Hospitali ya Mkoa wa Mtwara Ligula, kukosekana kwa Daktari wa magonjwa ya ndani pamoja na mifupa. Je, Serikali ina kauli gani kutuletea, ingawa tunajua tunayo hospitali ya Rufaa lakini hii ni kuhusu ya Mkoa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, nimemwelewa Mheshimiwa kwa sababu sijaiangalia vizuri kama ya Mtwara lakini kwa kweli wana bahati moja kwamba, wana hospitali ya Mkoa ambayo ina baadhi ya *specialists* lakini haijafika hata kilometra moja kutoka Hospitali ya Mkoa kuna Hospitali ya Kanda, ambayo nayo ina Mabingwa. Kwa hiyo, mimi na wewe tutakuja tuangalie specifically tatizo ni nini ili tushirikiane na Mheshimiwa Waziri tuone tunafanya nini.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimesimama ili kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kwa sasa ina mpango maalum wa kusomesha Madaktari Bingwa na Madaktari Bingwa Bobezi ambapo katika Mwaka huu wa Fedha wa 2022/2023 tutasomesha Madaktari Bingwa na Bobezi 139. Madaktari Bingwa na Wabobezi 136 tutawasomesha nje ya nchi. Tumeamua kuwasomesha kwa utaratibu wa *set* badala ya kupeleka Daktari Bingwa Mmoja wa magonjwa ya ndani inabidi awe na Muuguzi Bingwa wa masuala ya usingizi, kuwepo na mtoa huduma Bingwa wa *radiology*, kwa hiyo ndiyo jambo ambalo tunaenda nalo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tuna Madaktari Bingwa 457 tunawasomesha katika *pair* moja moja. Kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, kwanza tutafanya *assessment*, tunafahamu kuna baadhi ya hospitali za Rufaa za Mikoa zinazo idadi kubwa ya Madaktari Bingwa kuliko hospitali za pembezoni. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, ameshanipa kibali kama wamezidi niwahamishe ili kuwapeleka ambako kuna shida wakati tukiendelea kusubiri hawa ambao tunawasomesha.

Mheshimiwa Spika, tunatambua ni changamoto kubwa lakini ndani ya miaka miwili itakuwa ni historia chini ya mpango wa *Samia Suluhu Health Super Specialization Program*. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa

3 NOVEMBA, 2022

Wabunge.Tunaendelea na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swalilake.

Na. 46

**Mashamba Makubwa ya Uwekezaji Yasiyotumika
Kuzalisha Mali**

MHE. NOAH L. S. MOLLEL aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani juu ya mashamba makubwa yanayomilikiwa na wawekezaji na hayatumiki kuzalisha mali na ajira nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete majibu.

NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swalilaka Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa yapo mashamba makubwa nchini ambayo yamegawiwa kwa wawekezaji ambapo baadhi ya mashamba hayo yanatumika kwa uzalishaji mali na ajira na mengine hayatumiki kama ilivyokusudiwa. Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine imeanza kushughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wawekezaji kwa kufanya ukaguzi na kuainisha changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata ni kufanya majadiliano na wawekezaji waliobainika kuwa na changamoto ili kuzipatia ufumbuzi kwa pamoja kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji. Kwa mashamba ambayo yametelekezwa, Wizara imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki walioshindwa kutekeleza masharti ya uwekezaji ikiwemo kuyarudisha na kuyapangia matumizi upya kwa manufaa ya umma.

SPIKA: Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swalii la nyongeza.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa naibu kwa Majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutaka kujua, kwa kuwa watu wa Aga Khan kwa maana ya Taasisi ya Aga Khan wanasesma kwamba ninyi Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara nyingine Tano ikiwemo Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani, mnazuia wao wasiendeleze shamba hilo kwa kuwa kuna jambo ambalo hamkulifanya ili waweze kuendeleza shamba hilo. Nini kauli ya Serikali kuhusu taasisi hiyo?

Swali la pili, ni lini utatembelea shamba hilo ili kujua wazi dhahiri shahiri kwamba kuna nini juu ya jambo hilo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe

taarifa kuhusu shamba hili la Aga Khan. Shamba hili wakati linaombwa mwanzo liliombwa kwa ajili ya kilimo, lakini kutokana na maendeleo ya ukuaji wa Mji wa Arumeru Magharibi ikalazimika matumizi ya shamba lile yabadilike na kuwa eneo la kupanga Mji kwa maendeleo ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo kumetokea changamoto baina ya maeneo ambayo yanaendelezwa na hii Taasisi ya Aga Khan na Serikali, hivyo ndivyo mgogoro anaouzungumza Mheshimiwa Mbunge ulipoibuka. Maelekezo ya Serikali ni kwamba, punde tutakapo maliza mazungumzo hayo taratibu nyingine kwa ajili ya uendelezaji zitaendelea.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lake la pili ulikuwa umeshalijibu?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ombi la kwenda kuona shamba hilo ili kuona maendeleo mengineyo. Natoa ahadi kwamba niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge ili kuona na kufuatilia yanayoendelea katika shamba hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu na wewe kuna mashamba Dar es Salaam, swali la nyongeza. (Kicheko)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, ripoti ya sensa ya sasa ya mwaka 2022 imeonesha wazi kwamba ongezeko la watu ni zaidi ya Milioni 16 katika kipindi cha miaka Kumi, hii imeshabihiana

3 NOVEMBA, 2022

sana na wananchi wengi wasio na ardhi kuvamia mapori yasiyo endelezwa kwa miaka mingi.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kufanya tathmini upya ili yale maeneo ambayo hayajaendelezwa na wananchi wako mle wamejenga waweze kurasimishwa rasmi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwangu mimi na upande wa Serikali ninaamini ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mtemvu Mbunge ni jambo nzuri na ni jambo la kufanyiakazi nasi ndani ya Wizara nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tumekwishapokea taarifa ile ya sensa na ndani yake yako mambo mengi sana ikiwemo kuangalia jinsi gani Serikali sasa inaenda kuondokana na maeneo ambayo hayajapangwa vizuri lakini pia kurasimisha maeneo ambayo yameiva kwa ajili ya urasimishaji.

SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mzava,swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa zaidi ya miaka Sita wananchi wa Korogwe wanalia na shamba la Mwakinyumbi liliotolekezwa na Serikali imekuwa ikituahidi lakini hakuna matokeo. Mheshimiwa Waziri ni nini sababu inayoifanya Serikali ishindwe kulifuta shamba la Mwakinyumbi na kuwarudishia wananchi wafanye shughuli za uzalishaji? (Makofii)

3 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mnzava Mbunge wa Korogwe swalii lake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli juu ya shamba hilo ambalo limetajwa na Mheshimiwa Mbunge taarifa zimeshafika Wizarani na taratibu za kiutawala kwa ajili ya kulitwaa shamba hilo na kulirudisha kwa wananchi zinaendelea na tutakapo kuwa tayari tutakupa taarifa za kina juu ya jibu la maombi ya wananchi wa Korogwe.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea sasa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga Mbunge wa Ludewa sasa aulize swalii lake.

Na. 47

Hitaji la Minara ya Simu – Ludewa

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Jimbo la Ludewa pamoja na kuongeza nguvu kwa minara iliyopo iwe 4G?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius kamonga Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Seriakili kupitia Mfuko wa mawasiliano kwa wote UCSAF inaendelea kutatua changamoto za mawasiliano katika Jimbo la Ludewa kwa kushirikiana na watoa huduma wa mawasiliano kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Airtel ambao sasa tayari imewasha minara mitatu katika Kata za Madiru Kijiji la Ilawa, Kata ya Madope Kijiji cha Lusitu na Kata ya Mkongobaki katika Kijiji cha Mkongobaki.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya tiGo ambayo imejenga minara katika Kata ya Lupanga, Kijiji cha Lupanga, Kata ya Mkomang'ombe Kijiji cha Mkomang'ombe na Kata ya Ludewa Kitongoji cha Ngalahawe ambapo mnara unafika katika Kijiji cha Nindi. Aidha, kampuni ya simu ya tiGo ipo katika hatua za kutekeleza mradi wa kufikisha huduma ya mawasiliano katika Kata ya Lupingu na Mkwimbili ambapo changamoto kubwa imekuwa ni namna ya kusafirisha vifaa vya ujenzi wa mnara na kuvifikisha katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, pia Halotel inatoa huduma katika Kata zote za mwambao wa Ziwa Nyasa zikiwemo Makonde, Kimata, Nsele, Ndowa na Igala. Hata hivyo, Serikali inatambua changamoto kubwa ya mawasiliano inayowakabili wananchi wote wa kandokando ya Ziwa hususa ni Tarafa ya Jua. Kwa upande mwingine, TTCL inatoa huduma katika Kata ya Ibumi japo bado kuna

changamoto hasa katika Kijiji cha Masimalavafu. Serikali inatambua kuwa mradi wa uchimbaji wa madini ambao kwa namna moja au nyingine utachangia pato la uchumi kwa nchi yetu. Hivyo, Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote UCSAF inatumia wataalam wake kwenda kata ya Ibumi na kuangalia namna gani ya kutatua changamoto ya mawasiliano hususa ni katika eneo la uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na nguvu ya minara kwenda teknolojia ya 4G. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeanza kutekeleza mradi wa kuongeza nguvu kwenye minara yote nchini iliyokuwa na teknolojia ya 2G kwenda 3G na 4G. Hivyo, minara iliyopo Jimbo la Ludewa itaingizwa katika mradi huo. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga swalii nyongeza.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ninaomba tu kufahamu kwa kuwa nilishamwandikia barua na tumezungumza, ni lini sasa atakuja Ludewa ili aweze kupokea shukrani za wananchi wa Ludewa kwa Mheshimiwa Rais?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kamonga, kama ifuatavyo: -

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ni sikivu na ombi la Mheshimiwa Mbunge tunalipokea na mimi nitaongoozana nae kwenda kuangalia changamoto za wananchi wa Ludewa. Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Takribani wananchi Elfu Sita wa Kijiji cha Katurukira Kata ya Mkula na Kijiji cha Sururu Kata ya Signari hawana mawasiliano mazuri ya simu. Je ni lini Serikali itawasaidia wananchi miundombinu ili waweze kupata mawasiliano mazuri ya simu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mradi wa Tanzania ya Kidigitali (*Digital Tanzania*) na tayari mradi huu tenda yake imeshatangazwa tarehe 20 Oktoba na tarehe 2 Disemba tayari mradi utafunguliwa ambapo Kata na Vijiji vya Jimbo la Kilombero vimeingizwa katika mradi huo. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi pindi mchakato huu utakapokamilika basi ujenzi wa minara utaanza kufanyika rasmi katika Jimbo lake.

SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kata

3 NOVEMBA, 2022

ya Lahoda iliyopo Wilaya ya Chemba ina mnara ambao hauna nguvu, hivyo kuleta shida katika mawasiliano. Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba wanaimarisha mawasiliano ili wananchi wa Kata hii waweze kupata mawasiliano? (Makof)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Chemba tayari tumeshatuma wataalamu wetu kwenda kuangalia changamoto iliyopo katika minara katika Jimbo la Chemba. Kikubwa tulichokuwa tunakiangalia ni aidha kuangalia kama kulikuwa na huduma ya 4G au haikuwepo, lakini kama ilikuwepo na changamoto ni mawasiliano hafifu basi tutahakikisha kwamba tunafanya namna ya kuongeza nguvu katika minara hiyo inayo lalamikiwa na wananchi. Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali itapeleka lini mawasilino ya uhakika ya simu kwa wananchi wa Ushetu hasa katika Kata ya Ulewe, Igwamanoni, Igunda pamoja na Bukomela ambapo wananchi hao bado wanapanda juu ya mti na milimani kutafuta mawasiliano ambayo ni hatari sana kwenye maisha yao.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

3 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cherehani Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata ambazo Mheshimiwa Cherehani amezitaja tayari katika bajeti ya Serikali ambayo ililetwa Bungeni hapa Kata hizo ziliwekwa katika bajeti. Bajeti hii ambayo inaunganisha minara 763 na kama ambavyo nimesema hapo mwanzoni tayari tumeshatangaza tenda tarehe 20 Oktoba na tarehe 2 Disemba itafunguliwa na baada ya hapo ujenzi wa minara hii utanza mara moja. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Yahya Massare swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wakati wenzetu wanakwenda kwenye mfumo wa 4G Jimboni kwangu baadhi ya Vijiji havina kabisa mawasiliano ikiwepo Kijiji cha Mhanga, Kintanula na Kijiji cha Lulanga.

Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi yake ya muda mrefu ya kupeleka minara katika vijiji hivyo?

SPIKA: Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masare kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge tunawasiliana mara kwa mara na hivi vijiji tayari alishanijulisha na bahati nzuri viko katika bajeti,

kilichokuwa kinasubiriwa ni tenda kutangazwa na tenda tayari imeshatangazwa Tarehe 20 Oktoba. Hivyo, tunasubiri mchakato huu ukamilike ili utekelezaji wa mradi huu uanze mara moja. Mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge bahati nzuri tumeshafika katika eneo lake na vijiji ambavyo amevitaja mimi binafsi nimeshafika katika maeneo hayo, kwa hiyo nimhakikishie kwamba hilo ninalifahamu kabisa na Serikali itaenda kutekeleza. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsate sana. Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga Minara ya simu katika Kata ya Makame na Raiseli katika jimbo la Kiteto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halanga, Mbunge Viti Maalum Manyara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna changamoto ya Mawasiliano katika jimbo la Kiteto. Na bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto, ndugu yangu wakili msomi Olelekaita pamoja na Mheshimiwa Asia, kwa kweli tunashirikiana vizuri sana na wao katika kuhakikisha tunatatua changamoto hii. Bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge anafahamu kabisa kuwa orodha ya vijiji vyake vyote viro kwenye bajeti ya mwaka huu. Hivyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Manyoni

pamoja na Kiteto, tuhakikishe kwamba tunashirikiana katika kutoa maeneo ili kukamilisha ujenzi wa miradi hii. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui na wewe unaona mikono ya Waheshimiwa Wabunge wengi bado wamesimama hapo. Hii inaashiria kwamba hii minara ni mtihani. Hebu watie moyo Wabunge, maana wako wengi, hawawezi kupata nafasi wote, hapa ntawapa wachache tu. Hebu sema neno kuhusu Mawasiliano, maana kwa nchi yetu ilipofikia sasa hivi, tunatoa huduma hadi kule Jirani hivyo haiwezekani hapa kwetu tukawa tuna changamoto halafu tunamuona Mheshimiwa Waziri amekwenda DRC Congo kupanua Mawasiliano. Mheshimiwa Waziri hebu sema neno kuhusu Wabunge hawa waliosimama hapa. (makofi)

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA

YA HABARI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba suala la mawasiliano kwa sasa limekuwa ni sehemu ya haki za binadamu. Kwa hiyo Wabunge wana haki ya kutetea haki za wapiga kura wao na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Naibu Waziri ametoa majibu, mara kwa mara kila ilipoulizwa jimboni. Nilishukuru Bunge lako, lilipitisha bajeti hapa ya minara zaidi ya 728 ambayo tenda yake imetangazwa tarehe 22/10/2022 na inafunguliwa tarehe 2/12/2022. Najua watu walitamani baada tu ya bajeti ujenzi uenze, lakini pana process ya kutangaza tenda na kupata wakandarasi. Wabunge wengi katika majimbo yao wamepata minara hii. Wapo waliopata minara kumi, minara saba, minara mitano; na bajeti yetu pia tulitoa orodha.

Mheshimiwa Spika, wito wangu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuangalie kwenye ile orodha ili kama kuna kata ambazo hazina kabisa na hazipo kwenye ile orodha; tunao mradi mwingine ambao tunahangaika kupatia fedha wa minara takriban elfu mbili na mia sita na kitu. Kwa hiyo, baada ya muda hili jambo tutalifikisha mwisho. Nataka niwaombe mvumilie, mchakato unakwenda vizuri na hili jambo tutalimaliza. Ni nia ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha tunamuunganisha Mtanzania kila alipo. Niwaombe tuvumiliane, mradi huu ukikamilika utakwisha.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, kuna minara zaidi ya mia moja na kitu ambayo imejengwa na haijawashwa. Haijawashwa kwa sababu wakati inajengwa tukapata tatizo la corona, uzalishaji wa baadhi ya vipuri ambavyo vingekamilisha uwashwaji wa minara hiyo ulishindikana. Sasa vipuri hivyo vipo nchini uwashwaji wa minara hiyo upo mbioni, na hivi karibuni minara hiyo ikiwashwa yote hali itabadilika. Niwatie moyo Wabunge, tunakwenda vizuri, ikikamilika wote tutafurahia mawasiliano. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, tusaidie, hiyo orodha ya maeneo ambayo yametajwa Wabunge wakaiangalie wapi?

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA

YA HABARI: Mheshimiwa Spika, tulipoleta bajeti yetu hiyo orodha tuliiambatisha orodha hiyo. Ziko orodha za aina mbili, na kwenye vishikwambi hiyo orodha imo. Ukiangalia kwenye bajeti yetu tuliiambatisha orodha ya minara mipya inayojengwa, orodha ya minara ambayo imeisha lakini haijawashwa, pia tumeambatisha orodha ya minara 488 ambayo tunaiongezea uwezo kutoka 2G

kwenda 3G mpaka 4G. Orodha hii ipo kwenye vishikwambi kwa sababu tuliwasilisha Bungeni wakati tukiwasilisha bajeti yetu hapa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri nakubaliana kabisa na wewe. Sasa kwa sababu utekelezaji uko katika ngazi tofauti. Tusaidie hiyo orodha ambayo hili ulilosema Disemba ndilo linaisha, ile orodha tuipate ili Waheshimiwa Wabunge waipate na waweze kuwa wanawambia wananchi wao kule kwamba lini watapata mawasiliano. Kwa hiyo tusaidie ile ya Disemba. (Makofi)

WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA

YA HABARI: Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ipo tayari kuwasilisha hapa Bungeni ili kila Mbunge apate na maeneo yake, pia ni lini utekelezaji wake utakamilika.

SPIKA: Ahsante sana. Wahehsimiwa Wabunge, orodha italetwa Ofisi ya Katibu halafu mtawekewa kwenye vishikwambi vyenu ili sasa yule Mbunge ambaye vijiji vyake vitakuwa havijatajwa, akisimama hapa Naibu Waziri atakuwa anamuuliza kwamba ni lini? Kwa sababu sisi wengine tutakuwa tayari tumeshatajwa mule ndani, kwamba Disemba mambo yetu yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, niliwaona Waheshimiwa Wabunge wote mliosimama hapa, ndio maana nikaona nimwambie Mheshimiwa Waziri na Wizara yake waseme neno.

Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swalı lake.

3 NOVEMBA, 2022

Na 48

RUWASA Nyasa Kupatiwa Gari

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA aliuliza: -

Je, ni lini RUWASA Nyasa itapatiwa gari ili kurahisisha utendaji kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvumi, kwa niaba ya Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI k.n.y. WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuijengea uwezo RUWASA Mkoa wa Ruvuma ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya magari 86 yatanunuliwa na kupelekwa kwenye Wilaya mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Nyasa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, swalii la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kusitiza kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amedhamiria kumtua ndoo kichwani mama, na sasa anasema yuko asilimia 80. Wilaya ya Nyasa ni kati ya

wilaya ambazo bado hazina maji ya kutosha na kuna miradi inaendelea lakini inakosa usimamizi unaostahili kutohana na kukosa gari. Kwa misingi hiyo nashukuru nikiamini kwamba majibu haya hayatakuwa hadithi, tutaisaidia wilaya ya Nyasa ili iweze kuondokana na changamoto hiyo. Gari bovu liloko kule ni vema mkalichukua mlitengeneze au muone namna bora zaidi ya matumizi ya gari ile. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Eng. Manyanya kwa ujumbe huo. Nadhani sasa utampelekea Waziri wa Maji, ujumbe mahususi kabisa kwa ajili ya jumbo la Nyasa.

Waheshimiwa Wabunge, huyu anajibu maswali kwa niaba ya Wizara. Nimewaona mmesimama labda niwape nafasi muulize, halafu Maswali yenu atayapeleka kwa Waziri anayehusika maana hapa hakuna Waziri wala Naibu Waziri wa Maji. Mheshimiwa Catheline Magige.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga Bwawa katika Kijiji cha Wosiwosi Wilayani Longindo, Mkoani Arusha.

SPIKA: Hilo la kwanza nadhani utakuwa umeliandika. Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, RUWASA Meatu nayo kwa kipindi kirefu ina changamoto ya gari.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri nikuombe upeleke kilio hiki cha Wilaya ya Meatu kupatiwa gari ili kuepusha

watendaji kutumia gari la wakandarasi wakati wa kukagua miradi na kutoa certificate.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nalo umelichukua ukampelekee Mheshimiwa Waziri maswali hayo ya Waheshimiwa Wabunge wawili, kuhusu Longido na Meatu. Tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka Serikalini. Nitaleta matangazo niliyo nayo hapa mezani.

Kwanza, ni Tangazo la wageni. tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea na ambao ni washindi wa Dkt. Kimea CUP 2021 kutoka Korogwe Mkoa wa Tanga. Karibuni sana Bungeni.

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Jonas Vanzilent kutoka Jimboni Mvomelo Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana.

Tunao wageni kwa ajili ya mafunzo, tunao walimu na wanafunzi 168 kutoka American and British English Centre ya Jijini Dodoma. Karibuni sana watoto wetu na walimu, tunaamini mmejifunza mawili matatu.

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo lingine kutoika kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo baada ya kusitisha Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa kutakuwa na semina ambayo imeandaliwa na Wizara ya Afya ikizungumzia masuala ya Bima ya Afya kwa wote. Ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema

jana, nirejee tena, ni muhimu sana kuhudhuria semina hii tukitazamia kujadili Muswada unaohusu Bima kwa wote wiki ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa jambo lingine ambalo ni malalamiko ya Wabunge mbalimbali kwa maandishi kuhusu matangazo ya biashara yaliyowekwa humu ndani. Sasa sijui kama wamekabidhiwa kwa mkono ama wameyakuta mezani, sijaua; lakini inaonekana kuna matangazo ya biashara yapo humu ndani. Hairuhusiwi, kwa sababu chochote kinachoingia humu ndani huwa ni lazima kipate kibali. Hata wale wanaokuja kutangaza shughuli zao huwa tunawapa mabanda kule nje na humu ndani huwa wanaingia wao halafu tunawatangaza kama kuna ulazima.

Kwa hiyo kwa yeote ambaye anahisi anahitaji fursa hiyo afuate utaratibu ambao unaruhusiwa. Kwa sababu bila hivyo, humu bungeni kutakuwa kumejaa mambo. Sasa nimeletewa hapa, na kwa sababu sitaki kuanza kutaja ni kipeperushi cha kitu gani, lakini nimeletewa hapa mfano wa kipeperushi kilicho kwenye meza zenu. Kwa hiyo hilo nalo nimeona nilisemee, kwamba hairuhusiwi kuleta matangazo ya biashara hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo; siku ya jana Mheshimiwa Angellah Kairuki alikuwepo humu ndani lakini tulitangaza juzi habari zake na jana kuna Mbunge akawa kama anaitamani nafasi yake hivi. Sasa nimeona, kwa sababu hatopata nafasi ya kuzungumza hapa pengine katika wiki hii, na maswali yanajibiwa na Naibu Mawaziri, kwa hiyo nimpe nafasi awasalimu Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza na Bunge lako tukufu. Kipekee kabla sijaendelea nichukue nafasi hii kuweza kumshukuru Mheshimiwa Samia S. Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa nwangu na kunateua kuwa Mbunge na baadaye kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kipekee nipende kumuahidi utekelezaji wa majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa, weledi na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia niahidi ushirikiano wa dhati Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wengine, Wabunge, Madiwani, Mameya pamoja na Wenyeviti wa halmashauri zetu, lakini zaidi sana na wananchi wetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kipekee nipende kusema maeneo machache ambayo tutaweka mkazo, lakini vile vile kuendelea kuomba ushirikiano wa dhati kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Mawaziri wanakuja na kuondoka, viongozi wakuu wanakuja na kuondoka. Jukumu langu kubwa na wenzangu ni kuendelea kujenga mifumo inayodumu ambayo pia ni endelevu ya kitaasisi. Leo niko mimi lakini kesho atakuja atahudumu Waziri mwingine hivyo uendelevu uwe wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa matumizi mbalimbali katika halmashauri zetu; ni eneo ambalo kwa kweli nitalliwekea mkazo mkubwa katika matumizi mbalimbali mengineyo. Vilevile, matumizi katika miradi ya maendeleo na kuhakikisha kwamba taratibu mbalimbali

za kifedha zinazingatiwa. Jana nadhani kuna Mheshimiwa Mbunge Maimuna Mtanda, kama ntakuwa sjakosea, alizungumzia uwezo wa wahasibu wetu katika halmashauri au waweka hazina wetu katika kufunga hesabu; nashukuru ameweza kuliona. Hili ni eneo ambalo nitakwenda kukaa na CAG ili kuona ni namna gani tunaenda kujenga uwezo na pasiwe na kisisngizio kwa watendaji wote kwamba hajajua taratibu za kimasehabu au kufunga hesabu za halmashauri na mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu kuziba mianya mbalimbali ya upotevu wa fedha, pia kuhakikisha kuwa kuna matumizi sahihi. Kujiridhisha matumizi yanayotumika kwamba kweli ni yale ambayo yanastahili kutumika na si kwamba watu wametumia pasipokuwa na sababu za msingi. Kwa sababu, tukizingatia halmashauri zetu nyingi ni maskini, fedha hizo zinazotumika hovyo hovyo zingeweza kufanya masuala mengine muhimu ya kuweza kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali vijiji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni ukusanyaji na ukadiliaji wa mapato. Ukiangalia katika maeneo mengine katika mwaka wanakadirio wa mapato yao. Zipo halmashauru ambazo zimekuwa zinakadilia kwa viwango cha chini sana, lakini baadaye inapokuja katika makusanyo halisi wanaonekana wamevuka lengo. Hivyo katika mwaka huu wa fedha unaokuja, tutapitia kwa kina halmashauri moja baada ya nyingine ili kujiridhisha ni vipi vyanzo halisi vya mapato katika halmashauri hizo na kuahikikisha kwamba ni kweli wamekadilia kwa kuzingatia aina ya vyanzo ambavyo viro lakini pia kubuni vyanzo vipyta katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kubwa ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Kwa sababu tukitegemea vyanzo hivyo hivyo vya mapato hatutaweza kupiga hatua. Kwa hiyo, tutaona namna gani katika halmashauri zetu waweze kuwapokea vyema wafanyabiasha na wawekezaji ili kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya biashara kwa ufanisi na kufurahia katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, neo lingine ni kusimamia utoaji wa huduma mbalimbali za afya ya msingi na utoaji elimu. vilevile masuala ya barabara tutaendelea kukarabati na kufanya matengenezo wa barabara zetu mbalimbali za mitandao katika wilaya kujitia TARURA na tutaendelea kuomba ushirikiano kwa Waheshimiwa wabunge kuweza kutujulisha pia hali inayoendelea huko endapo kuna kitu hawajardhika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na mengi tutakayoyafanya, tutaendelea kujenga uwezo kwa watumishi wetu ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, yako mengi ambayo tutayafanya, hakuna mapya. Nitaendeleza yale ya watangulizi wangu waliotangulia, lakini vile vile tutakuwa wasikivu kwa kuwasikiliza waheshimiwa wabunge. Jana nilikuwa na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma, leo nitakuwa na Wabunge wa Dar es salaam, kesho nitakuwa na Wabunge wa Mkoa wa Mbeya. Mpaka Bunge litakapokamilika naamini tutakuwa tumemaliza mikoa yote.

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, niwashukuru, na niendelee kuomba ushirikiano wa dhati . karibuni sana TAMISEMI ya wananchi. (Makofii)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kagazi za Ufanisi Kwa Mwaka wa Fedha Ullioishia Tarehe 30 Juni, 2021

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa Kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa Zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha Ullioishia Tarehe 30 Juni, 2021

na

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ullioishia tarehe 30 Juni, 2021

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, ajiandae.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa nikupongeze wewe kwa kazi unayofanya ya kuliongoza Bunge letu. Vile vile nimpongeze Rais wetu kwa kuliongoza Taifa letu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jana wachangiaji wengi waliongelea mambo makubwa ambayo Taifa letu linayapitia. Sisi kama Kamati ya PIC, kazi tunayoifanya ni kupitia uwekezaji wa mitaji unaofanywa na Serikali yetu kwenye mashirika yetu ya Umma. Katika mashirika ambayo yako chini ya TR yanafika zaidi ya 237 na haya yote Serikali inawekeza pesa ya walipakodi kwa lengo la kuboresha hayo mashirika na kutengeneza fedha.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wetu tumepitia mashirika na baadhi ya ripoti za TR na ripoti ya CAG, takwimu zinaonesha kwamba mashirika yetu yanafanya vizuri. Mpaka mwaka 2021 mitaji ambayo imewekezwa na Taifa letu kwenye hayo mashirika inanafikia Shilingi trilioni 67.95. Huo ndiyo utajiri ambao uko chini ya mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ukisoma takwimu, thamani ya uwekezaji wetu katika mashirika haya umekuwa ukipanda lakini ongezeko hilo limekuwa likipungua. Kwa mfano, mwaka 2016/2017 thamani ya mashirika yetu ilikuwa ni Shilingi trilioni 49.6, imeendelea kupanda mwaka 2017/2018 imekwenda Shilingi trilioni 57.79, mwaka 2018/2019 imekwenda Shilingi trilioni 60.3, mwaka 2019/2020 Shilingi trilioni 65.19, na mwaka 2021/2022 Shilingi trilioni 67.79.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukuaji wa ongezeko la thamani ya mifuko imekuwa ikishuka. Tunayo sababu ya kujiuliza, kwa nini uwekezaji unaongezeka lakini ongezeko au ukuaji wa ongezeko unashuka? Mwaka 2016/2017 ongezeko ilikuwa ni 63.8%, mwaka 2017/2018 ilishuka ikaja kuwa 13.6%, mwaka 2018/2019 ilishuka mpaka 8.1%, mwaka 2019/2020 ilibaki pale pale 8.1%, na mwaka 2021 ilishuka ni 4.2%. Tunao wajibu wa kujiuliza kwa nini inashuka hivyo? Tusipojiuliza leo, baada ya miaka miwili au mitatu inawezekana tukaja zero tukaanza kwenda kwenye hasi tusipochukua hatua leo.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia haya mashirika yote, yako chini ya usimamizi wa *Treasure Registrar (TR)*. Ukiangalia sheria inayomwanzisha wa *Treasury Registrar* ya Tanzania ni ya mwaka 1957, ni ya zamani sana, ni sheria kongwe. Imefanyiwa marejeo chini ya *Miscellaneous Amendments Act, 2010*. Ila yaliyofanyiwa marekebisho hayampi *TR* wetu uwezo madhubuti wa kusimamia haya mashirika. Ukiangalia, *TR* anatoa vigezo vyta utendaji wa haya mashirika ya Umma lakini haimpi nafasi; haya mashirika ya Umma yasipotekeleza vile vigezo anavyoviweka, *TR* hana mamlaka ya kuwajibisha haya mashirika ya Umma. Hicho ni kikwazo kikubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tukirejea hiyo sheria ambayo nimeiongelea, ni kongwe, ni ya zamani, na ukiangalia umuhimu wa uwekezaji kwenye haya mashirika, *TR* anapaswa kuwa na nguvu madhubuti ya kuyasimamia haya mashirika. Taasisi yoyote ambayo inashindwa kutekeleza hivyo vigezo alivyoviweka, lazima ayawajibishe ipasavyo, vinginevyo yataendelea kushuka na tutaeendelea kupoteza mitaji yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kuna mashirika ambayo tusipoyaangalia vizuri ni *cash cow* ya Taifa hili. Mashirika kama *TPA*; mashirika mengi ambayo tukiwekeza vyta kutosha, tutaweza kutengeneza mitaji na Taifa litaweza kujitegemea kwenye uwekezaji. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, viko vikwazo vingi ambavyo vinafanya mashirika yetu yasifanye vizuri. Mojawapo ya hivyo vikwazo ni sheria yenewe. Napendekeza Bunge hili liitishe hiyo Sheria ya *TR*, Tuifanyie marekebisho. Kwa upande wangu ningependa tuifute kabisa hiyo sheria tuanze upya, *TR* apewe mamlaka kwenye haya mashirika ambayo anayasimamia, awe na nguvu kiasi kwamba bodi ambazo zinashindwa kufanya vizuri, wakurugenzi ambao wanashindwa kufanya vizuri awawajibishe yeye mwenyewe, akisubiri mamlaka za uteuzi kuteua bodi mpya na kuteua wakurugenzi wapya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mamlaka nyingine, kwa mfano, Ofisi ya *TR Malaysia*, *TR* ana uwezo uwezo mkubwa sana kusimamia mashirika ya *Malaysia*. Ukiangalia performance ya mashirika hayo

yanafanya vizuri kiasi kwamba TR ana uwezo wa ku-suspend mamlaka yoyote ambayo iko chini yake bila kuuliza mtu yeyote. Ana mamlaka ya kufanya hivyo, baadaye anaandika ripoti kwa mamlaka za uteuzi, zinachagua mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, ripoti yetu imebaini pamoja na mambo mengine, kuzorota kwa utendaji wa mashirika ya Uumma kunasababishwa na mambo kadha wa kadha. Mojawapo, limetokea kwenye ripoti ya CAG ukurasa wa 13 kwamba mashirika mengi uteuzi wa bodi unachelewa. Baadhi ya mashirika yanafanya kazi chini ya wakurugenzi ambao hawana bodi na baadhi ya mashirika yametajwa. Kwa mfano, Mfuko wa Kulinda wanyamapor Tanzania; Hospitali ya Rufaa Mbeya, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania. Hayo ni baadhi ya mashirika ambayo yametajwa na ripoti ya CAG. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa ukijiuliza kwa nini tunakuwa na mashirika ambayo hayana Bodi za Wakurugenzi? Mnajua fika, kama taasisi haina Bodi ya Wakurugenzi, Mkurugenzi na Watendaji wote hawawezi kufanya maamuzi ya kuliendeleza hilo shirika, watabaki tu ku-suspend maamuzi kwa sababu hawana chombo cha kuwa-guide. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo limebainika ni mwingiliano wa majukumu kwenye baadhi ya taasisi. Jana nadhani Mheshimwia Dkt. Chaya aliyasema hapa. Baadhi ya taasisi zetu zinaingiliana kimajukumu. Jana ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Chaya alisema, TANROADS na TAA, kwamba tuna mamlaka mbili; tuna TANROADS ambayo kazi yake kubwa na ya msingi ni kutengeneza barabara. Ila hapo nyuma tumefanya maamuzi tukaipa TANROADS kutengeneza viwanja vya ndege, lakini tuna Mamlaka ya Kutengeneza Viwanja vya Ndege ambayo ni TAA.

Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa viwanja vya ndege na usafiri wa anga kwa ujumla, kwa wataalam mnajua, usafiri wa anga unaendeshwa kwa misingi ya Kimataifa pamoja na miundombinu yake TAA na ujenzi wa viwanja vya ndege uko chini ya mamlaka ambayo inaitwa ICAO, ni mamlaka ya Kimataifa. Hii ndiyo inatoa viwango na vigezo. Kama unavyojua TAA inakuwa

3 NOVEMBA, 2022

regulated na Mamlaka ya Usafiri wa Anga. Sasa unashangaa, ukijiuliza huyu TANROADS anajenga viwanga vya ndege kwa mamlaka ipi na kwa vigezo vipi?

Mheshimiwa Spika, nimesikia wakati tunaongea kwenye Kamati, TANROADS walikuja pale, wakasema wamechukua wataalam wote kutoka TAA wamewapeleka TANROADS. Najiuliza, kwa nini uchukue wataalamu kutoka TAA uwapeleke TANROADS? Kwa nini hiyo kazi ya kujenga viwanja vya ndege ambayo kisheria ipo chini ya TAA, wewe unafanya kazi ya kuhamisha watumishi na kuwapeleka kule. Hii inatupa wakati mgumu na inawapa mamlaka za udhibiti wakati mgumu hasa TCAA ambayo imekasimiwa jukumu la kuhakikisha kwamba viwanja vya ndege vinajengwa kulingana na mikataba ya Kimataifa ambayo inatolewa na ICAO kuititia Chicago Convention Annex 14 ambayo inakwambia viwanja vya ndege vijengwe kwa viwango vipi na ubora upi? Sasa hii tumeikasimisha TANROADS.

Mheshimiwa Spika, naomba ujenzi wa viwanja vya ndege urudi TAA na TANROADS wafanye kazi yao ya msingi ya kujenga barabara, siyo viwanja vya ndege. Kuna maeneo wanasema pale kwamba uwanja wa ndege ni sawasawa na kujenga barabara, siyo hivyo. Kila mwaka tunakuwa na ukaguzi amba unafanywa na ICAO, tutakwenda mbele, tutafika wakati ICAO itatu-blacklist, ndege za Kimataifa zitashindwa kuja hapa na tutakuja kufanya marekebisho tumechelewa.

Mheshimiwa Spika, nadhani wakati wa kufanya marekebisho ni sasa, ujenzi wa viwanja vya ndege urudi TAA na TANROADS iendeleee na majukumu yake ya kisheria. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia kwenye kamati zetu hizi tatu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Kamati hizi pamoja na Wajumbe wake kwa kufanya kazi ambayo kwa kweli ni nzuri sana na ripoti zao zimesheheni taarifa za muhimu tupu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kuona kwamba hizi Kamati tatu ni uti wa mgongo wa Taifa letu na kuzitengea muda mwingi ili Wabunge waweze kuzichambua, kushauri na kuisimamia Serikali. Kila siku umekuwa unatuambia tumuunge mkono Rais kwa maneno, lakini kwa kufanya hivi unatuambia tumuunge mkono Rais kwa vitendo kwa kuhakikisha fedha zinazokwenda kwenye halmashauri kwenye mashirika yetu, basi zifanye kazi ambayo imetakiwa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana umesema kwamba umetenga muda mkubwa ili watu waweze kuchangia kwa ustadi, pia umeongeza dakika kwa sababu kikanuni ni dakika 15, lakini mara nyingi tumekuwa tunachangia kwa dakika 10, dakika saba, hata dakika tano pia. Kwa kuona unyeti wa hili suala, umesema tuchangie dakika 15. Tunakupongeza sana kwa kutuonesha unamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa vitendo. Hongera sana. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu wetu, amekuwa mionganoni mwa watu wanaofuatilia fedha zilizotumika kama zimetumika inavyostahili. Tumemwona siku zote, mara zote anaenda kukagua miradi na anagundua vitu ambavyo vilitakiwa kugunduliwa labda na Wakurugenzi na taasisi zetu nyingine ambazo zipo kule, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu anaofuatilia kitu kwa kitu na anaenda kugundua vitu ambavyo unaweza usiamini kama vitu hivi kavigundua Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tunampongeza sana kwa kufuatilia *value for money* kuona fedha inayokwenda inafanya kazi kama ilivyotakiwa. (Makofij)

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, binafsi nianze kuongelea 10%. Kwa nini naongelea 10%? Mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, kwenye ilani yetu tumeongea kwamba tutawawezesha wanawake, vijana na walemvu kwa kuwapa mitaji ili waweze kufanya shughuli zao, lakini nikiangalia *trend*, kama alivyosema jana Mheshimiwa Getere kwamba tunashauri, lakini hakuna kinachoonekana; ukiangalia *trend* mwaka 2016/2017 halmashauri 84 hazikufanya *revolving*. Watu walipewa fedha na hazikufuatiwa ambazo ni Shilingi bilioni 5.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 Shilingi bilioni 10 kwa halmashauri 90. Angalia kila siku inaenda inapanda, baadaye inaenda ikishuka. Mwaka 2018/2019, halmashauri 111 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 13 hazikufanya *revolving* wala marejesho ya Shilingi bilioni 13 hazikurudishwa. Mwaka 2019/2020 zinaenda zinaongezeka, halmashauri 130 hazikufanya *revolving* jumla ya Shilingi bilioni 27 zimeachwa mikononi. Kwa hiyo, kila Wabunge wakiongea, ndiyo kwanza inaenda inaongezeka, haipungui.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021 halmashauri 155 zenyе thamani ya Shilingi bilioni 47 hazikurejeshwa wala hazikufanyiwa *revolving*, wakurugenzi wake wapo, waweka hazina wapo, Maafisa Maendeleo wapo, Serikali haijachukua hatua yoyote. Kwa hiyo, tutegemee 2021/2022 halmashauri zote zitafanya *revolving*, zimebakia 31 tu ndizo ambazo zilirejesha, tena siyo kwa 100%, zilirejesha kwa asilimia chache sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini? Wabunge hapa tunachoongea, hakuna kinachochukuliwa, hakuna kinachofanyiwa kazi, matokeo yake, leo unaongea kwamba fedha zirejeshwe, kila mwaka zinaenda zinapanda mpaka zimefikia halmashauri 155. Tulitegemea zitashuka kutokana na Wabunge wanavyosema, ma-auditor wanavyokagua, Kamati zetu za LAAC zinavyokwenda kule watashusha, lakini ndiyo kwanza kama watu hawajali wala hawafuatili.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia kwa kina hiki kitu, kinaleta ukakasi kabisa kwa sababu halmashauri 83 yenye thamani ya Shilingi bilioni saba, hazikutoa hata hiyo 10%, wakati hapa

3 NOVEMBA, 2022

Wabunge tulipitisha sheria kwamba ni lazima on source 10% wakopeshwe vijana, walemavu na wanawake. Ukijuliza, hizi halmashauri 83 ambazo hazikutoa hii 10% zimechukuliwa hatua gani? Kwa nini na nyingine zisiache kutoa? Kwa sababu hizi zipo, hazijatoa na hazijachukuliwa hatua. Kwa hiyo, tutegemee nyingine nyingi ambazo hazitatoa, zimevunja sheria, na hazijachukuliwa hatua yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaposema tunashauri na tunaongea hamna hatua yoyote, nadhani unatuelewa vizuri, na jana umeongea vizuri sana nadhani unatuelewa. Tunajua kabisa kwamba sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tutaenda kuomba kura na tuliahidi kwenye ilani, tunamwona Mheshimiwa Rais anavyohangaika huku na huku kutafuta pesa ili aweze kutekeleza ilani yake ya Chama cha Mapinduzi. Tunamwona kabisa anavyoshusha fedha kwenye TARURA, kwenye Halmashauri kwa asilimia 100, kwenye RUWASA, yote hiyo anatimiza ahadi walizoziahidi Chama Cha Mapinduzi wakati wa kuomba kura, lakini sisi leo hapa tunaacha tu hivi vitu, tunaviona tu viko kawaida lakini ni vitu ambavyo watanzania wana akili, wanajua na watakuja kuvihoji.

Mheshimiwa Spika, mtaji wa Shilingi bilioni 75 ultumbukizwa mwaka 2020/2021 katika hii *revolving fund*. Hebu tuijulize, Shilingi bilioni 75, zingekuwa zina-revolve, leo hii tungekuwa na Shilingi bilioni karibia 300. Kwa hiyo, watu wetu wangeenda kutoa umasikini kwa kiwango kikubwa, lakini tukubali tumeshindwa kusimamia hizi fedha, zinashuka siku hadi siku. Yaani zimekuwa kama fedha ambazo hazina mwenyewe hivi, yaani watu wanazitumia tu, wanajiita vikundi vya kindugundugu wanapeana, hazirudi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani hili suala sasa Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki ameongea vizuri sana hapa leo, nami Mheshimiwa Angellah namwamini sana, ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi. Kwa hiyo, tumwombe aanze na hili suala kwa sababu linamgusa mwananchi mmoja mmoja wa kule chini. Tunaomba aanze nalo kufanya kazi vizuri kwa ustadi mkubwa

Mheshimiwa Spika, hizi fedha, nashauri zingefanyiwa vitu maalumu, mfano, kule kwetu Tabora sisi tunalima mpunga. Fedha hizi za vijana zingechukuliwa zikajengwa ghala kubwa, ikajengwa mashine ya kukobolea mpunga, vijana hawa wakakabidhiwa ghala pamoja na mashine wakafanya biashara. Moja, wangeajiri vijana wenzao; pili, wao binafsi wangejikomboa na umasikini; na tatu, ile fedha ingezunguka na wengine wangekopa, wakakopa, wakakopa, ikawa fedha ambayo inaonekana inazunguka na vijana wetu wengi wangeweza kufanikiwa, kuliko kuvipa vikundi viwili au vitatu vinaenda vinakula hela, moja kwa moja ile hela haizunguki, hatimaye tunaonekana kama Serikali tuliwadanganya watu wakati wa kampeni, lakini hatufanyi. Kumbe Serikali inafanya kwa uwezo mkubwa sana, lakini hakuna usimamizi unaojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba pesa hizi sasa zirudi kufanya vitu vya kimiradi. Kwa mfano, sisi Tabora tumelima alizeti sana, halmashauri iamue kununua mashine za kukamulia mafuta ya alizeti, ipeleke kwenye vikundi, wakamue alizeti, wakashakamua alizeti, wataawaajiri wenzao, lakini mashine zote zitaendelea kukamua alizeti siku hadi siku na hela itarudi halmashauri. Vile vikundi vitakuwa vinasimamiwa.

Mheshimiwa Spika, tunaangalia kule Mtwara wenzetu wanalima korosho, naona kuna mtu ana kiwanda cha kubangua korosho, ameajiri wanawake kama 200. Hivi zile hela zote zingekusanywa zikanunulia kiwanda kidogo cha kubangua korosho, wakachukua akinamama na vijana, wakaajiri na wanawake wengine na vijana wengine, ile hela ingerudi na ingenunuliwa kiwanda kingine, kingine na kingine. Tungejikomboa katika umaskini kwa hali nzuri tu, tungelipa kodi ya Serikali kwanza, kwa sababu ukishafungua kiwanda utalipa kodi, utaajiri lakini owners wa kile kiwanda watakuwa ni wale akinamama na wale vijana wa pale Mtwara. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, alichukue hili na hizi

pesa sasa ziende moja kwa moja kwenye miradi ya kuwawezesha akinamama na vijana badala ya kumkopeshaa mtu mmoja mmoja na kuona kama shamba la bibi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hili suala tunaloongea wafuatilie, maana tumeshaongea sana lakini hakuna ufuatiliaji na nimekusomea hapa kwenye Jedwali, inapanda kila mwaka. Nimesoma chart one imeandika mchanganuo wa hati ya ukaguzi, ukiangalia paragraph 2.2.1, matumizi yasiyofaa ya akaunti ya Amana (*deposit account*).

Mheshimiwa Spika, kule halmashauri kuna account inaitwa *deposit account*. Kwa mfano, hizi hela za mikopo zinaweza zikaja zikaingia kwenye *deposit account*. Labda zimekuja bilioni tano, wakatoa bilioni nne, wakakopeshaa watu, bilioni moja ikabaki, ikatulia tu. Auditor akija akauliza mbona mmetoa bilioni tatu lakini mlipewa bilioni nne? Wanajibu, tulianza kidogo kidogo lakini baadaye tutazitoa, zikishasahaulika wanazitoa, wanafanya wanavyojuua wao. Nasema hivyo kwa sababu nimefanya kazi halmashauri ndani ya miaka 13, najua.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa ya ukaguzi, imetokea kwamba halmashauri 11, zimeweka kwenye *deposit account* bilioni moja na laki mbili na zimeshindwa kutolewa kwenye *deposit account* na zilikuwa ni hela za kuwakopeshaa akinamama na hazijulikani hizo hela ziko wapi, zimepotelea ndani ya *deposit account*. Hii ni taarifa ya CAG ambayo ameisoma Mwenyekiti wetu wa LAAC. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweza kujifunza kabisa, kwamba account ya *deposit* ni akaunti ambayo ina ushiriki mkubwa katika kupiga hela za halmashauri. For

example, leo tunalipa posho za chanjo za watumishi na watu walienda kwenye semina ya chanjo. Zimebaki milioni 400 zinawekwa deposit, kesho kutwa zinabaki milioni 100 zinawekwa deposit, baada ya muda, zile hela hazionekani deposit wala hazipo. Sasa, huwa najjuliza tu, hawa watu wanaogundulika wamefanya hivi, mwisho wa siku tunafanyaje? Tunawahamisha kuwatoa ofisi moja kuwapeleka ofisi nyingine, wanachukuliwa hatua ili mwingine asifanye tena au tunawaacha tu, tunakuja kuongea hapa Bungeni wanabaki? Nasema hivi kwa sababu wangkuwa wanachukuliwa hatua vitendo hivi visingepanda mwaka hadi mwaka, vingeshuka, lakini vinapanda mwaka hadi mwaka. (Makofi)

Mheshiwa Spika, hivi kweli tumeamua kumsaidia Rais juhudui anazozifanya au tumeamua kufanya kazi, yaani tupo ili mradi tunasema Bungeni, nimeoneka leo Munde nimechangia. Kwa hiyo tunaendelea tu, ripoti ya mwaka 2022 ikija leo halmashauri 155, inakuja halmashauri 160, tunaendelea tu. Nadhani hili suala nimeliongelea kwa makusudi mazima, naamini hili suala litachukuliwa hatua. Kwa mfano, Wilaya ya Buchosa milioni 94 hazionekani, zilikuwa deposit account (akaunti ya Amana). Nimesoma kwenye taarifa ya CAG. Kwa hiyo matendo haya yamefikisha bilioni tisa kwa mwaka 2021 hela ya deposit account. Bilioni tisa inajenga vituo vingapi vyatya afya au inajenga madarasa mangapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana, tumeahidi kwenye llani ya Uchaguzi, bilioni tisa zinapotea, imeandikwa kwenye ripoti ya CAG hakuna kinachoendelea na tunajua kila halmashauri unaweza kuona zimepotea shilingi ngapi za hela ya deposit account, mpaka kufikia bilioni 9.4 ambazo hazionekani zilipo na zilikuwa kwenye akaunti ya Amana. Pale kuna

Mhasibu, Mkurugenzi alikuwepo hata kama amehama, waulizwe zile pesa zimekwenda wapi? Kwa sasa hakuna kinachoendelea na ndiyo maana hivi vitu vinaendelea kufanyika siku hadi siku na vitaendelea kufanyika siku hadi siku tusipokuwa makini. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunajenga Taifa au tunajenga halmashauri ambazo zinapiga hela, ndiyo maana kila siku watu wakisimama wanasema, halmashauri inapiga hela. Naamini kwamba sio watumishi wote wa halmashauri wanapiga hela, wala sio Waweka Hazina na Wakurugenzi wote, lakini wapo wachache ambao wanaenda kuchafua jina zima la halmashauri. Siamini kwamba ofisi zingine za Wizara au za Taasisi za Umma hazifanyi haya yanayofanyika, naamini haya yanafanyika. Kwa sababu sisi tunatoka kwa wananchi na halmashauri zina-deal na mwananchi mmoja mmoja ambao kila siku tuko nao, ndio maana tunaziona kwa macho mengi zaidi hizi halmashauri zetu. Pia, tunapokea malalamiko mengi zaidi kutoka kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niliyosema, nimwambe Mheshimiwa Waziri wetu yupo, tena mwanamke mzuri ambaye ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi tunamfahamu, tumekuwa naye humu kwa muda mwingi, aende sasa akalete mabadiliko ndani ya halmashauri zetu hasa kwa hizi pesa tulizoziyahidi kwenye llani ya Uchaguzi, zitakwenda kuwainua watu kiuchumi. Ahsante. (Makofij)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Vuma Augustine Hole ajiandae.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye taarifa hizi za Kamati ambazo zimewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kabla sijachangia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya katika nchi yetu. Sisi wananchi wa Jimbo la Hai kwa kweli tuna msemo wetu, 'Mama ametuletea miradi kedekede na tunamshukuru sana'. Kila eneo limeguswa na tuna miradi mingi inatekelezwa ndani ya Jimbo la Hai, jambo ambao halijawahi kutokea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze wasaidizi wake wote, nikianza na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Wakuu wa Mikoa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Wakuu wa Wilaya wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Wakurugezi na Watendaji wote, Wenyeviti wa Halmsahauri na Madiwani mpaka Mwenyekiti wa Kitongoji, kwa kweli wote tunashirikiana kujenga nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo makubwa anayoyafanya Mheshimiwa Rais, nimesoma taarifa hizi, lakini natokea Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, hiki kinachoendelea kuhusu Matumizi ya Fedha za Serikali, kimenistua, na kikanifanya nijiulize sana. Dhamira ya hawa wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ni ipi, ikiwa Mheshimiwa Rais anahangaika huko kutafuta fedha, anazileta hapa hiki kinachoendelea huku ni kitu gani, leo tumeona namna amehangaika ameleta hela za UVIKO. Watu wameenda kujificha, yale mapato ya ndani ambayo yalipaswa kutekeleza miradi hayafanyi kazi iliyokusudiwa, maana yake wanajifika kwenye UVIKO na vitu vinavyofanana na hivyo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ukurasa wa sita, utaona mambo yalivyo magumu sasa hivi. Kwanza wamesema ununuzi wa bidhaa za thamani ya shilingi bilioni 7.9 ulifanyika bila idhini ya Bodi, kwamba taasisi zinajиendesha zinavyotaka, mamlaka imeteua Mwenyekiti wa Bodi pale ambaye ni Mteule wa Rais, lakini wao wanaenda kufanya matumizi bila kushirikisha bodi. Hii ni hatari kama tutaiacha.

Mheshimwa Spika, wameenda mbali zaidi, hapa kuna bilioni 3.84, hizi ni ununuzi wa bidhaa ambazo zimenunuliwa bila kuwa kwenye mpango. Hapa halmashauri 24 zimehusika. Ukiogea tena kuna bilioni 5.34 katika halmashauri 39, wamefanya manunuzi bila ushindanishi wa bei. Hizi zote ninazotaja ni fedha, lakini ukienda kuna bilioni 1.2 zimetumika bila kuwa na hati ya kuagiza vifaa (*LPO*) kwenye halmashauri 14. Wamesogea mbali, ununuzi wa thamani ya bilioni mbili bila kushindanisha wazabuni.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kama tutaacha jambo hili. Niliombe sasa Bunge lako Tukufu, kwa kweli tuone namna ya kuchukua hatua, kama hatutachukua hatua hii ni hatari, tutakuwa hatumsaidii Mheshimiwa Rais. Hawa wote ambao wamehusika wawajibishwe kwa mujibu wa sheria, ili iwe fundisho. Naomba kabisa Bunge lako hili Tukufu, safari hii tusiache kuchukua hatua kwa hawa watu. Tutoe maelekezo thabiti ya kuhakikisha Serikali inafanya kazi yake ya kuwawajibisha hawa ambao wamehusika na vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia, mambo yanayofanana na hayo hayo yapo ukurasa wa 11 kuhusu asilimia 10 ambayo inatengwa kutokana na mapato ya

halmashauri. Kimsingi fedha hizi kanuni zinaeleza wazi, sheria inatamka wazi kwamba ukishakusanya mapato yasiyolindwa, asilimia kumi nenda kakopeshe kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. Kanuni inasema kakopeshe 4:4:2 ambaye hatumii *formular* hii, huyu ana jambo bayo na sisi, hamtakii Mheshimiwa Rais mema. Sisi kwenye Kamati yetu ya USEMI, tumesema sana na hizi halmashauri, lakini hawatekelezi kwa sababu wana jambo lao na jambo lao ni hili, halmashauri 154 zimeshindwa kukusanya bilioni 47.01 ambazo zilipaswa kurejeshwa kwenye vikundi.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni nyngi, sisi tumepiga hesabu kwenye Kamati yetu tumebaini karibu bilioni 65 kila mwaka zinatengwa kwenda kukopeshwa. Hizi fedha ni mtaji wa kuanzisha benki kabisa, lakini fedha hizi haziendi kama ambavyo kanuni inataka na hazikopeshwi kwa kuzingatia utaratibu. Sasa naomba, kwa sababu Kamati yako ya USEMI tumekuwa wabobezi sana kwenye eneo hili. Tupe fursa twende ndani tupate muda wa kutosha, tukuletee taarifa sahihi kwenye asilimia hii 10 tu; kwa sababu hizi ni fedha nyngi ambazo kusudio la Serikali ni fedha hizi zikasaidie kule chini: pamoja na kwamba tumeshashauri hapa, sheria hiyo iletwe, ifanyiwe marekebisho ili kundi la wanaume nao wanufaike. Sasa kama kundi hili linapokwenda kunufaika kama hatuna mechanism ya kusimamia na tunaletewa na CAG taarifa hii, hii sio sawa, hatumsaidii Mheshimiwa Rais kwa namna hii.

Mheshimiwa Spika, wameenda mbali, wamesema bilioni 1.2 zimetolewa kwenye akaunti ya Amana bila kuzingatia utaratibu. Wamesogea mbele zaidi wamesema, halmashauri 17 zimetoa mikopo, bilioni 3.26 bila uwiano unaotakiwa kwa maana ya 4:4:2.

Wanafanya hivi sio kwa bahati mbaya, siyo kweli. Kuna taarifa tulikuwa tunaletewa unaambiwa halmashauri nzima hakuna walemavu, siyo kweli, halmashauri nzima hakuna watu wenyе sifa, siyo kweli. Nia ikiwa njema kukiwa na utayari wa kumsaidia Mheshimiwa Rais, hivi vitu viro na wenyе mahitaji ni wengi mno, hatuwezi kusema kwamba kuna fedha zinaweza kurudi kwamba hazikutumika.

Mheshimiwa Spika, sasa nishauri kwenye eneo hili, nafahamu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMi amekuja vizuri na ameanza vizuri na wamezindua mfumo ambao utatusaidia kwenda ku-control, wameshauzindua mfumo wa kieletroniki ambao utajumuisha Tanzania nzima. Wale waombaji wataingia kwa *NIDA* zao, maombi yao na vikundi, kwa kweli umeonyesha vizuri. Hata hivyo, bado nasema kwa kuwa fedha hizi ni nyingi na hao wanaoandaa mfumo huu tuliwashauri kwenye Kamati washirikiane na e-government, ili ku-control, namna ya kudhibiti. Bado tunahitaji kutafuta proper mechanism, bilioni 65 sio ndogo, lakini lazima tutafute mechanism ya hizi fedha ambazo zimeachwa hazijakusanywa ziweze kurejea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nirejee kukuomba tena Kamati ya USEMI na LAAC ziungane pamoja ziende kwenye mambo haya ya msingi, zikatazame hizi asilimia kumi, zikatazame kuna kitu kinaitwa bakaa kwenye taarifa za halmashauri. Wanafanya mambo yao, mwishoni unakuta bakaa milioni 35, halmashauri ndogo kabisa, halafu hizi zinaenda kutumika, wakati mwingine hata Waheshimiwa Madiwani hawashiriki. Ndio maana Bunge lilitopitwa Madiwani hawa tuwatazame, tuwape nguvu, tuwawezeshe ili waweze kuzisimamia vizuri halmashauri zetu. Bila kufanya hivyo hivi vitu vinapita,

unakuta bakaa milioni 60, hii inaitwa bakaa, Madiwani walishamaliza kazi yao, hao wanaenda kupanga mapato na matumizi kadiri wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba nihamie kwenye eneo lingine ambalo lilizungumza hapo jana kuhusiana na eneo la uwekezaji, tumepitisha mabadiliko ya sheria, lakini bado kuna changamoto. Kwa halmashauri zenyé mapato machache ambayo ni wanufaika na mpango wa uwekezaji. Wale wawekezaji kuitia mfumo wa EPZ, wanakuja kwenye halmashauri zetu, wanalipa centrally kwa Serikali Kuu, zile halmashauri kule chini hazinufaiki. Kwa mfano, Jimbo la Hai, asilimia 78 sisi tunategemea kilimo na ufugaji, anakuja mwekezaji kuitia mashamba ya ushirika, anachukua anaweka mashamba ya kupanda maua kama mwekezaji kuita mfumo wa EPZ, pale Halmashauri ya Hai hachangii chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unakuta maeneo yetu, ukienda kule kuna wawekezaji wengi wana mashamba huku na huku, lakini halmashauri haipati kitu. Naomba turejee, watakapoenda kuandika kanuni, waseme kwamba na sisi halmashauri zillzopo kule, hawa watu wawajibike kwetu. Hata zile bodi zilizoundwa pale zimeeweka *level* ya Kitaifa kwenye *level* ya ngazi ya halmashauri hakuna kitu. Hakuna mwakilishi wetu, sasa sisi ambao tunapokea ile miradi mtu anaweka shamba la maua pale, sisi ndiyo tunampa maji, sisi ndiyo tunamsaidia kila kitu lakini halipi kodi. Niombe sana hili litazamwe kwa jicho la huruma, kwa sababu halmashauri nyingi ambazo zinahusika na maeneo ya uwekezaji zinaenda kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja nizungumze jambo ambalo lilzungumzwa jana hapa kuhusiana na KADCO. Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro ni mali ya Serikali, mwanzoni kulikuwa na wabia mbalimbali pamoja na KADCO, lakini Serikali ilinunua hisa zile na kwa mkopo wa CRDB na ikalipa. Kwa hiyo, picha iliyopo ili tusichanganye wananchi wa Jimbo la Hai ambao kule kuna suala linaendelea chini ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, wakadhani uwanja wa ndege sio mali ya Serikali, naomba tuweke sawa hapa. Ule uwanja ni mali ya Serikali, eneo lile ni mali ya Serikali, mradi unaoendelea pale ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna changamoto ya yule anayeendesha pale kwa maana ya msimamizi na anaye-run ile activity, KADCO, tuone namna ya kuutunza vizuri ili tusiwachanganye wananchi wakaona kwamba ule uwanja sio mali ya Serikali. Ni vizuri hilo likawekwa sawa, uwanja ule ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kama nakosea utanielekeza namna gani ya kufanya, lakini taarifa sahihi ni hizo ili tusiwachanganye wananchi kwa sababu kuna suala la fidia linaendela.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nisisitize tu, hiki kitu kinachoitwa bakaa, Waziri atakapokuja kusimama hapa, atutolee mwongozo kwamba, huu utaratibu wa kubakisha hela kwa makusudi fulani, maana yake ni nini na atoe maagizo sahihi kwenye jamobo hili.

Mheshimiwa Spika, lingine, kumekuwa na ubadilishwaji wa matumizi wa fedha za Serikali kwenye hizi halmashauri zetu, wanakuja hapa, wanaleta bajeti, tunaipitisha hapa, nendeni mkajenge madarasa kadhaa. Tunawapitishia kwa asilimia 100, wanaenda

wanakusanya. Hili tena niseme hapa, upo ujanja sasa hivi, kila halmashauri utaambiwa imekusanya zaidi ya asilimia 100. Ukija kwenye utekelezaji wa miradi hawatekelezi, hawapeleki fedha na hizi asilimia 100 zinawekwa kimkakati, halmashauri ina uwezo wa kukusanya bilioni tatu, watakuambia tunakusanya bilioni mbili ili wafikie malengo haraka na wasifiwe, lakini hata wale walioshindwa hawapeleki fedha.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI iende ku-review mifumo ya kupeleka makadirio ya makusanyo kwenye halmashauri zetu. Kuwe na vipimo ambavyo ni bayana vyatuhusu kupeleka haya, vinginevyo tutaumiza halmashauri nyingine ambazo zinafanya kazi na hili la bakaa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kubadilisha miradi pasipo kufuata utaratibu, wanafanya *reallocations* ya funds. Kwa mfano, sasa hivi tulikuwa tunaangalia fedha zilizokuwa zimepelekwa za UVIKO na fedha nyingine ambazo zimepelekwa kwa ajili ya kujenga zile shule za kidato cha tano na sita. TAMISEMI imepeleka fedha, kila halmashauri inasema hazitoshi, kwanza kabla hawajenga na ukiwaliza hebu tuambieni, ukiwaliza TAMISEMI hii BOQ mlio peleleka huku ndugu zetu mlikuwa mnakadiria ifanye kitu gani na sasa mnasema fedha hazitoshi, tuleteeni basi BOQ ya kusema hapa sisi tunaongeza bilioni mbili au milioni 200. Kwa mfano, Halmashauri ya Bahi, wao wamesema milioni 58, wengine 150, wengine 200, fact za ki-engineer zipo wapi na ukienda kuangalia hizo unakuta ramani inasema jambo lingine, yaani ramani inasema ina milango nane, ukienda kwenye BOQ kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema, pamoja na kwamba tulishauri kwenye Kamati nasema hapa ili

Mheshimiwa Waziri akaweke mikasi mikubwa ya kuwabana hawa watu, wafanye kazi kwenye uhalisia, warudi kwenye neno lao, wanasema ni wataalam wafanye kazi kitaalam ili tuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, niombe, sote tunaijenga nchi yetu, kila mmoja aliyepo hapa, tusiposhirikiana na kupenda nchi hii na kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa dhati, hakuna mtu mwingine atatoka nje ya Tanzania kuja kufanya kazi hii, huu wajibu ni wakwetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga hoja zote mkono na mchango wangu ndiyo huu. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu umelizungumzia hili jambo la KADCO na kwamba linaweza kuwachanganya wananchi, ukasema mimi nikuongoze, huo ndio uhalisia, Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro ni wa Serikali, ambacho kinazungumzwa hapa ndani hakina uhusiano kabisa na umiliki wa kile kiwanja cha ndege. Kinachozungumzwa hapa ndani ni msahangao kwamba kama ni wa Serikali KADCO inafanya nini pale? Kwa hiyo wananchi waelewe hivyo kwamba uwanja ni wa Serikali na mambo yote yanayoendelea huko kwa ajili ya maboresho ya ule uwanja yanafanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Huu mshangao tutamalizana nao tutakavyomaliza hizi Kamati na wao watatuelewa vizuri, ila kwa sasa wajue tu kwamba kinachoendelea na pia uwanja ule ambaou po kwenye Jimbo la Hai ni wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshamwita Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ili kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza kabisa nami naomba nitoe pongezi kubwa sana kwa Kamati zote ambazo zimewasilisha ripoti zao ili tuweze kuzijadili, kwa sababu wamewasilisha ripoti ambazo kwa kweli wamewasilisha vizuri sana nasi tumeweza kuzitambua na tunaweza kuzichangia vizuri. Moja kwa moja nami nianze na Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya ufanisi wa mfuko huo unaonyesha kwamba kuna vikundi 155 havikurejesha mikopo ya Bilioni 47 iliyotolewa katika vikundi mwaka 2019. Pia umebaini kwamba kuna mamlaka 83 za Serikali za Mitaa hazikuweza kuchangia jumla ya Shilingi Bilioni 6.26 katika vyanzo vyao vya mapato. Hili jambo siyo dogo, kumekuwa na hoja nyingi sana katika utoaji wa hii mikopo, Bunge letu lilitunga sheria ya utoaji wa ile asilimia 10, asilimia Nne kwa akina mama, asilimia Nne kwa vijana na asilimia Mbili kwa watu wenye ulemavu, sasa ni kwa nini sheria hii haitekelezeki? Kwa nini Halmashauri zinakuwa hazitekelezi hizi sheria, siku zote tumekuwa tukizungumzia hili jambo katika hili Bunge. Tumekuwa tukiuliza maswali tunaona yanajibiwa lakini bado tatizo linaendelea, zikija hoja bado tunaona hoja zile zinajirudia mara kwa mara. Kuna baadhi ya Halmashauri hoja zimejirudia miaka saba, kumi, au miaka mitatu ni kwa nini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zingine tunaona kwamba zinatoa fedha hewa katika vikundi, Halmashauri nyinginezo zinatoa fedha chini ya kiwango ya mikopo na Halmashauri nyinginezo zinabadilisha matumizi ya hizi fedha. Ipo haja Serikali sasa ipendekeze adhabu kwa Halmashauri ambazo hazitekelezi hii sheria ambayo tumeitunga wenyewe hapa Bungeni, kwa sababu imekuwa kila siku tunaongea lakini hakuna adhabu yoyote inayotolewa pengine ikitolewa leo adhabu hizi fedha zitaweza kutekelezeka na kila Halmashauri itatendewa haki, na wananchi wetu inapotolewa hii mikopo maana yake sisi tunapigania kwamba Serikali ilikuwa inayo nia njema kabisa kuhakikisha kwamba wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu waweze kukopeshwa ili ilete tija.

Mheshimiwa Spika, naomba nami niungane na watu wa Kamati kwamba sasa ipo haja kuwepo na akaunti maalum ya hizi fedha za kutoa na kukusanya. Itakukwa rahisi sasa kui-monitor ili iweze kuleta manufaa zaidi. Pia kuwepo na mpango mahsus wa wanufaika kupatiwa elimu, kwa sababu bila elimu tumeona kwamba vikundi vingi sana vinapewa hii fedha lakini hawana elimu hata ya kuweza kufanya biashara ambazo wanapatiwa.

Mheshimiwa Spika, tumeona sasa hivi, tunavyo Vyuo vya VETA, tunavyo Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu na Mikoa yetu, ni kwanini sasa elimu isitolewe katika hivi vyuo vya VETA? Tumeona vijana wengi sana wanamaliza vyuo vya VETA bado hawana mkakati wowote hata wakisaidiwa kupewa hii mikopo ya vijana, mpaka vijana muda mwingine wanajishughulisha kwenye bodaboda hata wengine hawakupenda kukopa hizi bodaboda lakini kutokana na pesa ndogo sana ambayo vijana wanakopeshwa na akina mama. Unakuta

kikundi kimoja kinapatiwa labda mkopo wa Shilingi Milioni Mbili akina mama 20 au vijana 10 wanapatiwa mkopo wa Milioni Tatu, matokeo yake wanaona bora tukinunua bodaboda tuzungushe ili iweze kutusaidia. Bado kungekuwa na mkakati, vijana wanaomaliza vyuo vya VETA, wamesoma wapatiwe mashine badala ya kupatiwa fedha, wanaweza wakapatiwa hata mashine ya kufyatua tofali, wakapatiwa mchanga, simenti na baadae Halmshauri iweze kuchukua ijengee labda shule na hospitali. Utaona hawa vijana watakuwa na uhakika wa kulipa ule mkopo kuliko ilivyo sasa hivi vijana wanapatiwa fedha hawana elimu au utaalam wowote wa kuendesha hizi fedha na matokeo yake zinashindwa kurudishwa kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwamba sasa hivi vijana wamesomea mambo ya uvuvi, wamehitimu masomo ya mifugo na kilimo, hizi fedha bado baadhi ya Halmashauri tunapata fedha nyingi sana kwa ajili ya kilimo au uvuvi au mifugo. Kwa nini vijana wasipatiwe elimu ya ufugaji wa samaki, wakajengewa bwawa, wakanunuliwa samaki, wakapatiwa vyakula halafu baadae wakianza kurudisha tena kuna masoko mengi wakapatiwa hata hayo masoko, Kwa hiyo Halmashauri zinakuwa na uhakika kwamba hizi fedha ni lazima zitarudi kwa sababu ni *revolving fund* ambazo mtu akirudisha, vijana wengine wanakopa au akinamama wanakopa na watu wenye ulemavu pia.

Mheshimiwa Spika, kwa watu wenye ulemavu kuna miradi maalum ingetengenezwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kwa sababu tumepitisha kwamba mlemavu mmoja mmoja anaweza akakopa ama walemvu wawili. Sasa kungekuwa na miradi maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu wapatiwe vifaa na pia wasaidiwe

kutafuta masoko ili iweze kuwasaidia kuliko ilivyo sasa hivi tunapoteza mapato makubwa bila sababu lakini kumbe nia ya Serikali ilikuwa nzuri sana kuhakikisha kwamba tunawasaidia watu wenyewe ulemavu, akinamama na vijana ili ulete tija. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tulifanya ziara na tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri ambae ameteuliwa sasa hivi Mheshimiwa Angella Kairuki, alipokuwa Katibu wa Wanawake kwenye Chama chetu hiki cha Wanawake hapa Bungeni, alitutafutia ziara nyingi sana kwenda kujifunza miradi ya akina mama. Kwa mfano, tulikwenda China, Uingereza na sehemu nyingi sana, tulikuta pale China akina mama wana miradi mikubwa sana kwa sababu wanavyo viwanda vidogovidogo vya ndani, sasa ifikie sehemu hata Halmashauri zetu, badala ya kuwapatia pesa tuwapatie viwanda vidogovidogo ambavyo kila nyumba ikiwa ina viwanda tayari hata ajira kwa vijana tutatengeneza ajira nyingi sana hata wenyewe tutajiajiri kwa kutumia viwanda vidogovidogo ambavyo viko katika Halmashauri zetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tayari Halmashauri zetu zitapata chanzo cha mapato kwa sababu watalipa kodi za Halmashauri pia tutaongeza pato katika nchi yetu na ndivyo ambavyo hata Wachina wenzetu wanafanya vitu vingi ni kwa sababu badala ya kuwapatia fedha wanawapatia viwanda vidogovidogo ambavyo viko katika nyumba zetu wenyewe. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nilikuwa nataka kuchangia ni kuhusu uteketezaji wa madawa ya binadamu kwenye vituo vya afya na katika hospitali zetu. Taarifa ya CAG ya mwaka 2020/2021 inaonesha kuwepo

kwa wimbi kubwa kabisa la uteketezaji wa madawa. Kitu ambacho mimi nimejifunza hapa, utaona hivi vituo vya afya na Hospitali za Wilaya, Mkoa zimekuwa zinalipia madawa kule MSD lakini unakuta kwamba haya madawa yanacheleweshwa kuletwa kwenye hospitali zetu kwa muda mrefu kiasi kwamba sasa muda mwingine yakiletwa inakuwa muda wa matumizi umekwisha. Kwa hiyo, matokeo yake sasa madawa yanateketezwa, kunatakiwa kuwepo na fedha tena ya kuteketeza hayo madawa. Vilevile tatizo kubwa wananchi wanakwenda kutibiwa, wanaandikiwa dawa na dawa hazipo. Huo ni uzembe, tunapoteza mapato makubwa wananchi wakitegemea kwamba watapata huduma za afya lakini matokeo yake hawapatiwi huduma za afya, dawa zinateketezwa na fedha za Serikali inaliwa, matokeo yake tunaletewa hoja kubwa kwa Serikali, hakuna kinachofanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilisahau kusema, tulivyokwenda China, tuliambiwa kwamba wao watu wanaoiba fedha ya Serikali adhabu yao ni kuuawa lakini sisi kwa sababu ya haki za binadamu hatuwezi kufanya kitu kama hicho, tufanye kitu kikubwa ambacho kitasababisha watu wawe na nidhamu ya matumizi ya fedha ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri zetu. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, mimi ninaomba uteketezaji wa hayo madawa....

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, hebu hapo kwenye mchango wa China na watu kuuawa na haki za binadamu hebu paweke vizuri.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nimesema hivi: tulipokwenda China kuangalia miradi ya akina mama, tulipokuwa tunapewa ripoti kwamba wao China, watu wakiiba fedha ya Serikali adhabu ni kifo, lakini kwa sababu Tanzania hatuna adhabu ya kifo kwa sababu ya haki za binadamu, basi angalau tutoe kitu kikubwa kitakachowafanya hawa watu wanaoiba mali za umma, wapewe adhabu kali ambayo itawafanya hata wananchi waone kwamba sisi wananchi tunachangia pato la nchi lakini watu ambao wanafanya uhujumu wa hii fedha kweli wanapatiwa adhabu ambayo inasababisha wananchi turidhike na kile wanachokifanya. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, nilikusudia kusema hivi kwa sababu unazungumzia nchi, watu kuuawa, Bunge lisielekezwe upande huo, kwa hiyo huo mchango wa China na kuua watu, hata sisi tunayo adhabu ya kifo haijafutwa, tunayo adhabu ya kifo ila siyo kwa haya unayoyazungumzia. Kwa hiyo, hii habari ya China na mfano wa wao kuwa wanaua watu naamini na wao wanafuata utaratibu kama ambavyo na sisi tunayo adhabu ya kifo. Kwa hiyo, mchango wako hapo uondoe kwenye Hansard halafu weka hoja yako ni nzuri tu, inaenda vizuri sana bila huo mfano. Ahsante sana.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba basi Hansard iweze kutoa mambo ya kifo lakini kupoteza mali ya umma siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni kuhusiana na michango ya NHIF. Kuna mapato mengi sana yanapotea. Yanapotea kwa sababu gani? Tumeona jana kuna Mheshimiwa Mbunge

alizungumza kwa uchungu sana kwamba hata akinababa wanaambiwa kwamba wamejifungua iko kwenye madai yao kwamba wanaume wamejifungua na fedha ipo imekatwa *NHIF*. Tumeona sasa hivi wanao utaratibu mzuri sana, unatoa taarifa kwamba umetibiwa katika kituo fulani. Sasa kwa nini wasiseme kwamba wametibiwa kwa mfano, mimi labda nimetumia kadi yangu ya *NHIF* kwenye hospitali hata ya *private*, sasa niambiwe kwamba nimetumia kiasi gani? Kwa sababu tunaona kama kuna mapato mengine mtu anasingiziwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mfano wa Mbunge mmoja alikwenda kutibiwa kwenye kituo cha afya, alipokwenda kutibiwa kwenye kituo cha afya, ana *ulcers* tu, akapewa dawa za *ulcers*, baadae akapigiwa simu kwamba ulikuwa umelazwa? Akasema sijalazwa lakini inaonesha kwamba amelazwa siku saba, katumia *drip*, wakati alikuwa ametumia dawa tu na mfano hai upo, Mbunge aliyepigiwa simu yupo. Kwa hiyo, *NHIF* basi ingekuwa wanafuatilia wanatuletea hizo taarifa za matibabu yetu pamoja na *bills* tumetibiwa kiasi gani itakuwa rahisi, hata kama sisi wenyewe Wabunge saa nyingine tunakwenda kutibiwa kwenye Mkoa mwagine basi taarifa ziletwe Bungeni kwamba Mbunge fulani katibiwa sehemu fulani na gharama zake ni kiasi hiki itakuwa rahisi hata kufanya reconciliation kwamba Bunge letu, Wabunge tumetumia kiasi hiki kuliko ilivyo sasa hivi, mtu unalimbikiziwa gharama ambazo zisizo zinakwenda kwenye Mfuko matokeo yake wanaua Mfuko bila sababu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninaomba Serikali yetu iangalie huu Mfuko kwa sababu ni muhimu na tunaenda sasa kupitisha Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya lakini kama kutakuwa hakuna control yoyote ya matibabu ya

watu wanavyotibiwa itakuwa haina maana yoyote kwamba nia nzuri ya Serikali inakuwa inapotoshwa. Watu wachache wasifanye watu wakaichukia Serikali yao kwa sababu ya vitu vidogo sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikushukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa anazozifanya. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan ajiandae.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla kwa mambo mengi ambayo anayafanya, *to be specific*, mambo makubwa matatu: Jambo la kwanza ni ujenzi wa barabara za kiwango cha lami kwenye Mkoa wa Kigoma unaendelea kwa kasi kubwa sana, hizo ni barabara mbalimbali, pia ujio wa Umeme wa gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma ni historia kubwa na ya kuenziwa. Pia mpango wa kujenga SGR kuelekea Kigoma ambao bado upo kwenye hatua ya manunuzi ni jambo la kujivuna na la kihistoria. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nitaenda kwenye hoja ambazo ziko mezani. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja zote. Baada ya hapo nianze na Benki ya Kilimo. Naanza na Benki ya Kilimo kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wamejiajiri kwenye sekta ya kilimo,

hii ni sekta ambayo inabeba Watanzania walio wengi kuliko sekta yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu kwenye bajeti tulitenga Bilioni zaidi ya 700 kwenye bajeti ya Kilimo ukiondoa Bilioni 150 ambazo zimetolewa kama ruzuku. Tume ya Umwagiliaji tulitenga zaidi ya Bilioni 361, sasa ukiangalia Wizara wamejipanga vizuri kuweka miundombinu vizuri sana kwenye upande wa umwagiliaji na sehemu zingine. Wanaweza wakajenga miundombinu vizuri kwa maana ya umwagiliaji, wao hawatalima wataenda kulima wakulima, lakini wakulima wetu hawa wa Tanzania uwezo wao wa kifedha ni mdogo mno.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya benki nyingi zinatangaza kwamba zinakopesha wakulima lakini hazifanyi hivyo, benki nyingi hazikopeshi wakulima. Ni Benki moja tu ya Kilimo ndiyo ambayo imefanya kwa vitendo kuwakopesha wakulima kiwango kikubwa cha fedha, wengine wanafungua dirisha lakini ukienda wanakuambia hatujaanza kutoa mkopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina ushauri, katika hizi Bilioni 361 ambazo zimetengwa kwa ajili ya umwagiliaji, kwa nini tusipeleke Bilioni 250 kwenye umwagiliaji halafu Bilioni 100, tukaenda kuwapa hawa TADB - Benki ya Kilimo ili wakulima kama Serikali ikiweka miundombinu vizuri, wakulima wawe na uwezo wa kwenda kukopa ili waweze kuendesha kilimo, otherwise unaweza ukajenga mifumo vizuri, miundombinu mizuri ya kilimo lakini baadae wakulima sasa wakawa wako weak halafu ikawa ni *white elephant*.

Mheshimiwa Spika, nitaenda kwenye zao la pamba. Mwaka 2019 kidogo tuingie kwenye mkwamo kwenye

zao la pamba, nakumbuka vizuri ulikuwa Naibu Spika, wakati ule zao la pamba lili-drop sana duniani na tulikuwa tunaelekea kwenye uchaguzi, presha ilikuwa ni kubwa sana Kanda ya Ziwa, Wabunge wa kule walikuwa matumbo joto. Hivi inakuwaje, inakuwaje! Pamba hainunuliki huko chini. Serikali iliwaita wafanyabiashara wa pamba, tena ambao karibia wote ni Watanzania. Ilivyowaita iliwapa assurance kwamba wanunue pamba kwa bei elekezi ya Serikali halafu Serikali itaenda kuwa-compensate au kuwapa ruzuku. Mpaka tunavyoongea hivi toka 2019 mpaka leo 2022 hawa wafanyabiashara wanadai zaidi ya Bilioni 21. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, suala la kutengeneza mjasiriamali Mtanzania ambaye ataenda kwenye *level* hiyo ya kuombwa na Wizara aweze kunusuru hali, siyo kazi ndogo! Hawa waliopo wachache Watanzania tujaribu kuwalinda na kuwatetea. Serikali inapata kigugumizi gani cha kuwalipa fedha zao? Wakati wanawaita Serikali ilitumia maneno mazuri sana ambayo ni very promising, sasa kwenye utekelezaji, yaani kukopa ni furaha halafu kulipa ni matanga. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hapa iko sababu na iko hoja, lazima Serikali ichukue hatua. Tulipata nafasi ya kukaa na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo, wanasema ooh! kuna vikao. Mimi nasema kama hawa watu walivyoitwa 2019 na wao wangesema ngoja kwanza tuna vikao, mwaka wa kwanza kikao, mwaka wa pili kikao, tungeendelea na benki yetu, hivi nani angweza kutuondoa kwenye huo mkwamo? Iko sababu ya msingi na iko hoja ya haraka hapa, Serikali ihakikishe inalipa madeni hayo haraka iwezekanavyo ili kuweza kutowaingiza kwenye mgogoro wa kiuchumi hawa

wafanyabiashara wetu wa Kitanzania wazalendo, ambao walitutoa kwenye mkwamo wakati ule. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wa Kamati yangu wamezungumza suala la mwingiliano kwenye taasisi hizi ambazo tunazisimamia Kamati ya *PIC*, tunalo Shirika la Marine Services ambalo zamani ilikuwa chini ya *TPA* lakini sasa hivi ni linajitegemea lenyewe, ziko mali za marine services nyingi ambazo *TPA* wanazing'ang'ania ziko kwao, inaifanya marine service iwe weak ishindwe kuwa na kipato kizuri, ishindwe kupanga mambo yake vizuri kwa sababu mali zake nyingi zimeshikiliwa na *TPA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilete hapa, kama ni *point* za kisheria tuweze kufanya mabadiliko ya kisheria ili marine service wapewe mali zao waweze kujengeka vizuri. Walikuja kwenye Kamati wanalamika, wanaomba msaada.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu bodi za mashirika mbalimbali. Kwanza mimi na-*discourage* sana kuwa na bodi hizi za ushauri. Mimi nadhani ni vizuri, na kwa taasisi kubwa kama *TANROADS*, *TANROADS* ambayo kila mwaka tunawapa ma-trilioni ya shilingi hapa, lakini wana bodi ya ushauri tu. Ipo tofauti kati ya bodi ya ushauri na *independent board*. Hii bodi ya ushauri sana sana ni kumshauri Waziri tu basi, lakini hii *independent* inao uwezo wa kupanga vitu na kuvisimamia bila kuingiliwa na mtu yoyote.

Mheshimiwa Spika, sasa kuwa na hizi bodi za ushauri kwenye taasisi nyeti kama hizi hiyo kwanza mimi na-*discourage* sana. Hata hivyo, lipo suala la ucheleweshaji wa uteuzi wa bodi. Mimi nakumbuka Machi Mheshimiwa Rais alikuwa anapokea ripoti ya CAG, CAG akasema

kwamba yako mashirika mengi ambayo hayana bodi. Mheshimiwa Rais alishtuka pale, akasema mimi nikiletewa kila kitu pale huwa hakikai hata siku mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa ziko bodi nyingi ambazo zimekuwa miaka mitatu au minne. Kuna sheria fulani hivi wanasema eti bodi ambayo ina zaidi ya watu 10 ikiisha muda wake eti majukumu yale anachukua Katibu Mkuu wa Wizara. Yaani Katibu Mkuu wa Wizara kichwa kimoja kianze kubeba vichwa 10 vya bodi nzima? ni mambo ya ajabu kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado amepewa mwaka mmoja kwa mujibu wa sheria, hata huo mwaka unaisha bodi haijateuliwa. Sasa nashindwa kuelewa kwamba nchi hii Tanzania kweli hatuna wajumbe wa bodi, watu milioni 61 hatuna wajumbe wa bodi na wenyeviti wa bodi ambao wanaweza waka-fit kwenye hizi taasisi ambazo hazina bodi?

Mheshimiwa Spika, ninaomba, kama tunataka kunusuru mashirika yetu ni lazima tuhakikishe kwamba tunapata bodi kwa wakati. Kwa sababu bila kuwa na bodi, tumeona mashirika yenyе bodi na yasiyo na bodi utendaji wao ni tofauti kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini, baada ya kupata bodi, hata hao wenyе bodi ukiangalia hakuna mfumo imara wa uwajibikaji. Shirika kupeleka gawio Serikalini yaani ni mpaka wajisikie. Hakuna sheria ngumu ambayo inawalazimisha kupeleka gawio; na ndiyo maana akisimama Mheshimiwa Rais akiwakaripia akitoa tamko kali kuhusu kupeleka gawio, gawio linapanda, asiposema gawio linashuka. Hatuwezi Kwenda namna hiyo, lazima tuweke utaratibu mzuri wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Kairuki ulivyompa muda wa kusalimia, akasema anaweka mifumo mizuri wizarani pale ili hata akiondoka yeye, ibaki inafanya kazi. Sasa hata hizi bodi zetu hizi lazima tuziwekee utaratibu ambao utawalazimisha, kwamba mkishindwa kufikia *level* hii ya mafanikio kwenye shirika fulani basi bodi ivunjwe. Hata utaratibu wa kupata hawa watendaji wakuu wa mashirika tunaweza tukawaangalia pia.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukaweka utaratibu, mtu anatakuwa Mkurugenzi wa TANESCO ruhusu watu waombe, watu waombe ukurugenzi wa TANESCO halafu Mheshimiwa Rais apelekewe majina atue; maana inawezekana labda ukateua mtu labda hataki. Maana kuna mtu mwingine unamwita kwenye Kamati, anakuja pale unaona yaani nia ya ndani ya kusaidia shirika hana kabisa, yupo tu pale anakula posho basi. Ukimuuliza mpango mkakati hana, kama ipo haitekelezeki, yaani hasaidii chochote Serikali. Mimi nadhani tuunde utaratibu waombe hawa watu, tutafute watu *competent*, waombe, wakishaomba baadaye apelekewe Mheshimiwa Rais kwa mamlaka yake atue. Haya mambo wakati mwingine, maana tuko watu wengi kidogo...

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa nani kasimama, Mheshimiwa Mtaturu, Mheshimiwa Vuma Holle kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mtaturu.

TAARIFA

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba ni jambo zuri kuwa na bodi katika mashirika, katika taasisi kwani bodi hizi zina nafasi kubwa sana katika kutoa ushauri. Naomba achukue taarifa kwamba taasisi imara kama za Simba zina bodi ambayo inaongoza mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Vuma Augustino Holle unapokea taarifa hiyo.

MHE. VUMA A. HOLLE: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri mmoja, kama utaratibu wa kupatikana kwa bodi umekuwa ni mgumu kidogo pale ambapo bodi zimemaliza muda wake, tumetoa ushauri hapa; labda wale wajumbe wateuliwe kwa muda tofautitofauti, si wako wanne, leo teua wanne, halafu mwakani teua wanne, ili kwamba hawa wanne wakimaliza wanne wabaki wana-save. Au tuletewe sheria tubadilishe, tuseme kwamba bodi hata kama ikimaliza muda wake kwa mujibu wa utaratibu, kama haijatumbuliwa basi iendelee kufanya kazi mpaka pale ambapo bodi nyingine itakapopatikana na si kuacha tu Katibu Mkuu pale eti ameshikilia. Kuna bodi zingine unashangaa wamemaliza vizuri unakaa hata mwaka baadaye wanarudishwa walewale, sasa maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tuweke utaratibu, watu kama huwataki watumbue waondoke, lakini kama

hujawatumbua muda wao umeisha hujaleta wengine wapya, Serikali iwaache waendee kukaa kama bodi ili waweze kuteua watu wengine.

Mheshimiwa Spika, nataka niguse kidogo kuhusu Bodi ya Mikopo. Pale Bodi ya Mikopo, mimi juzi nilikuwa napitia ripoti ya CAG, nikagundua hata walivyokuwa wanamgomea Waziri wao kwa kweli sijashangaa. Ukipitia ile ripoti ya CAG vizuri huwezi kushangaa kwa nini Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilikuwa inamgomea Waziri wake, kwamba ile kamati yake hawataki kuipa ushirikiano, yaani huwezi ukashangaa.

Mheshimiwa Spika, watakuja kusema wenyewe kwa sababu umewaita. Lakini madudu yaliyoko kwenye ripoti ya CAG kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni jambo serious na ambalo mnahitaji kufanya hatua za haraka sana; na ndiyo maana hawataki kuchunguzwa maana ukiwachunguza utaona madudu yao. Lakini CAG ameshatusaidia kuyaonyesha yatima hawapati mikopo, maskini hawapati mikopo, wanatoa hela excess ambazo hawatakiwi kutoa, zaidi ya nilioni tano. Sasa unataka uambiwe na nani kwamba hawa watu hawafai?

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, tunao utajiri mkubwa sana kupitia mashirika haya, hayawezi kuwa operated kama mashirika ya *Private Sector* lakini yapo mambo ambayo tunaweza tukakopa kule tukayaleta kwetu, tukabdalisha sheria zetu kama ndicho kikwazo ili tuhakikishe tunaweza kwenda kwa speed ambayo Mheshimiwa Rais anaitaka. Mheshimiwa Rais anasema kazi iendelee lakini yako mashirika ambayo hayaendani na kauli mbiu ya Mheshimiwa Rais.

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja nashukuru sana sana. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela atafatiwa na Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema; lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Taarifa ya Kamati ya LAAC na taarifa zingine.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na shukrani kama sitaanza kwa kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu shupavu jemedari Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kipekee nimpongeze yeye mwenyewe binafsi. Hii ni kwa sababu ya utashi wake na dhamira yake aliyokuwa nayo katika kutekeleza au kutatua changamoto za wananchi wake. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia Hassan anafanya kazi kubwa sana, kazi ambayo hakuna mwananchi wa nchi hii hazioni. Amekuwa na dhamira njema kabisa ya kuhakikisha kwamba kila palipokuwa na changamoto, changamoto hiyo inatatuliwa. Pamoja na dhamira hii njema kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo zinazoweza kupelekea matarajio haya ya Mheshimiwa Spika yasifikasiwe.

Mheshimiwa Spika, kumeripotiwa makosa, changamoto mbalimbali au dosari mbalimbali na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika ripoti zake. Dosari hizi

zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara, mwaka hadi mwaka hali ambayo imesababisha baadhi yetu kufikiri kwamba ripoti hizi hazina majibu au hazina suluhisho, jambo ambalo sio kweli.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi ukiziangalia kwa umakini kabisa unaweza ukakuta kwamba zinatatulika. Nataka niziangalie changamoto chache tu kama mfano.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa changamoto zilizokuwa zikiripotiwa mara kwa mara na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni kama ifuatavyo: -

Kumekuwa na matumizi mabaya kwenye akaunti ya amana. Hapa pamekuwa na kizungumkuti kwa sababu akaunti ya amana si akaunti ya halmashauri. Akaunti hii ni imewekwa kwa ajili ya kutatua migogoro ya kimkataba wakati panapotokea changamoto; kwa hiyo pesa zinazowekwa kwenye akaunti hii zinaweza kutumika kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na manunuzi yasiyozingatia taratibu. Hiki ni kichaka kikubwa sana kinachotumika kupoteza fedha za wananchi kwa makusudi kabisa. Hapa kuna mambo mengi sana. Kunakuwa na kutokushindanisha kandarasi, hali kadhalika kunaweza kukawa na mtu mmoja amekusanya document zote, akitaka kutengeneza kandarasi anajitengenezea mwenyewe lakini mtu huyu akapewa tender. Kwa maana hiyo mara zote yeye atakuwa ndio mpataji wa tender hizo. jambo hili limekuwa ni gumu sana hususan kwa watu ambao wako makini katika suala zima la manunuzi.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na changamoto katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Fedha nyingi zimebekwa katika maeneo ambayo hayana tija. Mara nyingi watu wamekuwa wakijiamulia kutengeneza mradi pasipokufata taratibu kama vile kufanya *visibility study*; pia bila kujua hata *break-even point* itafanyika kwa wakati gani au itatokea lini. Mambo mengine ni kama vile halmashauri kushindwa kukusanya madeni ya mikopo ya vikundi ambavyo imevikopesha. Kuna pesa nyingi sana zimekopesha na halmashauri kwenye vikundi vyatia mama, vijana na watu wenye ulemavu lakini imekuwa ni shida sana urejeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, kuna vitu vingine ambavyo vinaweza vikakushangaza zaidi, kama vile ujazaji wa fomu. Kama suala la kujaza fomu tu limekuwa ni changamoto ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa sana upotevu wa fedha katika halmashauri. Fedha nyingi sana zimekuwa hazipewi halmashauri kwa kisingizio hiki. Pia kuna tatizo hili la uteketezaji wa dawa. Nchi kama Tanzania yenye mahitaji makubwa sana ya dawa inashangaza sana inapofika wakati kwamba dawa zinateketezwa eti kwamba zime-expire.

Mheshimiwa Spika, sasa, haya yote ni matatizo ambayo kama tusipokuwa makini yataendelea kujitokeza na kuendelea kupoteza fedha za wananchi walipa kodi, wavuja jasho pasipokuwa na mafanikio yoyote wala kuwa na matumaini kwamba mambo haya yatarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo, kwamba mambo haya yanaweza yakatekelezeka. Kutokana na taarifa za ripoti ya CAG kumekuwa na

ushauri mara nyingi jinsi gani ya kuenenda kutatua changamoto mbalimbali nilizojaribu kuziorodhesha hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama halmashauri ikijielekeza katika kujengea uwezo kamati zake zile za halmashauri hapa patakuwa na tija. Shida iliyopo kamati hizi zimekuwa dhaifu kiasi kwamba panapohitajika kwenda kukagua miradi mbalimbali haziwezi kukagua miradi hiyo. Aidha ni kutokana na uelewa wa wanakamati au wakati mwingine vitendea kazi vya Kwenda kukaguliwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lkage alipendekeza na mimi naendelea kusitiza na kukumbusha kwamba kamati za halmashauri zitumike kikamilifu. Kwanza zijengewe uwezo wa kutosha kusudi waweze kuwa na uwezo wa Kwenda kukagua vizuri. Lakini kwa sababu Kamati ya Fedha na Kamati ya Ujenzi ni kamati ambazo zinahusika au zina mahusiano ya moja kwa moja na masuala ya pesa basi kamati hizi zitambuliwe kuwa ni kamati maalum za ukaguzi wa miradi na pesa za maendeleo katika halmashauri. Halmashauri iwajibike kwa namna yoyote kutenga pesa ambayo itaiwezesha kamati hizi kufanya kazi kikamilifu. Ikitokea kamati zimeshindwa kufanya kazi kutokana na upungufu au kutokana na uzembe wa halmashauri kuitengenya fedha basi halmashauri inatakiwa iwajibike.

Mheshimiwa Spika, kamati hii ipewe jukumu la kutengeneza ripoti ya miradi ya maendeleo na pesa za maendeleo. Ripoti ieleze waziwazi kiasi gani cha pesa zimepokelewa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Kwa mfano vyanzo vya maendeleo kutoka Serikali Kuu, kutoka kwa wafadhili; lakini pia ieleze chanzo cha maendeleo kinachotokana na mapato yake yenye.

Mheshimiwa Spika, vilevile kamati hii katika ripoti hii iielezee waziwazi kila akaunti; kwamba akaunti hizi zilizopo zina bakaa ya kiasi gani. Hali kadhalika kamati hii ni lazima iweze kujadiliwa na Baraza la Halmashauri. Baada ya ripoti hii kujadiliwa iunganishwe pamoja na ripoti ya ukaguzi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupelekwa kwenye vikao vya LAAC kwa ajili ya kuendelea kutumika katika matumizi ya vikao hivyo. Jambo hili litakuwa limetengeneza *check and balance* katika maeneo yote ya halmashauri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linaweza likainusuru halmashauri ni suala la ajira. Mapendelekezo mengi sana yametolewa mara kwa mara pamoja na Khaji akipendekeza kwamba ajira katika halmashauri husika lazima zizingatie weledi. Watendaji katika idara mbalimbali, hali kadhalika katika vitengo na Mtendaji Mkuu lazima wawe na ueledi, kwamba lazima wawe na ujuzi wa vitengo ambavyo wanavyovisimamia, pia wawe na ujuzi husika wa idara wanazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mtendaji Mkuu lazima apimwe kutokana na *performance* kwa maana ya uwezo au kwa kile alichokitimiza katika eneo lake la kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litafanya kila mtu awajibike na pia awe na ajira ya mkataba pamoja na wale viongozi wa vitengo wawe na ajira za mikataba. Hii itasaidia sana kuwafanya wawajibike wakihofia kwamba kama hawatafanya vizuri watakatishiwa mkataba wao au hawatapewa mkataba mwingine.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limejitokeza ambalo linahusiana moja kwa moja na Wizara ya

TAMISEMI, halikadhalika Wizara inayoshughulika na masuala ya utoaji wa fedha. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kwamba fedha zile za maendeleo haziendi kwa wakati. Jambo hili limeleta changamoto nyingi sana kwa sababu unakuta fedha zinaenda zikichelewa na wakati mwingine zinakuwa hazitoshi hali ambayo mipango iliyotarajiwa katika miradi ya maendeleo haifanikiwi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kumekuwa na changamoto kwamba pesa ile ikienda imechelewa miradi haifanikiwi. Mfano mkubwa unaonekana hata sasa hivi, fedha yetu ya Majimbo haijaenda. Kwa hali ilivyo, kama itakwenda kwa kipindi hicho cha baadaye, maana yake, kwa vyovoyote vile fedha hii itakuwa imechelewa na kushindwa kutekeleza mambo yaliyokusudiwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza kuzungumza kule mbele kwamba changamoto nyingi sana zinazoonekana katika *level* ya Halmashauri ni zile ambazo zinaweza zikatekelezeka lakini zikatibika pia. Hivyo tunayo kila sababu ya kumsaidia Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan katika kutekeleza yale anayodhamiria yatokee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. (Makof)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Profesa Mbarawa, ajiandae.

MHE. MAIMUNA A. PATHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia hoja. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wake na leo hii tunaweza kuhudhuria Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Rais wetu kipenzi, Mheshimiwa Mama Samia Suluhi Hassan kwa kazi yake kubwa anayoifanya kwa awamu hii. Mama huyu ametoa fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali katika Halmashauri zetu. Ametoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya, ametoa fedha nyingi kwa ajili ya umaliziaji wa maboma mbalimbali, kwa ajili ya ujenzi wa shule, madarasa na mambo mengineyo. Mwenyezi Mungu ambariki sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Halmashauri. Tumebaini udhaifu mwingi sana kwenye ripoti ya CAG kwenye halmashauri zetu. Kwanza kuna udhaifu mkubwa katika usimamizi wa maeneo ya ununuzi na mikataba. Kama tunavyofahamu kwamba eneo la manunuzi linatumia fedha nyingi sana za Serikali, ni zaidi ya asilimia 70 ya pesa zote za nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, ndiyo maana Serikali ikaona ni vyema Bunge litunge sheria kwa ajili ya matumizi ya fedha hizi za manunuzi. Kuna *Public Procurement Act* ya 2011 pamoja na *Regulation* yake ya mwaka 2013. Lengo kubwa ilikuwa ni kudhibiti fedha hizi za Serikali ili zitumike vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kusikitisha na kushangaza sana kwenye halmashauri zetu hili eneo limekuwa ni bovu kweli kweli. Kuna fedha nyingi za Serikali zimetumika isivyo. Inaonekana kuna halmashauri 42 zilitumia fedha zenye thamani ya Shilingi bilioni 7.93 bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Kwa kweli hapa nashindwa kuelewa. Hivi unafanyaje manunuzi bila kupitisha kwenye Bodi ya Zabuni? Hapa kuna question mark, huu

unawezekana ukawa ni mpango wa makusudi wa kutaka kutumia vibaya na kutumia tofauti fedha ya Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia kuna halmashauri 24 zilifanya ununuzi wa Shilingi bilioni 3.84 bila kuzingatia Mpango wa Manunuvi ya Mwaka. Kwenye Taasisi zote za Serikali ikiwemo halmashauri, huwa tunakaa, tunaandaa *procurement plan* ya mwaka husika. Unapoona kuna matumizi ya dharura yamekuja, labda kuna fedha zimekuja, mnatakiwa mwombe kibali maalum kwa matumizi hayo, na pia mnatakiwa muweke kwenye nyongeza ya mpango wenu wa manunuvi. Unapoona haya hayafanyiki, tunaanza pia kuwa na question mark kwamba fedha hizi hazikutumika kihalali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia kuna Halmashauri 39 zilifanya ununuzi wenyewe thamani ya Shilingi bilioni 5.37 bila kuitisha nukuu za bei (*competitive tendering/competitive quotation*). Ni kitu cha kushangaza kama hujaitisha nukuu za bei, umempataje huyo mzabuni kwenda kuleta bidhaa katika halmashauri? Hapo panaonesha kuna upendeleo, rushwa na ubadhilifu wa fedha za Umma. Haiwezekani mimi kama *procurement officer* nimekaa ofisini kwangu nikaamua kampuni 'X' ije ifanye kazi ya Ujenzi, au Kampuni 'Y' ije ifanye kazi ya kuleta bidhaa fulani, hiyo siyo sahihi na haikubaliki. Moja kwa moja inaonesha kwamba kuna rushwa ndani yake, kuna upendeleo na ubadhirifu wa mali za Umma. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia kuna baadhi ya halmashauri 21 zilinunua bidhaa ya Shilingi bilioni mbili, lakini cha ajabu ziliingizwa kwenye *ledger* bila Kamati ya Mapokezi kuzikagua bidhaa hizo. Pia hapa kuna ukakasi ndani yake. Sheria inatutaka tunaponunua bidhaa zozote au

huduma yoyote accounting officer aunde Kamati Maalum kwa ajili ya Ukaguzi na mapokezi ya bidhaa hizo. Ni ajabu, inaonekana baadhi ya halmashauri wanapokea kinyemela hivyo vitu, mtu wa *procurement* ameagiza yeye na anapokea yeye na anaingiza kwenye *ledger* yeye na ana-issue yeye. Hii haikubaliki. kwanza tuna wasiwasi, inawezekana hizo bidhaa hazikufika ipasavyo au hazikufika kabisa au hizo huduma hazikufanyika na ndiyo maana Kamati ya Mapokezi na Ukaguzi haikufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia kuna halmashauri wanafanya ununzi wa bidhaa mbalimbali au huduma mbalimbali kwa kuwatumiua wazabuni ambao hawajasajiliwa GPSA. Hili ni kosa kubwa kwa Sheria za Manunuzi. Ina maana mtu anaamka tu nyumbani kwake asubuhi anaenda kupanga, leo nitachukua Kampuni 'Z' ilete bidhaa fulani. Hiyo siyo sahihi, kwa sababu manunuzi haya ni ya Serikali, yana sheria na taratibu zake, siyo kama manunuzi ambayo tunayafanya majumbani kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache tu kwanza Kamati ilibaini kwamba kuna upendeleo, udanganyifu na ubadhirifu wa mali za Umma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, inashangaza pia kuna halmashauri nyingine ilionekana imenunua vitu lakini haijaingiza kwenye *ledger* na wala hawaja mu-issue *local fundi*. Kuna mizania ambayo iko tofauti kwenye hizi force account, watu wanataka kuzitumia vibaya hizi force account. Haiwezekani mimi nimenunua labda mchanga au nimenunua matofali halafu fundi anayajengea bila mimi kumkabidhi. Sidhani kama hiyo ni sahihi. Hapa pia kuna ukakasi, inaonekana kuna mambo yanaenda

ndivyo sivyo kwa dhamira ya makusudi, kwa nia potofu na nia ovu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunachoomba Wabunge, ushauri wetu, watu wanaofanya haya mambo, wachukuliwe hatua kali kwa haraka. Tatizo linaonekana kwamba, kama mtu amefanya kosa mwaka 2022, inafika mwaka 2023, 2024, 2025 issue ni ile ile moja haijachukuliwa hatua, kwa kweli hii haikubaliki na ndiyo maana watu wengi wanaendelea kufanya mambo haya wanaona kwamba zile sheria za kinidhamu hazichukuliwi kwa haraka. Vilevile tunapendekeza kwamba ifanyike hivyo, haya mambo yatapungua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna uteketezaji wa dawa za binadamu katika vituo vinavyotoa huduma ya afya. Hii inasikitisha sana. Kuna vituo vya afya, zahanati na hospitali hazina dawa. Hivi inakuwaje mpaka dawa zinafikia wakati wa kuteketezwa? Kuna sheria inaruhusu, kama mimi kituo 'X' nina dawa za ziada/za nyongeza, nimeona labda baada ya miezi mitatu zinaweza ku-expire au miezi minne, ninaruhusiwa kuwapa zahanati 'Y' hizo dawa. Kwa nini wasipeane hivyo? Kwa nini kama unajua kwenye eneo fulani hayo magonjwa siyo mengi, upeleke dawa ziwe nyingi?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwa sababu inaonekana kuna fedha nyingi zimetumika kununulia dawa hizo ambazo wananchi wetu wanazihitaji, lakini baadaye zinakwenda kuteketeza. Hiki nacho ni kichaka kingine, tunatakiwa tukiangalie sana, haikubaliki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia kuna maeneo manne ambayo Kamati imeyabaini ambayo ni mianya ya upotevu wa mapato ya halmashauri. Vilevile kuna ushuru

wa huduma (*service levy*), inakusanya bila uthibitisho wa mapato halisi ya kampuni ya mwaka (*turnover*). Hiki kitu siyo halali, inabidi kifuatiliwe. Kuna halmashauri nyingine zinafanya malipo bila kukata kodi la zuio (*withholding tax five percent*).

Mheshimiwa Spika, hii ni fedha ya Serikali ambayo inatakiwa itumike kwa ajili ya Serikali, lakini cha kushangaza, mzabuni analipwa fedha yake kama kawaida, inakuwaje halmashauri usikate hii kodi ya zuio ukairudisha TRA ili iweze kutumika na Taifa letu? Huu ni mwanya mwingine wa matumizi mabaya ya fedha ya Serikali. Pia tumebaini kuwa kuna halmashauri nyingine zinafanya malipo bila kutumia risiti ya *electronic*. Hiyo ni kosa kisheria.

Mheshimiwa Spika, pia inaonekana kuna halmashauri nyingine zinaendelea kutoa leseni mbalimbali za biashara nje ya mfumo. Pia hicho ni kichaka kingine. Vile vile kuna baadhi ya stahiki za watumishi kutolipwa ipasavyo. Rasilimali watu ndiyo msingi wa utendaji wa mafanikio ya taasisi yoyote, lakini rasilimali watu usipoitendea haki kuna matatizo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, inaonekana kuna watumishi wengi wa halmashauri wanadai stahiki zao; wengine wanadai malimbikizo ya mshahara baada ya kupanda cheo, lakini hawapati kwa muda mrefu. Hiyo ipo sana, na mimi mwenyewe ni mfano halisi nikiwa mtumishi wa Serikali, nilipokuwa Serikalini, nilifanya kazi, nikapanda cheo, lakini nilikaa zaidi ya miaka sita bila kulipwa arrears. Hiyo inashusha morali na ari ya kufanya kazi. Kwa sababu hiyo ni haki yao, tunaomba TAMISEMI na Serikaki kiujumla iangalie eneo hilo.

3 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kuna wafanyakazi wengine wanahamishwa; kwa mfano, anahamishwa kutoka Wilaya ya Buchosha unampelewa Wilaya nyingine. Mtumishi huyu ana familia na mizigo yake, anatakiwa alipwe stahiki yake, lakini unamwambia aripoti ndani ya siku saba au siku 14 aende pale lakini fedha yake haumlipi, anaendaje kule? Hii nayo inashusha morali ya kufanya kazi vizuri. Tunaomba wafanyakazi hawa walipwe stahiki zao vizuri ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika,....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. MAIMUNA A. PATHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ajiandae.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kwa kuungana na waliotangulia kuchangia kumshukuru Mheshimiwa Rais hasa kwa kazi kubwa anayofanya ya kutuletea miradi mingi kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kujieleza kwenye chimbuko halisi, chimbuko lenyewe la Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Mamlaka ya Serikali za Mitaa chimbuko lake tutakumbuka wote wakati wa Ukoloni Serikali za

Kikoloni zilianzisha mamlaka hizi na waliziita Local Authorities, lakini walizigawanya kwenye makundi takribani matatu na zinazotuhusu Waafrika waliziita Native Authorities.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini Tanzania, Hayati Baba wa Taifa mwaka 1997 aliamua kuziondoa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Baadaye miaka ya 1982 aliona umuhimu wa kurudisha Mamlaka za Serikali za Mitaa na zikatungwa sheria mbili za Bunge; Sheria za Serikali za Mitaa Mamlaka ya Wilaya (Sura Na. 287) na Sheria za Serikali za Mitaa Mamlaka ya Miji (Sura Na. 288).

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika mwaka 1998 tukawa na Sera ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Dhana ilikuwa ni kutengeneza mazingira wezeshi kwa wananchi na ugatuaji wa mamlaka ulikuwa unakusudia kwamba wananchi washirikishwe moja kwa moja kupitia mamlaka zao pale kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata halikadhalika mpaka ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa ya CAG ukurasa wa tisa, taarifa inaeleza kwa habari ya udhaifu katika uwekaji wa mitaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Taarifa nimeitolea mfano, Manispaa Jiji la Dar es Salaam wamewekeza hisa takribani 24,036,348 kwenye Benki ya DCB zenyе thamani ya Shilingi bilioni 5.77, lakini taarifa inaendelea kusema kwamba Benki hii utendaji kazi wake hauridhishi. Sasa udhaifu huu chanzo ni nini? Naomba nianze hapo.

Mheshimiwa Spika, leo hii hakuna mwongozo, sheria hata kanuni inayoweza kutoa mwelekeo au kuelekeza halmashauri namna gani zinaweza kufanya uwekezaji. Tuanze hapo. Hatuna mwongozo, sheria, au kanuni

inayoelekeza namna gani halmashauri zetu nchini zinaweza zikawekeza mitaji. Ameendelea mbele zaidi akatolea mfano Jiji la Dodoma kwamba hapo awali ndani ya Jiji la Dodoma; ukisoma ule ukurasa wa tisa kuna mfano bora, mzuri wa Jiji la Dodoma kwamba limejenga Hoteli ya nyota tano pale Mji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze hapo. Jiji la Dodoma sisi tilijiongeza tu wakati huo na nitangaze maslahi, nikiwa nahudumu kama Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma. Nianze bajeti sasa, nitoe mifano ya namna gani mlolongo wa namna gani mapato ya ndani yalikuwa yakikua mwaka hadi mwaka hadi mwaka. Mwaka 2015/2016 bajeti ya Jiji la Dodoma ya Manispaa ya Dodoma bilioni 4.5 na makusanyo yalikuwa bilioni 3.6. Mwaka wa Fedha 2016/2017, makisio yalikuwa bilioni 3.9 na makusanyo yalikuwa bilioni 4.8 wakati huo, tukatumia bilioni 1.8 kupeleka kwenye miradi ya maendeleo, hapo awali ilikuwa ni ngumu hata kujenga choo cha shule ya msingi kupitia mapato ya ndani, tulianzia hapo. Mwaka wa fedha 2017/2018, makisio yalikuwa bilioni 20 kutoka bilioni 3.9, tukakisia bilioni 20 na tukafanikiwa kukusanya bilioni 25, tuka *break even*. Kwa nini tulikisia bilioni 20 kutoka bilioni 4.8?

Mheshimiwa Spika, tulikisia hivyo kwa sababu, mtakumbuka mwaka 2017 Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliondoa iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (*CDA*) na yenyewe ilikuwa na bajeti yake. Sasa mwezi Disemba tukafanya mapitio ya bajeti, wao bajeti yao tukaingiza kama bilioni 13 ambayo inatokana na viwanja na ya kwetu ikawa bilioni saba ikawa bilioni 20, lakini viwanja vile havikuwepo, ilikuwa ni bajeti tu kama bajeti. Tukavipima, ndio vikapatikana na tukapata hiyo bilioni 13 na tuka-*break even* kwa bilioni 25.

Halikadhalika sasa mamlaka ya upangaji ikawa jiji kwa maana ya manispaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2018/2019, tukakisia bilioni 67, kutoka makusanyo ya bilioni 25, tukakisia bilioni 67, tuka-break even, tukakusanya bilioni 71. Tukasema viwanja muda unavyokwenda maana yake itafika mahali soko litapungua na sisi karibu asilimia 70 ya mapato tunategemea viwanja na ndio ilikuwa fursa kwetu Dodoma. Badaye nitarejea namna gani halmashauri nyingine zinaweza kufanya hivyo kwa fursa ambazo zipo huko.

Mheshimiwa Spika, tukasema hapana, Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi, sasa haya mapato ya bilioni 71 yatakuwa sustainable? Jibu likawa hapana, *sustainability*, yaani uendelevu wa mapato hayo utafika mahali utashuka kwa sababu chanzo cha ardhi kikipungua hatuwezi kufikia hayo malengo. Tukakaa na *management team* yetu tukakubaliana tutafute uwekezaji ndani ya Jiji la Dodoma. Tukaona fursa pekee Dodoma, watumishi wanahamia, watu mbalimbali wanahamia, tukasema tuanzishe hoteli. Tujenge hoteli na hii miradi ni ya kimkakati, lakini pia tujenge nyumba za kupangisha watumishi, tulikuwa tunafikiria hivyo ili hii fursa tuitumie kama Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, tukaanza na hoteli. Pale Mji wa Serikali ule mradi uliitwa *Government City Complex* na lengo lilikuwa ni kujenga miradi mbalimbali hadi *shopping mall* pale. Kwa phase one tumefanikiwa kujenga hoteli ya bilioni 18. Naomba niweke sawasawa hapo, phase one ni bilioni 18, ile hoteli inayoonekana pale Mji wa Serikali na ni hoteli yenye hadhi ya nyota tano. Kama haitoshi tukatumia tena bilioni tisa kwa mapato ya ndani, sio

mkopo wa benki wala fedha kutoka Serikali Kuu, tukajenga hoteli nyingine mkabala na White House, ukumbi wa pale Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi ya bilioni tisa.

Mheshimiwa Spika, hii yote ilikuwa ni mikakati ya kuhakikisha kwamba, mapato yetu, *demand* ya viwanja ikipungua maana yake sasa hii inakwenda kuwa mbadala wake. Leo hii hoteli hizo nadhani wanatafuta operators ili zianze kuleta fedha.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini? Ni kweli kuna udhaifu mkubwa kwenye namna ya miradi inayoanzishwa kwenye halmashauri, kwa nini? Hoja ileile, hatuna sheria, mwongozo wala kanuni inayoelekeza namna gani halmashauri zinaweza kuwekeza au kufanya uwekezaji. Niseme tu dhana hii ya sera yenyewe huko duniani, nitoe mfano mathalani Jiji la Pretoria, South Africa; ukienda pale *Tshwane Metropolitan City Council* wale wana-deal hadi na kampuni, wana idadi ya kampuni zaidi ya sita, wanatoa dividends to central Government, *Tshwane Metropolitan City Council*.

Mheshimiwa Spika, sasa huko nchi nyingine, ukienda vilevile Nigeria, majiji mengi duniani yanajitegemea yenyewe bila kutegemea Serikali Kuu. Sasa nchini kwetu ni tofauti kidogo, mathalani Jiji la Dar-es-Salaam. Nilikuwa naangalia hapa Jiji la Dar-es-Salaam, lenyewe kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limekusanya bilioni 75, lakini leo hii recurrent ya Serikali Kuu inapeleka, mishahara ya watumishi inalipa Serikali Kuu. Bilioni 75 wanakusanya, lakini hata kamradi tu, hata kujenga tu zahanati, Hospitali ya Wilaya bado tunasema central government.

Mheshimiwa Spika, nataka kueleza hapo kwa hiyo, namna gani naweza kusema, lakini halikadhalika Kinondoni 49 bilioni, Arusha 23 bilioni, Mwanza bilioni 17. Nikirudi kwa maana ya fursa za halmashauri huko zilizoko, natoa mfano kule niliko kwa sasa Jimbo la Mlimba. Sisi bajeti yetu kwa mwaka ni bilioni 3.7. Tumetengeneza mpango wa kujenga kila mwaka kituo cha afya kimoja na mpaka sasa ninavyozungumza tunajenga vituo vya afya vitatu, Serikali kuu imetupa kimoja tu. Tunajenga Kituo cha Afya Chita, OPD imekamilika na tumefungua, Kituo cha Afya Kata ya Igima kinajengwa, lakini na vilevile Kituo cha Afya Kata ya Mofu kwa mapato ya ndani, *1.5 billion*.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Halmashauri ya Mlimba ndogo, yenye bajeti ya *3.7 billion* inajenga vituo vya afya, hivi kweli na Dar-es-Salaam wanapiga magoti Serikali kuu? Majiji? Arusha Jiji? Ndio maana sasa matumizi mabaya ya fedha yanatokea kwa sababu, pesa haina matumizi. Wizara ijipange kutengeneza mpango kwenye majiji haya. Niliwahi kushauri huko nyuma watengeneze *clusters* kwa majiji na manispaa na ruzuku inavyokwenda waangalie, halikadhalika Wilaya. Kwa sababu, kwa mfano, nilikuwa naangalia pia halmashauri nyingine; kuna halmashauri zinakusanya chini ya bilioni moja, lakini fedha ya ruzuku ya maendeleo inaenda sawa na nyingine ambazo zinakusanya zaidi ya bilioni 10. Sasa Mheshimiwa Waziri kwa sababu yupo hapa hebu aliangalie hili ili tusiwe na *uneven distribution of national income*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hatuwezi kupeleka fedha kwenye halmashauri zote ambazo zina uwezo wa kukusanya fedha kwa hiyo, lazima tuangalie, tutengeneze *clusters*. *Cluster A, Cluster B, Cluster C*, ili sasa

tupeleke fedha za miradi ya maendeleo na *recurrent* kwa maana ya matumizi mengineyo ziende kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hayo, niende eneo lingine. Mfano nilisema Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, sisi tumekubaliana sasa, tumeanza, tumeshalima shamba la miti lenye ekari takribani 1,386, fursa tumeona ni miti. Nilivyokuwa Dodoma niliona hoteli ni fursa, kule tumeona fursa ni miti ya mbao, halmashauri zote zinaweza kufanya haya, Mungu alivyoiumba Tanzania ina fursa za kila aina kwa sehemu yao. Halikadhalika kule Songea wanaweza kulima hata mahindi, huku Rukwa wanaweza kulima hata mahindi ambayo ni miezi minne mitano unavuna.

Mheshimiwa Spika, sasa tukiendelea kusubiri kodi za wananchi, kama haitoshi tunalima pia na korosho na tumeponda ekari takribani 135 mpaka sasa. Nilikuwa nimesema Mlimba baada ya *five years*, huko nyuma nilisema Dodoma kwa sababu ndio Makao Makuu ya Nchi, kule *actually* tumeanza from the scratch, inawezekana.

Mheshimiwa Spika, changamoto tuliyonayo, narudia kusema, ni *mindset*, fikra. Wakati mwingine unaweza ukazungumza hapa kuwa kama uko sayari nyingine kumbe uko sayari hii hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni fikra (*mindset*), utayari wa kuamua kufanya jambo (*commitment*), lakini mwisho uzalendo. Unakuta Mkurugenzi wa Halmashauri tangu ameteuliwa hata kubadilisha kitu hawezi, hata kitu tu. Hata kubadilisha mkao wa kitu tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kule South Africa nafasi hizi nyeti zinatangazwa watu wanaomba na wanamwita Municipal Manager, hawaii Director, wanaita Municipal Manager, City Manager, wanatangaza kazi na watu wanaomba Professionals, sasa sisi mfumo wetu ni wa uteuzi. Sasa mimi najaribu kueleza hali halisi.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze eneo lingine ambalo ni muhimu sana, eneo la Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani Halmashauri. Ofisi hii ni muhimu sana, lakini tunaitazama kana kwamba, haina kazi, haisaidii chochote na ndio maana mianya ya wizi wa fedha ya Serikali unatokea. Leo hii uliza Halmashauri ngapi zina Mkaguzi wa Ndani ana gari? Anakaguaje miradi ya maendeleo wakati hana gari wala *facility yoyote*? Kwa hiyo nadhani Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. Lazima Ofisi za Mkaguzi wa Ndani ziwezeshwe zifanye kazi zao vizuri. Huyu ndio *watch dog* wa kwanza kwenye *level* ya halmashauri kule.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nijielekeze kwenye eneo hili la Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi. Tuna sheria nzuri kabisa na niwaambie fedha hizi zinazokwenda kwenye vikundi zina tija sana kwa wananchi wetu na sisi Mlimba, nataka nitoe mfano Mlimba, nataka kusema kwa sababu tunayafanya hayo; Mlimba sisi kila mwaka hatudai chochote, wananchi wanarejesha fedha zote, tumefanyaje? Naomba ku-share experience.

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza utaratibu wa kugawana majukumu, kwa hiyo, Madiwani wao kwenye vikundi vyta kata fulani anasimamia kurejesha fedha. Kama kata hiyo kuna kikundi chochote hakijarudisha fedha mikopo ijayo hakipati, kata hiyo haipewi kwenye mgawo. Kwa hiyo, inakuwa ni jukumu la Diwani kuwa

mlezi wa kikundi na kuhakikisha fedha inarejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa kuwa kengele imelia, naomba kusema tu kwamba, nahitimisha mchango wangu hapo, lakini nakushukuru sana. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Mbarawa na nikasema atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo, lakini kuna Wabunge hapa wameomba kuchangia hii asubuhi kwamba, wana dharura mchana, kwa hiyo, Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo utachangia mchana. Nalazimika kusema hivi kwa sababu, nilikuita jina. Sasa wananchi wako wasije wakasema Mbunge wetu yuko wapi na ameitwa jina, kwa hiyo, utachangia mchana.

Waheshimiwa Wabunge sasa tutamsikiliza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na kama muda wetu utaruhusu, atachangia pia Mheshimiwa Godfrey Idelphonce Mwambe.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja hizi tatu zilizoko mbele yetu. Niwapongeze sana Wenyeviti kwa kuwasilisha hoja nzuri ambazo tunazichangia leo hii. Nitajikita kwenye maeneo mawili; eneo la kwanza nitaanzia na KADCO, Kiwanja cha Ndege cha KIA.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha KIA ni kiwanja cha ndege cha Serikali kwa asilimia 100. Kabla ya mwaka 2009 Kiwanja cha Ndege cha KIA kilikuwa na

wanahisa wanne, mwanahisa wa kwanza alikuwa ni Serikali ambaye alikuwa anamiliki asilimia 24, mwanahisa wa pili alikuwa ni McDonald kutoka Uingereza ambaye alikuwa anamiliki asilimia 41.4, mwanahisa wa tatu alikuwa *South Africa Infrastructure Fund* ambaye alikuwa anamiliki asilimia 30 na mwanahisa wa mwisho alikuwa *Inter Consult Limited* ya Tanzania ambayo ilikuwa inamiliki asilimia 4.6.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2009 mpaka 2010 Serikali ilifanya maamuzi ya kununua wanahisa wengine ambapo Serikali ilinunua wanahisa hao kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya McDonald ambayo ilikuwa na asilimia 41.4 ilinunuliwa kwa dola za kimarekeni milioni 2.752.
- (b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *South Afrika, South Africa Infrastructure Fund* ambayo ilikuwa na asilimia 30 ilinunuliwa kwa dola za kimarekani milioni 1.994
- (c) Mheshimiwa Spika, na kampuni ya Kitanzania *Inter Consult Limited* iliyokuwa na asilimia 4.6 ilinunuliwa kwa dola za kimarekani 839,737.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo kuanzia mwaka 2011 au mwisho wa 2010 KADCO ilikuwa ni kampuni ya Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya KADCO inaendeshwa au imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, Sura Namba 212 ya Mwaka 1978. Kwa sasa Kampuni ya KADCO inasimamiwa na Wizara, lakini iko chini ya Msajili wa Hazina na Mtendaji Mkuu wa Kampuni

3 NOVEMBA, 2022

ya KADCO pamoja na Bodi ya Kampuni ya KADCO wanateuliwa na Serikali, wote wanateuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya KADCO inalipa kodi. Inalipa kodi Corporate Tax na inalipa Service Levy kwenye Halmashauri ya Hai, pia, Kampuni ya KADCO inalipa dividend. Kwa mfano, mwaka 2016/2017 ililipa shilingi milioni 555; mwaka 2017/2018 ililipa milioni 583; mwaka 2018/2019 ililipa shilingi bilioni moja; mwaka 2019/2020 haikulipa kwa sababu, kulikuwa hakuna wasafiri kutokana na ugonjwa wa Covid; mwaka 2020/2021 vilevile haikulipa dividend kwa sababu ilikuwa kuna ugonjwa wa Covid-19 na wasafiri walipungua sana. Na hizi dividends zote zililipwa kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wote wa KADCO ni Watanzania, hakuna mtu mgeni wote ni wafanyakazi wa Tanzania na karibuni ni vijana wadogo tu. Kwa vile mtu akisema kama ni kampuni ya wageni, Hapana, haelezi ukweli na sio sahihi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya KADCO, kama nilivyosema, inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria za Makampuni, haiko chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa sababu, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iko chini ya Sheria ya Uwakala wa Serikali (Agencies). Hivi tulivyo tuko katika mpango wa kuibadilisha sheria hiyo na kuifanya iwe mamlaka au authority, pengine huko mbele ndio tunaweza tukaziunganisha taasisi hizi mbili, lakini kwa sasa ni taasisi ambazo zinaendeshwa kwa sheria tofauti.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hili lilikuwa ni jambo muhimu kulieleza kwa sababu, leo limezungumzwa sana kwamba, Kampuni ya KADCO ni kampuni ambayo

inamilikiwa na watu wa nje wakati si kweli. Kwa asilimia 100 inamilikiwa na Watanzania, yaani ni Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam unaendeshwa na kampuni gani?

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam unaendeshwa na Kampuni ya TAA... (Makofij)

SPIKA: Ngoja kidogo Waheshimiwa Wabunge.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, unaendeshwa na Kampuni ta Tanzania Airport Agency (TAA).

SPIKA: Wakati Serikali ikilipa pesa 2009 na kununua zile hisa na kurejesha uwanja kwenye umiliki wa asilimia 100, ule mkataba unazungumziwa sasa hivi ni mkataba gani? Baada ya kuwa Serikali imeshalipa pesa zote?

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni mkataba ambao ni wa Serikali kwa asilimia 100, lakini kwa jina unaendeshwa na Kampuni ya KADCO. Ni jina tu, lakini kampuni yenyewe ni ya Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naweza kuitwa Peter ama nikaitwa Mbarawa, lakini hakutakuwa na tofauti yoyote ndio nitakuwa ni mimi tu.

(Hapa, baadhi ya Wabunge walipaza sauti)

SPIKA: Unajua tunapata hii changamoto kwa sababu, sasa hivi Waheshimiwa Wabunge hatuamshi jambo jipya, tunatazama Taarifa za Mkaguzi wa Hesabu

za Serikali amesemaje. Mkaguzi wa Hesabu hicho alichokisema, Kamati wamepata nafasi ya kuonana na Wizara na hao watu wa KADCO na TAA, bado inaonekana kuna changamoto.

Ukisoma taarifa ya Kamati yetu wanazungumzia mkataba kwamba, mkataba unaisha Juni, 2023. Ni mkataba gani kwa sababu, KADCO kimsingi ile iliyokuwepo awali ni kwamba, haipo, ndio msingi, kisheria ni kwamba ile kampuni iliyokuwepo awali sasa haipo kabisa. Kama haipo haya mazungumzo ya mkataba yanatokana na nini? Hilo moja. (*Makofi*)

La pili, kwa nini hiyo KADCO wakati Serikali iliponunua haikurejesha TAA kama ambavyo TAA inafanya Dar-es-Salaam ifanye na huko kwa sababu, haya yote yasingejitokeza kama CAG hakuonesha kuna shida? (*Makofi*)

La tatu, pesa umeeleza hapa na niwapongeze sana Serikali kwamba, mnafuatilia kwamba, KADCO inalipa pesa. Sasa hata wewe unaona ni KADCO inalipa pesa, sio Serikali inajilipa pesa. Hii KADCO imezishikilia wapi hizi pesa ambazo kwa kawaida zinashikiliwa sehemu nyingine halafu yenyewe ndio inailipa Serikali? (*Makofi*)

Hayo tu Mheshimiwa Waziri, halafu tuendelee na michango mingine.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza kama ulivyosema, mkataba unaisha tutalifanyia kazi, hilo sitaki kulizungumza sana naomba tulichukue tukalifanyie kazi tuone mkataba unaishaje na tunafanyaje, lakini kuna mpango wa Serikali ambao sisi wenyewe tunataka kuhakikisha kwamba, KADCO

inarejea kwenye TAA hiyo tunao mpango, lakini kwa sasa kwanza tubadilishe Sheria ya TAA ambayo inasimamia Kiwanja cha Dar-es-Salaam, kiwanja cha Mwanza na viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama nilivyosema TAA sasa hivi inasimamiwa na Sheria ya Uwakala (agencies), kwa vile tunachotaka kufanya ni kuhakikisha kwamba TAA inakuwa mamlaka na baada ya hapo mchakato wa kuhamisha KADCO utaendelea. Mazungumzo yameanza muda mrefu ya jambo hili kwamba KADCO lazima iwe chini ya TAA, hilo tunaendelea kulifanyia kazi, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pesa zinawekwa wapi, pesa kama kuna akaunti mbalimbali zinawekwa. Katika Mashiriki yote ya Serikali mengi yanaweka pesa zao katika akaunti zao BOT na ikifika wakati wakulipa dividend inatoa BOT inaipolekea Serikali, kama taasisi zingine zilivyo kama TPA na nyingine zote ambazo huwa kunakuwa na akaunti maalum ambayo inawekwa BOT, wakitaka kutumia kawaida wanaomba kibali kama taratibu zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo kwa ufanuzi wa jambo hilo, lakini kwa ufupi tutalichukua na tutalifanyia kazi kuhakikisha kwamba mwisho wa siku KADCO inarudi chini ya TAA.

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, mimi nitakupa tena nafasi, siyo leo ili hayo mengine ukayafanyie kazi. Nitakupa nafasi tena Jumamosi wakati wanahitimisha Wenyevit

wetu, Mawaziri mtapata nafasi ya kufafanua mambo mbalimbali na wewe Mheshimiwa Waziri pia utapewa.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, sawa.

SPIKA: Itaturahisishia ili Bunge liweze kufanya maazimio ambayo kwanza yanatekelezeka, pili yana uhalisia wa huko nje. Mheshimiwa Waziri utatusaidia kufafanua hii KADCO akaunti yake ipo pia BOT? Kwa sababu ni ya Serikali asilimia mia moja, halafu ulisema unayo mambo mawili kwa hiyo hili la KADCO umeshatoa maelezo, haya mengine ambayo nimeuliza kama ulivyosema unalichukua utalitolea ufanuzi Jumamosi. Hilo la pili sasa nakupa fursa, maana ulisema una mambo mawili, karibu sana.

WAZIRI WA UJENZI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili, jambo la pili lilizungumzwa kuhusu viwanja vya ndege sasa hivi vinasimamiwa ujenzi na TANROADS kwa nini visisimamiwe na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Ni kweli jambo hili uamuzi ulifanyika mwaka 2017 ambapo *instrument* ilibadilishwa na viwanja vya ndege kupelekwa TANROADS, vilipelekwa kwa kipindi hicho kukiwa na sababu za msingi lakini baada ya muda mrefu tukaona hizo sababu hazipo na sasa tuko kwenye mchakato wa kurejesha baadhi ya ujenzi chini ya TAA. Kuna ujenzi ambao umeanza mfano, hapa Msalato tumepata pesa za ADB itakuwa ni vigumu sasa kuanza kutoa uwanja wa Msalato chini ya TANROADS kwenda TAA kwa sababu mchakato wenyewe unakuwa mrefu na kazi imeanza. Kwa vile, viwanja ambavyo vitaanza kujengwa sasa hivi ujenzi utasimamiwa na TAA kama Sheria ya ICAO inavyosema.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha. Ahsante sana.(Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza niwapongeze sana Wenye viti wa Kamati na Wajumbe kwa taarifa nzuri, pia ninaipongeza Ofisi ya CAG kwa taarifa ambayo ametupa Wabunge kuweza kuona mapungufu.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwa upande wa Halmashauri. Jana nilimsikia rafiki yangu Boniphace Getere alizungumza kwa uchungu sana kuhusiana na madudu yaliyofanyika kwenye Halmashauri yake, hili ni somo zuri sana la kujifunza. Sisi Wabunge wote humu ndani tunamheshimu sana Mheshimiwa Boniphace Getere kwa sababu ya *information*, ni mtu ambaye anajua vitu kabla ya wengine hamjajua. Hebu fikiria mtu tunaemheshimu kama hivi Halmashauri yake kuongoza kuwa na Hati Chafu. Hili ni suala ambalo tunahitaji pia Serikali itusikilize.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba Mheshimiwa Boniphace Getere hajawahi kuona haya matatizo kabla, ameyaona hata kabla ya Mkaguzi lakini sasa ni nani anachukua hatua ambapo Mheshimiwa Boniphace anapoona yale matatizo akiyapeleka kwa wahusika yanachukuliwa kama majungu.

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza mara mbili mbili, hivi ni kweli Wabunge kwenye Halmashauri zetu tunasubiri mpaka Mkaguzi wa Hesabu za Serikali atutangaze kwenye vitabu kwamba Halmashauri yako ina Hati Chafu? Hapana hii ni aibu. Ni lazima tuone namna! Nilikuwa najaribu kujiuliza kaguzi kama tatu nikiwa hapa Bungeni, madudu mengi sana yanaonekana yako Halmashauri, ni kweli tunajadili humu na tunasema, sasa najiuliza tulitengeneza Sheria kwamba Mheshimiwa Rais anakabidhiwa ripoti ya CAG halafu inasema ipelekwe Bungeni sasa kujadiliwa kwenye Bunge la Wananchi, nasi tunakuja tunaongea, lakini mwakani yale yale yamezaa na kuzaa! hii siyo sawa nafikiria nasi tubadilike ni lazima na sisi tuone namna ya kuishauri Serikali au tuone namna kama ni Sheria tulitunga Sheria mbaya basi tubadilishe, hakuna maana ya kuja kujadili wizi kila mwaka, wizi wakati hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, najaribu kuchukua mfano mmoja, utanisamehe maana wewe ni Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Law School. Ni kama pale Law School watoto wanavyolalamika kila mwaka, wanalamika wanafunzi 600 wanafaulu 26 na sisi hatuchukui hatua, sasa najiuliza wakalie wapi? Kwa sababu tatizo ni walimu au tatizo ni wanafunzi? Maana kila mwaka Law School wakimaliza Mia Sita wanafaulu wanafunzi 20 au wanafunzi 30 na hakuna hatua tunachukua kama Bunge. Sasa ndiyo kama huku, kama chuo hakifaulishi tatizo ni Walimu wa Chuo au tatizo ni Wanafunzi? Sasa tunaambiwa kila siku na CAG matatizo yako Halmashauri na Bunge tunawalalamikia Viongozi wetu huku kuna wezi, huku kuna nini lakini matatizo yanajirudia yaleyale na hatuchukui hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili suala ningeomba sana Wabunge tuone aibu na ingependeza zaidi, maana wananchi wetu wanajua na ikitokea Halmashauri yako imepata hati chafu wa kwanza kuwa mchafu ni Mbunge kwa sababu wewe ndiyo wamekuchagua uwe mle, uwasaidie kuwasemea, uwasaidie kusema huyu ni mbovu, sasa unanioneshaje mimi kama Mheshimiwa Musukuma ni mchafu na sina uwezo wa kukagua hesabu, sina uwezo wa kusimamia miradi mpaka inakuja kusemwa na CAG? Nilikuwa nashauri sana kama wenzetu huko nyuma walikosea kutunga sheria, hili Bunge ni la kisasa tubadilishe sheria ili tutengeneze adhabu humu ndani. Nami naunga mkono maneno ya ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi, mengine hatuungani lakini hili nakuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, labda tufike wakati hizi nafasi za Wakurugenzi zitangazwe. Ukiuliza Wabunge humu kila mtu ana presha na Mkurugenzi! Mbunge pale yupo yupo tu kama mpita njia, yale mambo mabovu anajua sasa hivi mko kwenye Bunge anapitisha fastafasta na anakualika leo kesho ngoma inatembea, ninaomba sana kama tulifanya makosa huko nyuma ni vizuri tukarekebisha maana sote ni Wabunge, tunatoka kwenye Majimbo kwa hiyo, siyo vizuri na siyo sahihi kusemwa humu ndani. (Makof)

Mheshimiwa Spika, lingine ninadhani hata kwenye Ofisi ya CAG inatakiwa tuseme vizuri, kuna vitu najaribu kuona hapa sijui kama nitatumia lugha ya kuudhi kwamba muda mwingine hizi hati safi na hati chafu hazipatikani hivi hivi, kuna sehemu ambapo ni pachafu pamepewa hati safi, sitaki kutaja ni wapi. Sasa najiuliza, wenzetu hawa wanapokuja kukagua pengine huwa kuna mazungumzo ili itengenezwe hati safi na hati chafu au ni

vitu gani? Kwa hiyo, nishauri na wao watu wa CAG wanyooke kama wanavyotaka sisi tunyooke kwenye ripoti ili ripoti zao ziwe na msimamo mzuri. (Makofii)

Mheshimwa Spika, kwa mfano, kwenye Halmashauri tunapata wageni kwa mfano Mawaziri mnapokuja. Na hili Mawaziri mtusikilize mtuelewe, mnapokuja kwenye Halmashauri zetu punguzeni mwendokasi kwa sababu haya mambo tunayajadili humu mnayasikia na kila siku tunawauliza maswali, lakini Waziri unakuja dakika kumi unapelekwa kwenye majengo huna muda wa kusikiliza, sasa unajiuliza yaani Waziri unakwenda kupima performance ya Halmashauri kwa kukagua tu jengo au darasa lililopakwa rangi vizuri? Hapana kaeni ndani mtusikilize tunazungumza nini, sikilizeni Madiwani, kuna sehemu Madiwani hawana nafasi hata ya kuwashauri Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, Mimi naijuliza sijui muundo wetu sijui ulikuwaje kwa sababu hebu jiulize, huwa namuona Mheshimiwa Waziri Mkuu akienda mahala anakaa anaanza kutaja Tarehe Fulani, wiki fulani, *document* fulani huwa anatoa wapi hizo *document*? Kwa sababu nanyi ni Mawaziri, mbona huwa hampati huo muda wa kuwaambia hivyo wale mnaoweza kuwawajibisha? Lakini tunaona Mheshimiwa Waziri Mkuu anapoenda akifika pale anaeleza yale, anasindikizwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama hili nalo ni tatizo lingine tukitaka kukomesha haya mambo. Kwa sababu Kamati zetu za Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Wilaya uwezo ni mdogo wa Kwenda kukagua, ili akakague anahitaji mafuta ya Mkurugenzi, hivi vitu hawezi kuvikemea hata kidogo, kwa sababu mtu amekuwekea mafuta, ukute amekuandalia na *lunch*, haya mambo utafanya kwa *design* gani? unakuwa kama mtumwa! (Makofii)

Mheshimiwa Spika, unajisikiaje Mheshimiwa Waziri Mkuu ukifika pale unakosoa? Niliona kajengo Milioni 20, mimi naweza kukajenga kwa Milioni Moja na Laki Tano na Kamati ya Ulinzi ipo, unawaambie eeh... na jana walienda ku-reck njia ya Waziri Mkuu anapoenda pale, sasa najiuliza kwa nini tusifukuze wote wale? Kwa sababu kuna vitu vingine kweli muundo wa Serikali vilitengenezwa kwamba hili litafatiliwa na mtu fulani, lakini wenzetu hawatimizi majukumu yao. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana suala la Halmashauri linahitaji muda, Wabunge tupewe heshima tunapoleta matatizo yetu kwa Mawaziri, Mawaziri chukulieni serious, sisi siyo wapiga majungu! Mnachukua maneno yetu mnayapeleka kule ndani yanageuka kwamba huyu ni mwongeaji! Hapana, mwisho wake mtatukatisha tamaa na sisi tuwe watazamaji ili mkija, nakaa nyuma, ukiuliza maswali na mimi nashangaa. Hivyo, ni vizuri zaidi tuone vivu na Ubunge wetu siyo vizuri kuanza kukosoana humu ndani. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la asilimia Kumi, kama tuna mahala tulikosea muundo wake ni hapa. Hizi ni hela unamchukua mtu wa Maendeleo ya Jamii, unamkabidhi Halmashauri kama ya Geita ambayo kwa mwaka inatoa asilimia Kumi Shilingi Bilioni Moja, halafu anakwambia miaka mitatu sijakusanya. Hivi tuna watu wangapi waliosoma mambo ya uhasibu, mambo ya fedha? Kila siku benki zikitangaza kazi watoto wanaomba mpaka Elfu Tano, Elfu Kumi, kwa nini tusiwe na Kitengo cha Benki kweli Halmashauri ambapo zinao uwezo? Kama hatuwezi kuna Mbunge mmoja jana alisema, tukubaliane na mabenki, tupunguze tu masharti kweli kitengo cha vijana walemavu na akina mama,

Iakini fedha ziwe benki, watu ambao wana uwezo wa kuzikusanya hizo hela. Unakuta Halmashauri inadai karibia Bilioni Kumi na Sheria inakutaka utoe, sasa tunachukua hela tunaenda kuzigawa ambazo hazina *return* siyo vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumze kuhusu *DART*, nimesoma kwenye *DART* yale mambo ya mwendokasi, huwa najiuliza mara mbilimbili kwamba, *DART* tunamiliki miundombinu, kuna mwingine anaendesha magari, hata mwaka mmoja kila siku ana-declare matatizo, Iakini Serikali inachukua ela inarundika kutengeneza mabarabara, tuliutumia mfumo mzuri kweli kwamba, Serikali inatumia mabilioni ya pesa kutengeneza barabara kwa ajili ya kumtengenezea mtu mmoja apitishe magari ambayo tena hayafanyi vizuri! Sasa najiuliza tuna Mkurugenzi, tuna nani, tuna makoloko kwenye idara ambayo haizalishi! Ni vizuri tukawa tunatengeneza miradi ambayo inazalisha

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namsikiliza Ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi hapa anasema *hotel* nyota tano sijui nini, Iakini kama kuna vitu wasomi mnatuangusha, Mimi ni Daktari wa heshima ni hapo, kutengeneza vitu ambavyo havina *return*. Mimi ninakaa Dodoma hapa huwa naumia sana nikipita pale nikiona ile *hotel* najiuliza kwamba, wasomi walikaa na ku-discuss kutengeneza ile *hotel* wanaita mmh! (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, wakati hapa Dodoma kuna maeneo ya heka kumi na yeye ndiye aliyekuwa anauza viwanja! Hii *hotel* ilikuwa nzuri na ya mfano ya kutengeneza Jiji, ingekuwa sehemu yenyé heka tano, hivi vitu unatengeneza soko halafu unajisifu, tuambiwe *return* hizi ni hela za wananchi...

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunambi.

T A A R I F A

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa ndugu yangu Musukuma kwamba, tulikuwa tumeangalia kwenye hotel anazosema, kuna ile ya Mjini inaitwa *Drop off Hotel* na lengo tuliangalia *viability of the project, returns on investment*, tuliangalia pia muda gani utatumika. Kwa ile kulingana na andiko letu ilikuwa ni miaka sita, sasa hoja tulisema wawa-engage operator ili a-operate, lakini ndani ya miaka sita ile fedha ilikuwa inarudi Bilioni Tisa. Kwa maeneo anayosema, Mji wa Serikali tukaona lile eneo ni kubwa, tukatengeneza hotel nyingine ambayo ni ya nyota nne yenyewe parking kubwa sana. Kwa hiyo msingi wa hotel ya Mjini ni drop off hotel hata Dubai zipo. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Msukuma unapokea taarifa hiyo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa hiyo, mwenye macho ameona na mwenye masikio amesikia, kwa sababu tutajibishana na ninamheshimu ni mdogo wangu na nimheshimiwa Mbunge lakini ni lazima tushauri vitu vyenye maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukichukua hiyo hotel anayoisema na vitu viwili vitatu umevisema ukiweka na soko la Ndugai nikikuuliza *return yake* hata na mimi nitakuwa

nimeshakufa bado hata theluthi moja haijawahi kuwa na *return*, halafu unasema hiki tunatengeneza chanzo baada ya kumaliza ardhi, Hapana! Tutengeneze vyanzo vyenye maslahi, tushauri watu, vitu vyenye maslahi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mjumbe jana alisema humu ndani, ukienda kwenye kila Halmashauri wote tunaandika maandiko kwa sababu hela zipo tunataka stendi, lakini stendi siyo mradi endelevu. Kuna watu wengine wameweka stendi baada ya miaka mitano au 10 haina *return* yoyote. Lazima tuone sehemu kama Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, kwenye Majiji sawa lakini unachukua stendi ya Bilioni 29 unaenda kuweka kwenye Halmashauri inayokusanya Laki Tatu na Hamsini kwa siku, halafu unaita mimi nimesoma, nimefanya upembuzi yakinifu, hiyo haiwezekani! Tunawaingiza chocho kwa sababu wanaolipa ni wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wewe kwamba tunavyo vyanzo vya mapato ambavyo vitalipa yale madeni, kwa nini tusifikirie kuisaidia Serikali kama ulivyojenga kule Mlimba Vituo vya Afya na vitu vingine ambavyo moja kwa moja vitakwenda kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba nishauri suala lingine moja la mwisho. Nimepita pale Dar es Salaam ninajua tu hili litakuja kuamka, jana humu ndani nimesikia wamechangia. Ukiangalia mwendo kasi leo wa kutoka Mbagala stendi yake imeenda kuangukia pale kilipojengwa kitovu cha ramani nzuri sana ya mwendokasi mkubwa, watoto wa mjini tunaita Tanzanite pale. Jiulizeni jamani mtu anatoka Mbagala halafu kituo kinakuja kuangukia palepale kwenye ramani ambayo tunachukua ramani hata Kimataifa tunarusha kwamba mwendokasi,

tunadondoshea kituo pale cha watu wanatoka Mbagala. Kwa hiyo, mwingiliano ule ni vizuri yaani ...*(Makofi/Kicheko)*.

Mheshimiwa Spika, kwanza hata ramani, najiuliza kwa nini tusingeondoa elimu za darasani tukatumia kama yangu ya heshima? Yaani nafikiria unajiuliza kabisa kwamba wamekosa sehemu yoyote ya kuweka kituo? Ramani ya ile *Tanzanite*, glass yote ile nzuri, halafu inakuja kudondoshewa pale pale *giiih!*, Mtu ametoka rangi tatu kule, huku inaka...jamani, jamani ndugu zangu na lenyewe tunasubiri CAG mwakani atuletee taarifa? Kwa hiyo, ninaomba sana niwashauri, tuna wivu na Ubunge na Wasomi wetu tunawapenda, ningeomba mtumie shule zenu vizuri. Ninakushukuru ahsante sana.*(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mbunge mwenzetu ameomba atoe mchango ana dharula, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia na mimi hoja tatu ambazo zimewekwa mbele yetu lakini kipekee nitajikita kwenye hoja zilizoletwa na Kamati ya PAC.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudini kubwa anazozifanya za kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora kwa wananchi wetu na kuzingatia value for

money kwenye miradi yetu, lakini tunaongeza makusanyo na kuboresha hali ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naichukulia hali ya ukaguzi uliofanywa kwenye taasisi lakini pia na Wizara kama huduma ambayo CAG anaitoa kwa Bunge. Na ninachukulia kwamba sisi Wabunge ni Madaktari na tumemuomba CAG atuangalizie mgonwa ambae ni Serikali na CAG yeye ni mtaalam wa Maabra. Baada ya ukaguzi wa damu, CT scan MRI akatuletea matokeo na matokeo ambayo ametuletea Kamati inawasilisha kwenye Bunge kama jopo la Madaktari ili tuweze kujadili na kutoka na maazimio ya ni namna gani mgonjwa wetu atatibiwa.

Mheshimiwa Spika, tumesikia hoja za wajumbe mbalimbali lakini pia za Mwenyekiti wetu wa PAC kuhusiana na yale tuliyoyabaini kwenye majadiliano yetu na CAG pia na taasisi husika. Kuna changamoto nyingi tumeziona lakini ninaweza kuzipanga katika maeneo matatu au manne.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni mikataba. mikataba mingi ambayo inaonekana imesainiwa inatugharimu mabilioni ya pesa kama Taifa. Ukiangalia kwa mfano bilioni 355 ambazo tunaenda kuzilipa kwa Symbion, ukigawa milioni tano tano kwa wanafunzi wetu wa vyuo vikuu, tungeweza kuwahudumia wanafunzi 71,715 kwa kuwapa mikopo; lakini hiyo tunakwenda kuwalipa Symbion tu kwa mkataba wa awali ambao kimsingi ulisainiwa under emergency power plan, mwaka 2006/2007. Vile vile bado ukaongezwa mwaka 2008 ukasogwezwa ukatuletea matatizo.

Mheshimiwa Spika, tumeona kuna vihenge. Kuna mkataba wa ujenzi wa vihenge, kuna Mkataba wa Aurial ambayo ni kampuni ya Philips ambayo iko kule Uhlanzi ya ku-supply vifaa vya tiba. Kuna mikataba mingi ambayo imetusababishia hasara ya fedha nyingi. Pia kuna mikataba mingine mingi ambayo hatujaiona, na labda baadhi ya wabunge hawajaiona.

Mheshimiwa Spika, tunayo pia mikataba ambayo tunatakiwa tulipe kama *current liabilities*, kama madai sasa ni trilioni 1.7 kwa TANESCO kutokana na kesi mbalimbali zinazotokana na uzalishaji wa umeme, usamabazaji na matumizi yake, ambako kuna kampuni tatu zinatutadai ikiwemo kampuni maarufu *IPTL* kupitia *Standard Chartered Bank Hong Kong*.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo ukingalia mikataba mingi ambayo tu nayo inatunyonya sana kuliko kutusaidia kama nchi, na inatumika kama *conduit*, ni kama vile tumechukua tenga tunaenda kubeba maji; ambazo ni fedha, halafu yanadondoka nje kwa sababu tu hatujaweza kuziba mianya kupitia mikataba.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria na unafahamu uandaaji wa mikataba. Ni kesi chache sana ambazo Serikali imewahi kushinda kwenye mabaraza ya usuluhishi au Mahakama, kesi chache sana. Nafikiri wengi watakumbuka City Water ndiyo ambayo tumewahi kushinda, lakini kesi zingine zote tunashindwa, hata pale ambapo mwekezaji au mtoa huduma hajatimiza masharti yake lakini bado sisi tunashindwa kwenye hizo kesi na kulazimika kulipa mabilioni ya fedha za Serikali. Baadaye tunahangaiika Kwenda tunaenda kukopa, kuweka tozo, kuwabana wajasiliamali wetu na kuwabana

wafanyabiashara walipe kodi, pesa ambazo kimsingi tumeshindwa kuzilinda.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni manunuzi. Bahati nzuri Weheshimiwa wenzangu walizungumza hapa, akiwemo Mheshimiwa Maimuna Pathan na Mheshimiwa Deus Sangu. Upande wa manunuzi tunapoteza fedha nyingi, miradi mingi haishi kwa wakati, ina extension na variations za kutisha.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu na mwaka jana tulipewa taarifa hapa kwamba hata ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kufikia Novemba, 2021 ilitakiwa maji yaanze kuingia kwenye bwawa kwa miezi mitatu hadi minne na commission ingeweza kufanywa mwezi Juni, 2022. Hata sasa hapa tunavyoongea kuna extension tena ya miaka miwili sijui. Hatuelewi hiyo extension imetokana na nini na gharama ni nani analipa? Mapato ambayo tungepata kwa kuuza umeme nani atafidia? Hata kasi ya usambazaji wa umeme wa REA haiwezi kuwa kubwa kwa sababu kiwango cha umeme kinachozalishwa ni kidogo. Tulitegemea umeme huu ungeweza kuingia haraka kwenye grid. (makofi)

Mheshimiwa Spika, tunaona pia kuna madhaifu ya kiutendaji. Kuna maeneo mengi tumeona ukusanyaji wa kodi umekuwa ni mdogo. Kuna changamoto katika ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, moja, mfumo kupitia Tax admiration Act si mzuri sana; na kuna systems ambazo zinakadiria kodi kubwa kuliko uhalsia na pia kuna upungufu wa utaalamu. Wako wataalamu wa upande wa kodi hata mkopo wanaupigia hesabu ya capital gain tax, matokeo yake liabilities kwa wafanyabiashara

inakuwa kubwa na hawawezi kulipa, wanahangaika, wanalazimika kufanya *objection* tunakwenda huko kwenye TRAB na TRAT mnakokusikia.

Mheshimiwa Spika, hii yote ni kutokana na kubadilika na mfumo wa kiutendaji ambapo zamani kulikuwa na a proper tax accessor ndani ya TRA ambaye amefundishwa, ame-undergo *intensive training* kule TIA au sehemu nyingine ya nchi, akiwa ni mtaalaamu wa ukadiriaji wa kodi kwa sababu amebobea kwenye eneo lile na ni mtaalamu. Sasa hivi mtu ye yote tu, akikaa kule Masasi ofisini au Kalambo anakukadiria tu. Jambo hili limepelekea *tax disputes* nyingi na *objection* kuzalishwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuchukua muda mrefu kujielekeza kwenye mapendekezo. Naomba Waheshimiwa Wabunge mridhie mapendekezo haya ili tuweke kwenye maazimio yetu kupitia Mwenyekiti wetu wa Kamati ya PAC.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ninashauri; ili kuziba mianya ya mapato na matumizi ya Serikali, mikataba yote ambayo inazidi five bilioni iletwe bungeni kupitia kamati, au kamati maalumu tuweze kuihakiki na kui-approve.

Mheshimiwa Spika, la pili, mikataba yote iliyopo kwa sasa, najua kuna juhudzi zilikuwa zinafanywa na Serikali kupitia mikataba mbalimbali kuweza kuihuisha, kuiboresha na kuifanya ya kisasa angalau kulinda maslahi ya watu wetu, nayo iletwe tuihakiki na kuiona kama mikataba hiyo ina maslahi na kama haina maslahi tukae mezani tuweze kuijadili upya tuweze kufanya *review* ya hiyo mikataba.

Mheshimiwa Spika, iko mikataba ya upande wa madini, gesi na upande wa kwenye vitalu vya utalii kule na maeneo mingine ya kimkakati. Iko miradi ya SGR, *Stiegler's gauge* na upanuzi wa bandari. Tulienda Tanga, kule kuna vitu vya ajabu sana nafikiri na vingine mlivisikia, ambapo mtu amepewa tenda leo halafu kesho aka-subcontract kwa mtu mwingine kwa bei ya chini ya nusu ambayo analipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kushauri sana mikataba hii tuitishe upya, tuweze kuipitia na kuitengenezea *frame work* ili iwe mikata ambayo ina faida kwetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la adhabu na tuzo ambazo zinatolewa kwenye taasisi za usuluhishi au mahakama za usuluhishi wa migogoro ya wafanyabiashara na wawekezaji. Iko ICC International Chamber of Commerce pamoja na Icid ICSID ambako kule tunashindwa mara nyingi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri kabla ya Serikali haijalipa chochote huko sisi tutoe azimio, Serikali ije Bungeni tukae nao na tujadiliane nao tuone hicho kinachokwenda kulipwa ni nini, kina-make sense namna gani na kama kweli tunaridhia; ili fedha ya umma inapokuwa inatoka kule sisi kama wawakilishi wa wananchi basi tuwe na taarifa nayo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana kwenye suala la ukusanyaji wa kodi. Tumeambiwa hapa zaidi ya trioni 2.8 hazijakusanya. Ukiangalia zile sababu kutohana na taarifa za CAG zinaonesha kwamba mfumo wa kodi wa sasa umepitwa na wakati. Aliyekuwa Waziri wa fedha wakati ule ambaye kwa sasa ni Makama wa Rais

Mheshimiwa Philip Mpamgo, aliwahi kutoa mapendekezo kwamba kuna *Presidential Recall Committee on Tax Systems Reforms* ambayo ilifanywa mwaka 1992 chini ya Mzee Mtei na hajjawahi kufanywa tena. Ili tuweze kuona *fiscal policy* yetu ikoje, nani tumtoze, vyombo gani, tuendelee na VAT ya asilimia 18 ilhali wenzetu ni asilimia 16 kwenye kanda. Je, mfumo wa *TRA* upoje? Je, bado ibaki kama ilivyo? Au idara za *TRA* zibaki kama *thematic departments*.

Mheshimiwa Spika, kwamba kama Idara ya VAT iwe Idara ya VAT, na isiwe inafanya *tax payer* na kufanya VAT, *Domestic revenue* anakusanya VAT hii inaleta mkanganyiko mkubwa sana. Kwa hiyo nilikuwa naomba sana waheshimwa Wabunge tukubaliane, kwamba tuiagize Serikali kama maazimio iweze kufanya *comprehensive tax system review* ili tuweze kubaini mfumo wetu wa kikodi ukoje ili tupate kodi za kutosha.

Mheshimiwa Spika, hii itatusaidia kuongeza *tax effort*. Tax hatujilipi ratio ambayo kwa bahati mbaya tangu mwaka 1995/1996 bado tuko asilimia 10 hadi 11. Maana yake ni makusanyo yote ya kodi kulingana na uzalishaji (*tax over GDP*) ambayo tuko below African average ya asilimia 18. Hii naamini itatusaidia kutengeneza mfumo mzuri na kuitengeneza *compliance* kubwa, watu walipe kodi wakiwa na furaha kwamba wanachangia kwenye maendeleo kwenye taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kuna hii tabia ya Serikali kukaa na fedha za wafanyabiashara kwa sababu imeshindwa kulipa kwa wakati kutokana na zabuni au ukaguzi wa *imports duty* na *refunds*. Mimi ninasema, kama Serikali inatoza faini na *penalties* kwa mfanyabishara kuchelewa kulipa fedha Serikalini basi sasa kwa uwajibikaji Serikali

nayo ijitoze faini na riba kwa mfanyabiashara endapo tutachelewesha malipo kwao. Kwa sababu tunachelewesha malipo kwao tuna-*hold working capital* zao; hili linasababisha ku-paralyze private sector.

Mheshimiwa spika, nilikuwa natamani sana, tumeliangalia sana shirika la TANESCO. Shirika la TANESCO lina mzigo mzito ambao umetokana na mfumo uliopo sasa hivi. Napendekeza tufanye upya mapitio ya Sera ya nishati ya umeme ili tufanye *divestiture* ndani ya TANESCO. Tunajua TANESCO inajihuha na masuala ya uzalishaji, usafirishaji pamoja na usambazaji wa umeme, lakini tumeruhusu *independent power producers* kwenye uzalishaji peke yake halafu wanalahazimika kumuuzia TANESCO. Kwa hiyo TANESCO hata kama hajajiandaa analazimika kununua na kuingia power purchases agreement na kutengeneza mzigo mkubwa ambao TANESCO sasa hivi tunauona.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu, kama ambavyo ilikuwa TTCL zamani tukaruhusu Vodacom, Tigo na wengine waingie, tufanye *divestiture*, turekeboishe sera zetu ili turuhusu na wengine waje wawekeze. Kama ni Symbion aweke mtambo wake azalishe, asambaze umeme wake, atafute wateja wake aendelee ili TANESCO iendelee kubaki salama kutokuizingiziwa mzigo mzito kama ambavyo ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tumeona pia suala la bodi ya mikopo. Mimi ningependa kuungana na Mheshimiwa Japhet Hasunga, alitoa pendekozo hapa jana. Napendekeza Serikali angalie uwezekano wa kuunda mfuko wa taifa wa kugharamia elimu ya juu na si bodi ya mikopo; ambao na utakuwa ni mfuko wa pamoja. Watoto wote wa Tanzania wanastahili kusoma.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja, nilipata bahati kipindi fulani kwenda kusoma Kijerumani CDTC center pale Koloni (Cologne) Ujerumani; tukawa na watoto wadogo kama 20 hivi tunasoma nao pale. Nikawauliza, walikuwa wanaongea kifaransa, wale Watoto wanatokea nchi ya Gabon. Serikali ya Gabon imetengeneza utatibu kwamba, kila mwaka *the best science students form six wanapelekwa Ujerumani kusoma electrical engineering, mechanical engineering, civil engineering kwa gharama za Serikali for Seven-years, kila mwaka.* Gabon haitakuwa sawa sawa na sisi baada ya miaka 20. Kwa nini sisi tuone hasara kuwasomesha watoto wote? Kwa nini tulazimike kumbagua huyu, sjui mzazi wake yukoje, mzazi wake hana mguu mmoja kwa hiyo tumpe.

Mheshimiwa Spika, mimi ninapendekeza tuanzishe mfuko wa taifa, tutafute vyanzo, vyanzo viro ili kila mtoto aweze kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana la *Local content* ambalo jana hata Mheshimiwa Kigwangala alilizungumza. Ni namna gani tutawawezesha watu wetu? Tunafurahia sana kuona orodha ya mabilionea wa nchi nyingine? Tunatakiwa sasa kuwatengeneza wa kwetu, tuwaamini wafanyabiashara wetu tuwatafute tuwatengeneze.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri sana Serikali ije na *Local content law* ili tuweze kuitisha hapa tukainisha maeneo mbalimbali ambayo tunaamiani tunaweza kuwasaidia Watanzania wetu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. GEOFFREY I. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kikao chetu cha leo. Nitangaze majina ya baadhi ya Wabunge ambao tutaanza nao mchana. Yupo Mheshimiwa Joseph Anania Thadayo, Mheshimiwa Kilumbe Shaabani Ng'enda, Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mheshimiwa Radhia Idarus Faina, Mheshimiwa George Natali Malima. Wengine Tutaendelea Kuwatangaza Katika hao wanao anza hapo. Tunae pia Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni ambao wameingia hapa Bungeni baada ya matangazo yetu ya wageni, na hawa ni wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 100 na Walimu 10 kutoka Shule ya Awali ya Msingi Wesley ya Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana wanafunzi na walimu tunaamini mmeputa nafasi ya kujifunza mambo machache, karibuni sana. Mnaweza kuketi.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawakumbusha tena kuhusu semina inayohusu bima ya afya kwa wote, ambapo tukitoka hapa sote tuelekee Msekwa Kwa ajili ya semina hiyo muhimu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

3 NOVEMBA, 2022

(Saa 7.14 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihanzile) alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali
kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu
za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu,
Mashirika ya Umma na Kagazi za Ufanisi kwa Mwaka wa
Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za
Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa
zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu
za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni,
2021**

na

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa
Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma
kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Majadiliano yanaendelea.
Kuna Waheshimiwa walitajwa kwa ajili ya kuanza

kuchangia. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, wakati huo Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, wanajiandaa.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwa mchana huu. Nitachangia kwenye taarifa ya Kamati ya LAAC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naishukuru kwanza Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo imeendelea kutuongoza vizuri na kuwapelekea wananchi wetu huduma mbalimbali ikiwa ni za kiuchumi, za kijamii na kadhalika. Hivi ninavyozungumza, jimboni kwangu tulikuwa tunakabiliwa sana na tatizo la chakula, lakini leo hii kuna chakula cha bei nafuu ambacho kinashushwa kupitia NFRA. Naishukuru Serikali, na kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nilimlilia sana na hata kuomba kuongezewa kwa sababu ya hali ilivyo. Kwa hiyo, Serikali inafanya kazi nzuri kiuchumi, kijamii na pia kuwashudumia wananchi pale panapokuwa na majanga.

Mheshimiwa mwenyekiti, shughuli zote hizi, wasimamizi wakuu ni Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo nazizungumzia leo kwenye taarifa hii ya LAAC. Sote ni mashahidi kwamba miradi mingi inatekelezwa na mamlaka hizi. Nikitoa tu mfano kwenye Jimbo langu la Mwanga, Halmashauri ya Mwanga inasimamia vizuri ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, kazi inakwenda vizuri; Halmashauri imesimamia vizuri ujenzi wa Vituo vya Afya, na sasa wanamalizia Kitua cha Afya cha tatu cha kimkakati, shule na kadhalika. Kwa hiyo, kwa kweli wanafanya kazi nzuri, nawapongeza Halmashauri yangu

ya Mwanga, Viongozi wote pamoja na Baraza la Madiwani kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hizi wanazoendelea kuzifanya sasa, ili waendelee kuzimudu vizuri, yapo mambo ambayo Serikali pia inahitaji kuendelea kuyafanya kwenye Halmashauri zetu. La kwanza hasa ni kuwajengea uwezo kwenye eneo la Bajeti. Halmashauri yangu ya Mwanga kwa hesabu hizi tulizozzungumzia za mwaka 2021, ilipokea 33% tu ya bajeti iliyotengwa. Sasa hili ni tatizo kubwa sana kutegemea utekelezaji wa miradi kwa asilimia kubwa kwa kiwango cha bajeti ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ipo changamoto pia ya watumishi. Nikitolea mfano hapo hapo kwenye Malmashauri yangu ya Mwanga, mahitaji ya jumla ya watumishi ni 3,117 lakini halisi tulionao ni 1,861, kuna upungufu wa 1,256, upungufu huu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye sekta mbili nyeti sensitive; Afya mahitaji ni watumishi 786, lakini halisi ni 336 tu, kuna upungufu wa 400. Ukija kwenye elimu; elimu msingi mahitaji ni 1,274, lakini *actual* tulionao ni 674, na upungufu ni 450. Ukija kwenye elimu ya sekondari, mahitaji ni 683, halisi ni 583, kwa hiyo kuna upungufu wa 100. Kwa hiyo, pamoja na yote hayo tunayozungumza, lakini ni vema tukawajengea uwezo wa kibajeti, pia suala la watumishi na kuwajengea uwezo katika mifumo ambayo inafanya kazi kule, hasa mifumo hii ya kielektroniki ambapo imeonekana wazi kwamba ziko halmashauri nyingi ambazo zina upungufu wa watu wenye uwezo wa ku-manage mifumo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kutupitisha juzi kwenye mfumo huu wa TAUSI, sisi tumeuelewa kidogo, lakini tungependa kuuelewa zaidi. Sasa kama wenzetu kule hawatajengewa uwezo wa kutosha ambao ndio watumiaji wakuu wa mfumo huu, kutakuwa kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo linahitaji kujengewa uwezo ni juu masuala ya mikataba na manunuzi. Sasa pamoja na mafanikio haya na haya yote ambayo nimeomba kwamba wawezeshwe, bado katika mchakato wa kazi hii tulioifanya kwenye Kamati, yako mambo ambayo bado wangeweza kuyatimiza lakini hawaiyatimiza, nami nitazungumzia maeneo kama manne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, zipo kesi nyingi sana Mahakamani zinazoendelea na zilizokwisha. Kuna ambazo halmashauri zetu zinashtakiwa na kuna ambazo halmashauri zetu zinashtaki. Nikizungumzia zile ambazo tunashtakiwa, ziko ambazo nyingi tumeshindwa, lakini tukumbuke kwamba halmashauri haipelekwi Mahakamani kabla haijapewa notice ya siku 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wito wangu kwa halmashauri ni kwamba kwa kesi zile ambazo wanaona kabisa kwamba hapa mtu ali-supply kitu chake, kuna *delivery note*, kuna *invoice* na kila kitu, wanapopewa ile notice ya siku 90 watumie huo muda ku-settle hizi kesi kuliko kuacha ziende Mahakamani tushindwe halafu tuingie għarama kubwa ya kuja kulipa riba na għarama na kadhalika. Pale ambapo tumeshindwa, na kuna sababu za kukata rufaa, ni vizuri rufaa ikakatwa ndani ya muda ili tusiendelee kupoteza muda halafu tukaingia hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko *settlement* ambazo zimefanyika nje ya Mahakama, ni vizuri halmashauri zikafuata utaratibu wa kusajili zile *settlement* Mahakamani ili tusije tukaingia shida wakati wa utekelezaji wa hukumu tukashindwa kupata kile ambacho tunatakiwa kupata. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni masuala ya mikataba. Halmashauri zetu zinaingia kwenye mikataba mingi sana, ipo mingine mizuri na mingine mibovu; lakini upo udhaifu ambao ningependa kuuzungumzia. Udfaifu wa kwanza ni kutokufuata mikataba inavyotaka. Tumekutana na maeneo mengi sana ambapo mkataba wa ujenzi unasema kabisa kwamba kabla mkandarasi hajalipwa yale malipo ya awali (*advance payment*) lazima alete *advance payment guarantee*, lakini yapo maeneo ambako mkandarasi amelipwa bila *advance payment guarantee*, amefika mahali sasa ameshindwa, tunashindwa kupata zile fedha na hao wenzetu wakiulizwa huko, hawana maelezo kwamba kwa nini hamkuchukua *advance payment guarantee*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama Wanasheria wetu kule kwenye halmashauri au Maafisa Mipango au Wakurugenzi wanashindwa kusoma mikataba kwa mambo mepesi kama hayo. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo wanatakiwa kulikazia kuhakikisha kwamba wanafuata mikataba inavyosema. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna baadhi mikataba ambayo kwa kweli ni dhaifu. Yapo matukio ambayo tumekuta halmashauri tatu zimepewa dhamana moja kwa ajili ya mradi fulani, yaani mkataba unataka kwamba kabla yule mzabuni hajapewa ile tenda, basi

alete dhamana. Sasa mtu anakuja ameshinda *tender* kwenye Halmashauri 'A' analeta hati, anaweka pale, labda inapigwa copy hapo, kinyume kabisa na utaratibu, anaondoka nayo, anaenda kuchukua *tender* ya Halmashauri 'B' na Halmashauri 'C', sasa amefika mahali ame-default kote, wanashindwa ku-recover kwa sababu hati ni ile ile moja, kila mtu anaing'ang'ania na licha ya hivyo, utakuta thamani yake ni ndogo zaidi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika eneo kama hili, suala la kuchukua dhamana ni suala ambalo linafanyika na mabenki au na makampuni ya *insurance*, ambao wakishachukua ile dhamana, wao wanaisajili ile dhamana, halafu wanatoa *guarantee* kwa Halmashauri ili iendelee kumpa kazi yule mzabuni ambaye amepata. Wao wana uwezo wa kuchukua hata dhamana moja kwa halmashauri tatu kwa sababu wanazitengeneza kwa uratatibu wa *Pari-Passu* ambao unasajiliwa, na pale kunakuwa na *default*, kila mtu pale anapata haki yake, kwa sababu wanaangalia thamani ya ile dhamana, thamani ya mikataba ambayo inatakiwa kutoa dhamana ile, wanaitoa kwa utaratibu wa sheria na kunakuwa hakuna matatizo. Ila halmashauri zinapochukua kienyeji, ndiyo matokeo yake unakuta hati moja imedhamini halmashauri tatu tofauti na *default* inatokea, wote wanashindwa ku-recover. Tumelikuta hili sana kwenye halmashauri, tunaomba lizingatiwe kwa nguvu sana, lirekebishwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la kukabiliana na vitendo vya ubadhirifu, wizi, kughushi, matumizi mabaya ya madaraka na kadhalika. Hivi vitendo vinajitokeza kwa wingi kwenye halmashauri zetu, lakini imekuwa kama dini sasa kwamba likitokea tatizo, TAKUKURU; mtu anadaiwa

deni, peleka TAKUKURU; mtu amekimbia na hela za POS, amekusanya amekimbia nazo, peleka TAKUKURU; Mkandarasi hajamaliza ujenzi wake, peleka TAKUKURU. Sasa tunawajazia TAKUKURU mzigo wa mambo ambayo hata uwezo wao siyo mkubwa kiasi hicho. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote Waheshimiwa Wabunge, tuangalie kwenye majimbo yetu tuone Ofisi za TAKUKURU zina wafanyakazi wangapi; zina magari mangapi; zina resources kiasi gani za kukabiliana na haya mambo? Mengine ni mambo ya wizi yanayotakiwa yapelekwe Polisi yashughulikiwe na mambo mengine ni ya utakatishaji fedha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna halmashauri ambayo fedha za TANESCO za kwenda kufidia watu ambao zile waya za *high tension* zimepita kwake, zimekuwa diverted zikapelekwa kwenye vijiji, kutoka kule zikapigwa kwenye account za watu binafsi wakagawana, lakini mwisho wa siku unaambiwa Watendaji wa Vijiji wamepelekwa TAKUKURU, lakini wale wakubwa, huyu kahamishiwa huku na huyu kahamishiwa huku. Tunaipa mzigo TAKUKURU bure, tutailaumu wakati ambapo kwa kweli haya mambo wakati mwingine hayako ndani ya mamlaka yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosisitiza ni kwamba tusibebeshe TAKUKURU kila mzigo. Haya mambo yaende kwenye kila taasisi kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vina mamlaka ya kisheria na uwezo wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nimeliona lina-shout, yaani linaonekana kila mara, ni udhaifu unaotokana na matumizi ya force account hasa

kwenye miradi ya ujenzi. Utaratibu wa ujenzi uko wazi sana, kwamba mradi wa ujenzi unaanza na msanifu (architect) anachora, halafu unakwenda kwa mkadiriaji wa ujenzi (quantity surveyor) anakadiria kwamba ghamra ni kiasi gani, halafu kunakuwa na yule mjenzi; na mjenzi kuna contractor yule aneyejenga na kuna structural engineer; na kila mmoja hapa ana majukumu yake kisheria na yote ndiyo yanayopelekea kwenye kupata value for money.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu sasa ambao tunaukuta kule, unaenda unakuta mchoraji, yaani msanifu, Tadayo; mjenzi, Tadayo; sijui consultant ni huyo huyo. Kwa hiyo, hata zile certificate ni yeye mwenyewe anangalia, anajikadiria, anasema hapa nilipwe kiasi fulani. Tukiendelea hivi, hatutapata value for money. Tutapata product ambayo ni dhaifu na tusije tukalaumu sana hawa wakurugenzi au wale watu wanaosimamia ambao wengine ni walimu, lakini hao watu walioweka utaratibu kwamba miradi ya ujenzi iende na wataalamu wa fani mbalimbali walikuwa na maana kabisa kwamba bila hivyo hatuwezi kupata value for money. Sasa hiki ndicho kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikuta namna hiyo, utakapoenda kusoma lile bango la ujenzi, utakuta hata building permit hakuna, kwa sababu huwezi kupata building permit kama huja-involve hizi taaluma zote ambazo nimezitaja hapa. Kwa hiyo, hili jambo nadhani tunahitaji kuwa serious. Kama hatuna hao wataalam, tujaribu kutumia hata wataalam kutoka maeneo mengine ili tu kuhakikisha kwamba tunapata value for money. Hela inayokwenda kwenye halmashauri zetu kwa kweli ni kubwa, ni lazima tuitendee haki kwa kuhakikisha kwamba kazi inayifanyika inakidhi viwango. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, siyo mwisho kwa umuhimu, mimi binafsi katika mchakato wa kazi yetu ya kamati, nawiwa kabisa kuishukuru sana Ofisi ya CAG kwa kazi ambayo wamefanya. Ofisi ya CAG imekuwa mwalimu, imekuwa mlezi na imekuwa na umuhimu mkubwa sana katika hizi halmashauri zetu. Watakaofuata ushauri wao, watapona, lakini ambao hawataufuata watatuletea matatizo na hatutakubali kuendelea kuwa na matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja ya Kamati kama ilivyoletwala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Nimwite Mheshimiwa Shabani Ng'enda, wakati huo wafuatao; Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa George Natany Malima, wanajandaa.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, na zaidi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kuwa na afya ya kutumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema yale ninayokusudia kuwa ni mchango wangu katika eneo hili, napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa ziara nzuri yenye matumaini na iliyotutia nguvu sisi wawakilishi wa wananchi pamoja na Watumishi wa Serikali katika Mkoa wa Kigoma.

Ametufungua katika mambo mengi, ameelekeza mambo mengi ambayo kwa kweli yanakwenda kuipa Kigoma sura mpya ya maendeleo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunamwombea afya njema yeye pamoja na wanaomsaidia ili waweze kutimiza matarajio ya Watanzania. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizishukuru sana Kamati zote tatu zilizowasilisha hoja zake hapa Bungeni. Katika kuzishukuru, nipeleke shukurani vilevile kwa CAG kwa ofisi yake ya kufanya kazi nzuri ya kutupa miwani ya kutazama mambo mengine ambayo yanafanyika kwenye utendaji na sisi huwa hatuyaoni mpaka tuletewe na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujielekeza katika kuzungumzia hasa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya LAAC na PAC. Nianze na LAAC. Ushauri na mapendekezo haya yametolewa katika ukurasa wa 19 hadi 24 wa taarifa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia uwekezaji wenyе tija. Uwekezaji wenyе tija maana yake Halmashauri zetu zinapowekeza, ziwekeze katika maeneo ambayo zinakwenda kupata tija, zinaongezea mapato na mapato yale yanasakiha hata halmashauri zenyewe kuweza kufanya miradi ya maendeleo kutohara na fedha wanazokusanya kwa makusanyo ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana hapa kuna miradi mingine watu wanafuata mkumbo tu, kwamba madhali halmashauri fulani wana stendi na sisi stendi; madhali wana soko, na sisi soko; basi ni miradi kama hiyo. Kwa ujumla niseme, kwenye eneo hili napenda kuishauri Serikali kwamba zipo halmashauri ambazo zinakuwa na

matatizo ya kubuni miradi na kuisimamia kutokana tatizo la wataalamu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, nichukue Manispaa yangu ya Kigoma Ujiji. Manispaa ya Kigoma Ujiji ni mionganini mwa Manispaa ambazo zina makusanyo madogo, kiasi kama cha Shilingi bilioni tatu kwa mwaka, kiasi ambacho unaweza ukasema ni kidogo sana. Halmashauri hii ina tatizo kubwa la wataalamu. Ukienda kwenye wahasibu ni tatizo, ukienda kwenye wakaguzi; Manispaa nzima ina mkaguzi mmoja, yaani afanye kazi zote za ukaguzi zinazotakiwa kufanywa, wahandisi ni tatizo, valuer ni tatizo. Kwa hiyo, tuiombe Serikali iwezeshe halmashauri zetu kupata wataalamu ili waweze kubuni miradi na kuisimamia vizuri, hapo tutaweza kusaidia kuongezeka kwa mapato ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, wamesema hasara zitokanazo na taasisi za Serikali. Zipo hasara ambazo Halmashauri zinapata kutokana na taasisi za Serikali. Moja ya taasisi iliyotajwa ni MSD. MSD inatajwa kwa sababu inalipwa fedha kwa ajili ya kuleta vifaa vya hospitali; vitanda vya hospitali na madawa, baada ya kulipwa fedha wanachukua miezi mitatu, minne, mitano, sita hawajaleta vifaa hivyo. Kwa hiyo, wanaitia hasara halmashauri.

Mheshiniwa Mwenyekiti, kuna taasisi kama TEMESA, hawa yaani sijui niseme, ingekuwa ni mamlaka yangu, ningeweza kuangalia: Je, inastahili kuendelea kuwepo au isiwe? Yaani hawa ukienda, unataka kukagua magari, unataka kutengeneza gari, hawana wataalamu, hawana vipuri, waende tena kwenye maduka ya watu binafsi wakatafute vipuri hivi, gharama ya TEMESA inakuwa gharama kubwa kuliko gereji za watu binafsi. Kwa hiyo,

Iazima serikali iangalie eneo hili. Tumeweka kwa nia njema, lakini tusipoangalia litakuwa mzigo kwa Serikali na mpaka sasa *TEMESA* ni mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GPSA*; yapo malalamiko ya Idara za Serikali chungu mzima, zimeingiza pesa *GPSA*, kwa ajili ya kulipia magari, mwaka mzima mpaka leo hawajapata magari. Mwezi Novemba kuna taasisi zimeingiza pesa, mwezi Novemba huu hawajapata magari. Magari hayo yalitakiwa kuja kufanya kazi kwa ajili ya kuongeza tija kwenye Serikali, lakini *GPSA* wamepewa, hivi Serikali wanakwama wapi Ukienda gereji *TOYOTA* ukiwapa oda miezi mitatu wamekuletea gari, mwaka mzima *GPSA* hawajaleta gari.?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi nyiningine iliyoyatajwa ni *NHIF*. *NHIF* imetajwa kwa maana ya kwamba uko mfumo ambao nataka niishauri Serikali waone jinsi ya kuubadilisha. *NHIF* inaingia mkataba na hospitali za Serikali na binafsi kwa ajili ya kuhudumia wateja wao ili wao waweze kuwalipa. Wanapokwenda kuhakiki malipo, *NHIF* wanaamua haya tutalipa haya hatulipi labda kuna kasoro fulani fulani na wakishaamua wao ndiyo wa mwisho. Haiwezekani, tukawa na mamlaka ambayo yenyewe inaingia mkataba na watu na wakitofautiana yenyewe ndiyo yenyewe mamlaka ya mwisho ya kuamua, nikulipe au nisikulipe. Hata mikataba mbalimbali, hata ya Serikali, mnaambiwa kwamba tukitofautiana, tutatafuta arbitration kabla ya kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa arbitration ya hawa *NHIF* na zahanati zetu za Serikali na zahanati za watu binafsi, ni nani? Kwa hiyo lazima kitafutwe chombo hapa ambacho kitakuwa kati, iwapo *NHIF* watasema mimi siwezi kulipa, basi huyu aliyetoa huduma akimbie kwenye

chombo hicho aseme NHIF wananiaonea, nimetoa huduma hawataki kunilipa. Hilo ndilo wazo langu ambalo ningependa kuishauri Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Kamati ya PAC ukurasa wa 28, kuna suala la Polisi, kutoandaliwa kwa hesabu na kufanyika kwa ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Polisi. Kamati imelieleza vizuri, huu Mfuko upo kwa mujibu wa sheria ‘*The Police Force and Auxiliary Service Act, Cap No. 322*’, lakini CAG amebaini kwamba, kwenye Mfuko huu kuna pesa zimebekwa kwenye Benki Kuu, bilioni 35.3, lakini pesa hizi hazikaguliwi wala haziletwi taarifa yake katika ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo hivi sisi tunaviheshimu sana, vyombo vyetu hivi vya ulinzi. Tungependa viwe *clean*, wanafanya kazi nzuri, wasichafuliwe na mambo haya madogo madogo. Mimi niombe sana kwamba utaratibu usimamiwe chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kuhakikisha mifuko kama hii ambayo nia yake ni njema inakaguliwa na utaratibu unafanyika. Mzee wangu, mzee Yusuph Makamba aliwahi kusema, ukiumwa na nyoka utatibiwa na mzizi, sasa ukiumwa na mzizi unatibiwa na nini? Maana hawa polisi ndio kazi yao kukamata wezi na wahalifu, sasa kama wao ikitokea uhalifu tunafanyaje, kwa hiyo hivi ni vyombo vya kuviangalia sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kuna Idara ya Uhamiaji, kwenye idara hii ukaguzi maalum ulifanywa kwa mujibu wa kifungu cha 93, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikitoa stika bandia za visa. Hizi DCI alibaini katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere. Vitendo hivi na stika hizi zimekuwa zikiingia kupitia KIA. Sasa CAG baada ya kufanya ukaguzi kwa kipindi cha miezi sita tu,

CAG amebaini kwamba kuna upotevu wa kiasi cha Shilingi bilioni 2.4 na kuna Maafisa 32 wa Idara ya Uhamiaji ambao wanahusika na wamefika mahali wakacheza na kanzidata na kufuta kwenye kanzidata watu ambao walilipa visa, ambao ni wa nje watu 21,208.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mapato makubwa sana ya Serikali na vitendo hivi vimekuwa vikifanyika huko zamani. Hata huko Kigoma waliwahi kiwajibishwa Maafisa Uhamiaji kwa kugonga muhuri wa entry halafu ile nanii ya visa hawakukata au dola hamsini wanachukua dola 30 wanaacha dola 20, waliwajibishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nashukuru Mungu Kigoma mambo ni mazuri, tunaye Afisa Uhamiaji na Mkuu wa Mkoa ambaye wanasmamia mambo vizuri, yanakwenda vizuri. Uzoefu ule wa Kigoma ungeweza ukatumika kuangalia maeneo mengine yote na huu uliojitokeza KIA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofij*)

MWENYEKITI: Nimwite Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, wakati huo Mheshimiwa Ravia Idarusi Faina na Mheshimiwa Fransis Ndulane ajiandae.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru sana Rais wetu mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Pia, ye ye akiwa kama Rais wetu tunaona nia njema ambayo anayo kwa nchi yetu kwa kumpa maelekezo CAG, kwamba afanye uchambuzi wa kina, asipepese macho, aandike ripoti yenyé kueleweka

ili tuijenge nchi yetu. Ripoti hii ya CAG ambayo tunaiangalia leo sisi kama Wabunge tunapaswa kutimiza jukumu letu la kuismamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi ambayo yameelezwa ndani ya Ripoti ya CAG, lakini mawili makubwa ambayo ningependa kuyaangalia; kwanza ni uwekezaji wenyе tija, lakini pia kuangalia sehemu ya matumizi. Tunazungumzia Mitaji ya umma, kwangu mimi moja ya mitaji mikubwa ya umma ni nguvu kazi, ni rasilimali watu. Katika ripoti hii ya CAG, tunaona kuna watoto 53,755 ambao wanaandikishwa kuanza darasa la kwanza kati ya mwaka 2018 na 2021 ambao hawakumaliza elimu ya msingi. Tunafahamu nchi yetu inawekeza fedha nyingi sana kwenye elimu ya watoto wetu, kile ambacho kinaitwa elimu bure sio bure, mlipakodi wa nchi hii analipa fedha nyingi kama *capitation* kwa ajili ya watoto wetu waende shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa ambao wanaandikishwa darasa la kwanza hawafiki la saba, maana yake uwekezaji mkubwa ambao unafanywa na nchi hii na walipa kodi wa nchi hii unapotea bure. Ningemba kwa unyenyekevu kabisa, Bunge na Serikali kuchukulia ripoti hii kwa umakini mkubwa. Watoto 53,755 si idadi ndogo, watoto hawa wanaondoka katika mfumo katika elimu ya msingi. Tunapozungumzia elimu ya msingi huko ndiko tunapojenga Taifa, zile *manners* ndogondogo, raia mwema anatakiwa ku-behave vipi, kuheshimu wakubwa na wadogo, kuheshimu mamlaka, zote zinafunza katika katika shule ya msingi na ndiyo maana inaitwa msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuta watoto hawa wanaondoka katika mfumo huu wa elimu ya msingi, maana yake sio tu tunapoteza Watoto, lakini ni suala la security ya nchi yetu. Watoto hao wako wapi? Wanafanya nini? Wamekwenda wapi? Nani ambaye anasumbuka kujua watoto hawa wapo wapi? Watoto 53,755 si watoto wachache na hili ni suala la security ya nchi yetu na ni lazima tulichukulie kwa uzito ambao unastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kuwekeza kwa wananchi wetu, kama ilivyo kwenye elimu tunavyowekeza kwa hawa Watoto, lakini pia Serikali imekuja na mpango maalum kabisa wa kuwezesha makundi maalum ya vijana, wanawake na walemavu. Fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya makundi haya, kuyakwamua katika hali ya umaskini ni fedha nyingi sana ukilinganisha na mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua bajeti yetu ya nchi, fedha ambazo tunalipa madeni, fedha ambazo tunalipa mishahara ya watumishi wa umma, fedha kidogo ambayo inabaki kwa ajili ya maendeleo, hatuna anasa ya kupoteza hata shilingi tano. Hatuna anasa hiyo, kwa sababu tunapambana kukusanya hela ambayo inaishia kwenye mahitaji ya lazima, hatuna fedha za kufanyia anasa. Unaposikia fedha zinapotea, fedha za umma zinapotea, inaumiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hesabu ambazo CAG amewasilisha kati ya mwaka 2020/2021, zaidi ya bilioni 75 za mikopo zilitoka katika mwaka huu mmoja wa bajeti. Katika hizo zaidi ya bilioni 47 hazijarejeshwa. Fedha hizi ni nyingi sana, fedha hizi zinaweza zinaweza kubadilisha maisha ya watu wengi

katika nchi hii, kutengeneza barabara za vumbi kuwa za changarawe kilometra za kutosha; kutengeneza lami nyepesi, kutengeneza shule za msingi, shule za sekondari, zikakarabati vyuo vya ufundu, zikapeleka hata vifaa tiba katika hospitali. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposikia kuwa fedha hizi zimepotea na hatuoni jitihada za kweli za kuzikusanya fedha hizi, Bunge lako haliwezi kunyamaza. Ningombwa kwa namna ya kipekee, kwanza kabisa nishukuru Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuna jitihada za wazi ambazo imezichukua kuhakikisha kwamba wanaenda kusimimamia suala zima la utoaji wa mikopo lakini pia ukusanyaji wake. Ni hatua nzuri lakini jitihada pia zifanyike, kuhakikisha kwamba zile fedha ambazo zimetoka kimichongo wahusika wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa mkopo ni suala moja na suala la haki kwa makundi ambayo yanastahili kupata mkopo ni suala lingine. Wote ni mashahidi, juzi tulikuwa na mjadala mrefu sana kuhusiana na haki ya mikopo kwa wale ambao wanastahili elimu ya juu. Vijana wetu ambao wameomba mikopo na wanastahili kupata mikopo lakini hawajapata mikopo, hali si tofauti kwa mama zetu kwa vijana na wale mavu katika halmashauri tunazotoka. Kuna makundi mengi ambayo yanastahili kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uwazi kwenye ugawaji wa fedha hizi, linafanya makundi mengi ambayo yanastahili kupata fedha hizi wasizipate. Matokeo yake, Wabunge na Madiwani wamekuwa wahanga wa lawama kutoka kwa makundi haya na wenye we wanabakia kulalamika kwa sababu hata ushirikishwaji wao si mkubwa ukilinganisha na majukumu walijonayo

hasa kuwa sehemu ya majibu ya changamoto kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba tena, nilizungumza mwaka jana, lakini nazungumza tena leo, rasilimali za halmashauri kutumika kwa uwazi, kutumika kwa haki na wale wote ambao wana haki ya kupata fedha hasa hizi za *ten percent*, basi wajulikane na taratibu zijulikane na wao wanufaika wapate fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mgawanyo wa fedha za asilimia 40 kwa 60. Kwa maana fedha za matumizi mengineyo, lakini pia fedha za maendeleo. Haiyumkiniki na sijadili busara ya hawa ambao walitengeneza vigezo hivi, lakini napata shida sana kuona kwamba kuna halmashauri ambayo inapata bilioni 30, inaambiwa itenye asilimia 40 kwa ajili ya matumizi mengineyo na halmashauri nyingine ambayo inapata milioni 800 ama bilioni moja na yenyewe inaambiwa itenye asilimia 40 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiziangalia hizi halmashauri, utakuta huyu ambaye anaingiza bilioni moja anajitahidi kulipa malimbikizo ya posho za watumishi wake, Wauguzi na Walimu, lakini utakuta huyu ambaye anapata bilioni 30 hajishughulishi na madeni ya watumishi wake. Pia, hata kupeleka fedha ambazo kisheria anapaswa kupeleka, kwa maana ya asilimia 10 hapeleki. Sasa, rai yangu kwa Serikali tujaribu ku-review mgawanyo wa fedha za matumizi mengineyo na fedha za maendeleo. Ikiwapendeza waone mgawanyo wa haki ili fedha nyingi ziende kutibu matatizo na changamoto ambazo Serikali kuu haiwezi kuzibeba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilizungumze hapa, ni suala la matumizi ya hii akaunti ya Amana. Ripoti inaonyesha kwamba kimekuwa ni kichaka cha kufichia fedha, lakini pia kufanya ubadhirifu. Ni rai yangu, hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile matumizi ya bakaa, fedha za bakaa kwa maana ya salio ambalo halmashauri inaingia nalo katika mwaka mpya wa fedha. Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa zinaitaka halmashauri kuripoti kwenye vikao katika robo ya kwanza, lakini haizungumzii baada ya robo ya kwanza wanaripoti wapi na chenyewe ni kichaka cha matumizi mabaya ya fedha za Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwa Serikali na ikipendeza Bunge lako, ripoti ya matumizi ama kuchunguza akaunti za amana kwenye halmashauri zetu, lakini pia matumizi ya fedha za bakaa, ripoti hiyo ije kwenye Bunge tuijadili, kuona uhalali na matumizi sahihi za fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la uwekezaji wenge tija; halmashauri nyingi zimewekeza kwenye kile ambacho kinaitwa miradi ya kimkakati. Kwa mfano, stendi za malori na za mabasi lakini pia masoko. Pia, kuna halmashauri ambazo hazina wataalam wa kuandika maandiko, hazina utaalam huo, nyingi zimeishia kuwa wahanga wa mfumo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kuna ajenda ya kuzisaidia halmashauri hizi, ikiwemo Kilosa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Ravia Idarusi Faina na Mheshimiwa Francis Ndulane ajiandae.

MHE. RAVIA IDARUS FAINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kusimama mbele ya Bunge lako na kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi limeanzisha Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa Jeshi la Polisi, Mfuko huo kwa ajili ya ustawi wa askari, lakini cha kushangaza mpaka sasa hivi hakuna kanuni za kusimamia uendeshaji wa Mfuko huo, hivyo inapelekea kuwa na wasiwasi wa matumizi ya Mfuko huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi limeweka vizuri sheria na miongozo yake kwenye PGO. Kwa nini hawataki kufuata taratibu hizo walizojipangia hasa kwa askari wadogo. Kwa mfano, posho za maaskari wadogo haziendani na vyeo vyao, kama vile posho za mavazi, udereva, kibaka chekundu na kadhalika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, posho za safari, wanapofuata watuhumiwa kutoka mkoaa mmoja kwenda mkoaa mwingine hawalipwi. Sasa, naishauri Serikali kwa vile katika ripoti ya CAG imebainisha kuwa fedha zinazokusanywa kwenye Mfuko wa Polisi ambazo ni tuzo

na tozo, hazipangiwi sheria na kanuni za matumizi yake. Sheria na matumizi yake yaratibiwe kwa mujibu wa Sheria ya Fedha iliyokuwepo nchini ili ziweze kuondoa hizo changamoto za maaskari wadogo na stahiki zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri Serikali...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ravia Faina, unapokuwa unachangia, unawasiliana na Mwenyekiti moja kwa moja, ili isionekane unasoma au unaawaangalia watu wengine, kwa hiyo ni vizuri ukakiangalia kiti moja kwa moja.

MHE. RAVIA IDARUSI FAINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vile vile, nashauri fedha hizo aidha zitumike kwa ujenzi wa vituo vya polisi pamoja na nyumba za askari ambazo zimechakaa sana. Mashirika na taasisi za umma ziache mara moja kujilingiza kwenye shughuli zinazoweza kufanywa na vijana wetu na akinamama ambao wanataabika na ukosefu wa ajira kama vile usafishaji wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Faina. Nilimuita Mheshimiwa Francis Ndulane wakati huo Mheshimiwa Kwagilwa anajiandaa.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza jioni hii ya leo kuchangia taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, CAG. Nitachangia kwenye Kamati mbili, Kamati ya LAAC pamoja na Kamati ya PAC. Kabla

ya kuchangia ninaishukuru sana Serikali inayoongozwa na Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuwekeza fedha nyingi katika miradi ya maendeleo ambayo kuitia hiyo miradi ndiyo taarifa nyingi tumezipata hapa ambazo zinaonesha kwamba kuna hoja nyingi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane kwanza na Mbunge wa Kasulu, Mheshimiwa Vuma, ambaye asubuhi aliongea kwa kirefu kuhusiana na mapengo katika Bodi za Wakurugenzi kwa Taasisi zetu nyingi za Umma. Kwa kweli kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi au kuwa na Bodi za Wakurugenzi zenyet mapungufu kumepelekea kuwa na mapungufu makubwa katika uendeshaji wa taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema kwamba ilitolewa taarifa hapa kutoka kwa Mheshimiwa Mtaturu, akitolea mfano wa Klabu ya Simba na ubora wa Bodi yake ya Wakurugenzi, akazungumzia namna ambavyo timu fulani maarufu ambayo jana ilicheza katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika, namna ambavyo imeshindwa ku-cope na mazingira ya utawala bora ambayo yanafanikishwa katika Klabu ya Simba, ambayo tangu wameunda Bodi ya Wakurugenzi imara, miaka mitano iliyopita wamekuwa wakifanya vizuri kwa kucheza hatua za makundi katika mashindano ya vilabu Barani Afrika na kuweza kuiwakilisha nchi yetu katika hatua mbalimbali ikiwemo kufika hatua ya robo fainali. (Makofii)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

3 NOVEMBA, 2022

MWENYEKITI: Ngoja kwanza kuna taarifa, nafikiri Mheshimiwa alikuwa anataka kuelezea pia kwamba Bodi hiyo inasaidiaje kwenye timu za ndani au ni nje tu. Karibu Mheshimiwa Getere. (Makofi)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayechangia, mchango huo haupo kwenye taarifa za Kamati. Mimi naomba aifute.(Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndulane unapokea taarifa?

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hii taarifa kwa sababu hii mifano tunayoitoa ni mifano muhimu. Wenyewe mmeona jana hali ilivyokuwa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anachozungumza ni vitu ambavyo vinagusa watu rohoni na yaliyotokea jana ni mambo ya kawaida, sasa huwa yanatokea bahati mbaya hata yeye mwenyewe yalishamtokea, sasa ningeomba hiyo hoja aiache. (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndulane zingatia yaliyokutokea huko nyuma, unapoke taarifa ya Mheshimiwa Musukuma?

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaipokea kwa lengo la kuweka msisitizo

kwenye jambo hili. Tunawaombea ndugu zetu katika mechi ya marudiano kwa sababu hakuna nafasi nyingine ya kuwasaidia ni kupitia mazungumzo kama haya ndiyo maana tumeamua kusema, kwa hiyo, wana nafasi ya kujirekebisha kwenye mechi ya marudiano. Tulisema tangu kwenye Kikao cha Bajeti wakati tunachangia Wizara ya Michezo kwamba jamani hakuna dhambi kwenda kusikiliza ushauri kutoka kwa watani! Hapa kwenye Bunge hili tunae mmoja wa wanabodi ya Wakurugenzi ya Simba.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kuna taarifa, Mheshimiwa Rama eeh!

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:
Mheshimiwa Mwenyekiti, tungemuomba mchangiaji ajielekeze kwenye hoja zilizoko mezani. Simba na Yanga hapa siyo hoja ya leo ya kujadili. Kwa hiyo, ajielekeze kwenye hoja za Kamati zilizosomwa za PAC LAAC na PIC. Tuendelee mbele nchi hii inataka kusikiliza mawazo yake siyo habari za Simba na Yanga.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndulane unapokea taarifa?

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Siipokei taarifa lakini niishie hapo na ninawataki kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kwenye taarifa rasmi za Kamati zetu tatu, especially zile mbili za LAAC na PAC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na Kamati ya LAAC, taarifa ambayo waliitoa ilikuwa ni nzuri, imebainisha madhaifu mengi ambayo yalitokana na taarifa ya ukaguzi ya CAG. Nikienda moja kwa moja kwenye usimamizi wa miradi, dosari zilijitokeza nyingi lakini nijikite pale ambapo ilionekana kwamba kuna upotevu kwenye *interest* ambazo zilikatwa kutokana na malipo ya jumla ya Shilingi Bilioni 664,0 ambayo ilizalisha *interest* jumla Shilingi Bilioni 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukailaumu taasisi ya TANROADS wakati kumbe mfumo wetu wa malipo una changamoto nyingi. Huko tulikotoka tulikuwa tunatumia mfumo katika kulipa na kuandaa malipo ya Wakandarasi. Katika mfumo huu unatoa siku 56 ambapo inatakiwa Serikali imlipe Mkandarasi anapokuwa amefanya kazi, kinachoonekana kule nyuma tulikuwa tunakwenda vizuri kwa sababu hizi siku 56 zilikuwa zinagawanywa, siku 28 Consultant anatakiwa aandae *certificate*, iwe *approved*, ipitiwe lakini mwisho wa siku wanaisukuma TANROADS. Iifikika TANROADS kuna kitengo kinaitwa *IDA* kinasimamia malipo yote ya kazi za wale *development partners*, yale malipo ambayo yanafadhiliwa na wafadhili mbalimbali wa nje ya nchi. Tukifika pale nao wanapitia zile *certificates*, pamoja na wale *Engineers* wanapitia, wakishapitia inaenda kwa *Desk Officer* wa Wizara ya Fedha na Mipango ambapo kazi yake ni kuangalia usahihi wa yale malipo ambayo yameandaliwa au yale madai ambayo yameandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatimaye akishapitisha, na ni kazi inachukua kama masaa mawili tu, baadae zile *claims* zinarudi TANROADS, baadae zinakwenda kwa *development partner* naye anajiridhisha, malipo yako

sawa. Baadaye yanalipwa ndani ya siku 56 Mkandarasi anakuwa tayari ameshalipwa. Hii ilikuwa inazuia kupatikana kwa hizi *interest* ambazo tunaziona leo kwenye hoja za ukaguzi za CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo sasa hivi certificate ikishaandalika ikitoka kwa Mkandarasi inakwenda kwa consultant, ikitoka kwa consultant inakwenda TANROADS wanaipeleka Wizara ya Ujenzi. Pale kuna maafisa wasiopungua wawili wanashughulikia lakini ikitoka hapo inakwenda kwa Permanent Secretary wa Wizara ya Fedha na Mipango. Ikitoka pale kuna Maafisa zaidi ya Kumi wanasimamia, unapita katika mlolongo wa Maafisa zaidi ya Kumi. Ikitoka hapo inarudi TANROADS. TANROADS baadae inarudi kwa development partner, nae anajiridhisha hatimaye ndiyo inalipwa. Kwa hiyo kuna maafisa zaidi ya 15 wanahusika na malipo na matokeo yake ndiyo haya sasa tunayoyaona leo kwamba kuna fedha nyingi Serikali inalazimika kuongeza kulipia ile miradi kwa sababu ya uwepo wa riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo. Kwa maana zile siku 56 zinakuwa hazitoshi kulipa Mkandarasi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwa upande wa Serikali zetu za Mitaa, nilikuwa naperuzi vizuri sana kuhusiana na wingi wa hoja za ukaguzi katika Halmashauri zetu. Katika Halmashauri zetu nilitazama Halmashauri ya Korogwe nilikuta ina hoja ambazo hazijafungwa 91. Halmashauri ya Bumbuli ilikuwa na hoja za ukaguzi 89 ambazo hazikufungwa mpaka wanakuja kwenye Kikao cha LAAC. Kuna Halmashauri ya Msalala ilikuwa na hoja 61. Halmashauri ya Bunda ilikuwa na hoja 56 ambazo hazijafungwa mpaka wanafika kwenye Kamati ya LAAC. Nini nataka kusema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa, Halmashauri hizi zimekuwa na hoja nyingi za ukaguzi ambazo wameshindwa kuzijibu kwa sababu wameshindwa kuvitumia vizuri vyomba vyatani ya Halmashauri katika kukabiliana na hizi hoja. Kwa mfano, tunavyo vitengo vyetu vyatani ya ukaguzi wa ndani, vile vitengo vimkuwa havitumiki sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza, haviwezesewi kufanya kazi zake sawasawa. Vifaa vyatani usafiri hawana, vifaa vyatani ofisi hawana lakini mwisho wa siku hata ile *audit independence* imekosekana kwa hiyo wanajikuta mwisho wa siku, wale Wakaguzi wa Ndani wamekuwa kama ni watoto yatima ndani ya Halmashauri wakati ilitakiwa wawe msaada mkubwa kwa Maafisa Masuuli katika kuisimamia halmashauri. Kwa hiyo, ombi langu katika jambo hili ni kwamba Halmashauri ziwatumiye vizuri Wakaguzi wa Ndani katika kipindi hiki cha mpito, na kwakuwa Wizara ya Fedha iliahidi kwamba itarekebisha mfumo wa usimamizi wa hawa wakaguzi wa ndani. Ninawaomba waharakishe ule mchakato ili mwisho wa siku ikiwezekana hawa Wakaguzi wa Ndani wapelekwe katika Ofisi ya *Chief Internal Auditor* wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hii inaitwa *Audit Committee*, hii ndiyo msaada kwa Maafisa Masuuli wa Halmashauri ambao ni Wakurugenzi. Kuwepo kwa Kamati hii inawezesha kwanza kufanya mapitio ya fedha zinazoidhinishwa za bajeti kabla hazijaenda kwenye Baraza la Madiwani na kabla hazijaja huku kwenye Bunge. Pia mwisho wa siku inawezesha kupitia hoja zote za ukaguzi wa ndani na nje ili kuwezesha kuboresha kile ambacho kinaonekana kina dosari. Kwa hiyo, ninaomba

pia Maafisa Masuuli wazitumie vizuri hizi Kamati za Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. (Makofij)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ndulane kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, wakati huo Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo wanajиandaa.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia ripoti za Kamati zetu tatu. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Kamati ya Hesabu za Serikali. Mimi nitajielekeza zaidi kwenye Kamati hii iliyochambua ripoti ya CAG ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nimeisoma vema ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye eneo la Mashirika ya Umma. CAG amepitia Shirika la Bandari (TPA), TTCL, TANESCO, Shirika letu la Nyumba - NHC na TRC. Nitajielekeza kwenye Shirika la TANESCO na hususan kwenye mradi mkubwa tulionao. Mradi wa Trilioni 6.5 wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CAG anasema alivyokwenda kuangalia bwawa hili alikuta ujenzi umechelewa kuisha kwa asilimia 46.45. Bwawa hili ni la muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, Watanzania wanahitaji bwawa hili likamilike ili tuweze kupata umeme wa uhakika. Viwanda vyetu vinahitaji bwawa hili likamilike

ili viweze kufanya uzalishaji. Miradi yetu ya REA tunayoitengenza sasa inahitaji bwawa hili likamilike ili iweze kupata source ya umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gridi yetu ya Taifa ili iwe na umeme *stable* inahitaji bwawa hili likamilike ili tuweze kupata umeme wa uhakika. Vilevile, gharama zetu za umeme ziko juu, umeme wa maji ni umeme *cheap* kuliko umeme wowote, Watanzania wanahitaji bwawa hili likamilke ili waweze kupata umeme wa gharama nafuu. Sasa taarifa zilizopo hivi sasa, ukizingatia hii taarifa ya CAG, kwamba ujenzi umechelewa, bwawa lilitakiwa likamilike mwaka huu mwezi wa Sita, mwezi wa Sita umepita bwawa halijakamilika, hivi sasa ujenzi uko asilimia 74 na bado hujakamilika, Mkandarasi na Serikali wanabishana. Mkandarasi anaomba kuongezewa miaka mingine miwili zaidi na kwa maana hiyo kwa mujibu wa Mkandarasi, bwawa hili litakamilika mwaka 2024. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wao wanasema kwamba wamekataa kumwongeza miaka miwili, badala yake wamemwongeza mwaka mmoja. Nataka nilipitishe Bunge hili sababu ambazo zimetolewa na Mkandarasi na mpaka wakafikia kumwongeza mwaka mmoja, pamoja na kumwongeza huo mwaka mmoja yeye bado mpango kazi ambao ameuweka Serikalini unaonesha ni miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, anaomba nyongeza ya muda na kuongezewa gharama kwa sababu watengenezaji wa mitambo walijitoa. Sababu ya pili, anaomba nyongeza ya muda na gharama kwa Watanzania kwa sababu ya taarifa za miamba. Sababu ya tatu, anaomba kuongezwa muda na ongezeko la gharama kwa sababu pale site anasema

umeme haumtoshi. Sababu ya nne na ya mwisho, anaomba kuongezewa muda na gharama kwa sababu njia ya kupelekeea vifaa site ni mbaya. Jambo hili halikubaliki. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Trilioni 6.5, kodi za Watanzania, bado inafanyika janjajanja ya kutaka tena kuongeza gharama ya mradi huu? Kuongeza gharama ya muda na gharama ya fedha? Serikali inasema sababu zilivyotolewa haikukubaliana nazo. Kama hawakukubaliana nazo nataka Waziri mwenye dhamana akija hapa atuambie, kama sababu hizi hamkukubaliana nazo kwanini mmemwongeza mwaka mmoja? Kwa nini mmekubali kumwongeza mwaka mmoja ilihali mpangokazi wake unasema anataka miaka miwili, nani mnandanganya? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na Mkandarasi wameunda Bodi inayoitwa DAB, (*Dispute Adjudication Board*) kwa ajili ya kufanya suluhi ya haya. Mkataba Serikali umesema kwamba sababu hukubaliani nazo, inamaana ultakiwa ukabidhiwe kazi mwaka huu, mkataba unasema nini kama kazi haijakabidhiwa? Kwa nini madai ya Serikali kwa Mkandarasi hapa hatuyaoni? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza mpaka sasa Mkandarasi tumeshamlipa asilimia 65.9 ya fedha. CAG anasema mradi umechelewa, Mkandarasi tumeshamlipa asilimia 65.9 ya fedha zote yaani Trilioni 4.3, lakini Serikali badala ya kulipa trilioni 4.3, wamemlipa trilioni 4.43. Wamemlipa ziada ya shilingi bilioni 113. Sababu waliyoitoa ya kulipa ziada ya shilingi bilioni 113 wanasema eti ni mabadiliko ya kubadilisha dola na shilingi.

3 NOVEMBA, 2022

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa
Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa wapi?

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa
Mwenyekiti hapa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Twaha Mpembewne.

TAARIFA

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa
Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji
kwamba tofauti hii anayoizungumzia hapa ya fedha ya
Bilioni 113 fedha za walipa kodi zilizolipwa kwa uwiano wa
kawaida tu, kwa fedha tulizokuwa tumezizoea kawaida
kwa kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, Shilingi Milioni 500
inajenga kituo kimoja cha afya. Kwa hesabu za kawaida
hivi ni vituo 226 vya afya ambavyo vingeweza kujengwa
katika Jimbo la Handeni, Kibiti na Majimbo mengine yote
hapa Tanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa unaipokea
taarifa?

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa
Mwenyekiti, hiyo taarifa naipokea, shilingi
113,196,370,381.06 eti kwa sababu ya kubadilisha dola na
shilingi, mkataba gani huo kwenye nchi ya wanasheria
wasomi? Yaani unawezaje kuwa na mkataba wa hivyo?
Eti kwenye malipo mkianza kulipana wewe ukianza
kutafuta dola unapoteza bilioni 115. Vituo 226 vya afya!
Hatuwezi Kwenda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi wengine lazima tuwaambie tu, kazi yetu hapa ni kuwaambieni ukweli. Sisi sote tutapita lakini Tanzania itabaki. Bilioni 113 kubadilisha shilingi na dola, naongelea bilioni; hii si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu mkubwa mpaka sasa taifa halina uhakika kama utakamilika. Kwenye hili tuisitake kuumau ma maneno. Kutokukamilika kwa mradi huu kunafanya wananchi wa Handeni hawatapa umeme; kutokukamilika kwa mradi huu kunafanya ndugu Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo yenu miradi ya REA tunayopeleka haitakuwa na source ya umeme. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwa lugha fupi, kwamba hii ni hujuma. Tunanunua umeme kwa ghamra kubwa sana kutoka mitambo ya kukodisha. Kwa nini hatumalizi wa kwetu? Kwa nini mtu asishawishike kuamini kwamba hii ni hujuma? we cannot go like that as a nation, hatuwezi kwenda hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu leo tuko hapa kuisimamia Serikali ninamwomba Mheshimiwa Spika, aunde kamati tuchunguze hili. Haiwezekani mradi amba ni tegemezi kwa taifa usikamilike kwa wakati, na bado panaanzishwa longolongo nyingine zitakazopelekea tulipe zaidi na tukabidhiwe mradi baadaye zaidi, na huenda hata usikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mikubwa tunchi hii ya kwanza SGR trilioni 16, huu tunaotengeneza. Mradi wa pili ni huu takriban trilioni saba why can't we be serious on this.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa muda nawashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Venant Daud Protas, wakati huo Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge wajiandae.*

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia mawasilisho ya Kamati tatu zinazosimamia fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza wachangiaji waliotangulia, na nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa kuona unyeti wa kujadili fedha za wananchi na fedha za walipa kodi kwa kina ili kuona namna ya kutekeleza ripoti ya CAG, kama jicho letu kama Bunge kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mama yetu ya Mama Samia ambayo imekuwa ikitafuta vyanzo na ikitafuta fedha usiku na mchana. Serikali imekuwa ikisafiri kutafuta wahisani mbalimbali kuja kuwasaidia Watanzania. Lengo la Serikali si kumaliza matatizo yote ya wananchi lakini angalau kupunguza shida zao kama inavyoonekana kule kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa leo tunajadili ripoti ya kamati tatu, Kamati inayosimamia halmashauri zetu (LAAC), Kamati ya Mitaji ya Umma na Kamati ambayo inasimamia Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na michango mingi sana ya Wabunge; nikianza kwanza na Kamati ya kwanza inayosimamia halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo moja, unakuta Waziri Mkuu anakuja kwenye maeneo yetu kukagua miradi, Waziri Mkuu ndiye anayekuja kugundua kuwa top za milango zina ufa; Waziri Mkuu anakuja kwenye miradi ndiye anayegundua kibanda cha 1,200,000 kimejengwa kwa 20,000,000 ilhali Serikali ipo kuanzia ngazi ya kitongoji, Kijiji kuja kwenye kata, wilaya na mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata kigugumizi sana. Kama kweli katiba yetu tulivyoitengeneza tungeisimamia vizuri kazi ingekuwa ndogo sana. Haya mambo yanayokuja kugundulika na viongozi wa kitaifa wakija katika maeneo yetu si kama viongozi waliopo kule hawajayasema. Shida yetu iko moja, hata sisi wanasiasa, tuposema au tunaposhauri watu wanaona wanasiema wanasiasa acha waongee na hivyo hakuna utekelezaji wake. Kwa hiyo mimi niiombe Serikali kupitia Bunge hili kwa sababu Bunge limeumbwa na wanasiasa na Mheshimiwa Rais ni mwanasiasa. Kwa wale ambao wanaoona siasa haiwezi kufanya kazi au kushauri basi wakatafute kazi nyingine ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wametuleta huku kuja kuwatetea, wametuleta huku kuja kuwasemea. Leo tukienda kule zahanati ya pale kijiji mwananchi mwenyewe anakwambia mifuko ya cement ilikuwa inaondoka hapa halafu watu wanasiema wanasiasa wanapiga kelele. Kwa hiyo mimi niombe, sisi wanasiasa ni kweli tuna maneno mengi lakini kwenye ubadhilifu lazima tuwe wakali; na ndiyo maana nimemponegeza

Mheshimiwa Spika kwa kuongeza muda wa kujadili ili Wabunge wote waseme nini kilichopo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwenye Bunge la Bajeti nilisema hapa, kwamba tumekuwa na tatizo moja; fedha za Serikali zinapokuja kwenye miradi vitu vinapanda bei lakini chanzo cha kupandisha bei hatukioni. Juzi mmepeleka bilioni 160 kwaajili ya kujenga madarasa 8,000, cement ilikuwa 20,000 kwenye mikao ya mbali lakini baada ya kufika zile fedha siku mbili kabla cement imefika 24,000 mpaka 25,000 katika baadhi ya maeneo. Tatizo ni nini? pochi ya mama imetema. Sasa kama pochi ya mama anahangaika kutafuta fedha halafu na sisi Serikali tunajua hakuna kitu kilichosababisha kupandisha bei na tumekaa kimya, hakuna hata Waziri wa Viwanda na Biashara kwenda kubainisha na kutoa taarifa kama uhaba wa cement. Mimi niiombe Serikali kwenye haya tuwe serious.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Kamati ya PAC; tumejadili sana. Ukija kuiangalia ripoti ya CAG imebainisha sana, na sisi kama Bunge tumeiamini taasisi yetu ya CAG Kwenda kutuangalizia. Inapotuletea hapa inatuonesha kabisa kwamba sehemu fulani kuna mianya. Sisi tusipochukua hatua tunaivunja moyo taasisi ambayo sisi tuliiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nishauri jambo moja. Si kama hawa watu hatuwahoji. Tumekaa hapa tangu mwezi wa 10, tumeita mashirika mbalimbali na tumewahoji ni aibu sana. Kwa kweli ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, kama kanuni haziruhusu hebu tuone haya mashirika yakiitwa kwenye

kamati ambayo ni Bunge dogo ambalo limeundwa na Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Bunge zima ameyagawa mabunge madogomadogo ili kusimamia shughuli za Bunge. Hebu sasa kama tunaweza kurusha *live humu ndani hebu na kwenye kamati tuwe tunarusha live waone wataalamu tuliowapeleka kule.* Unakuta kabisa mwanasheria mbobevu, msomi darasa la saba anamuuliza swalii la kitoto anashindwa kujibu. Sasa wakipigwa mara tatu mpaka nne kwa mikataba *fake ambayo inatuingizia ghamama wananchi.* Wanalipa kodi kwa shida halafu fedha zinakwenda kupotea kirahisirahisi halafu mtu anajibu kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naliomba Bunge hili kama kanuni hazipo, kamati zote wanapoitwa, hasa hizi zinazosimamia fedha za umma, CAG akionyesha mianya, basi na vyombo vya habari viwe vinaingia ili virushe moja kwa moja ili wananchi waone kama tulihoji na wao wamejichanganya vipi. Hii itaongeza ufanisi mzuri katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hapa Wabunge wengi wamezungumza kuhusu Kampuni ya KADCO. Ukija kuangalia sinema inayochewa kule na KADCO ni aibu kubwa. Serikali imenunua hisa halafu bado ikajipangisha yenyewe. Imetengeneza mkataba ambako inamiliki asilimia 100 halafu yenyewe tena inaanza tena kujipangisha. Sasa nashindwa kuelewa kama mimi nina nyumba ninamiliki asilimia 100 halafu tena naanza kujilipa kodi, inaingia akilini kweli. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati ililiona hilo, tumewaita KADCO wanachokisema pale yaani kama watu vile wanaona tu hili acha goma liende kwa sababu halina mwenyewe. Sasa mimi niwaambie wenyewe ndio

sisi kwa niaba ya wananchi. Kama tusiposema, tusipotetea siku ya mwisho tutakuja kuhukumiwa. Jumba hili limepewa heshima kwa niaba ya wananchi milioni 60; na Tabora tumekuwa wa tatu tunaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo milioni 61 wametuamini sisi mia tatu, mia mbili na tisini na kidogo kwenda kuwatetea tunapokuja humu tunaleta maigizo, ngonjera, kuona kama hatuoni kumbe tunaona tutakuja kupata adhabu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe Bunge hili litoe maelekezo. KADCO tumependekeza kwenye kamati kwamba irudi chini ya usimamizi wa viwanja vya ndege. Lirudi kwenye usimamizi wa viwanja vya ndege kwa sababu Serikali ndiyo inamiliki hisa asilimia 100. Kama tunamiliki asilimia 100 na TAA iko chini ya Serikali kwa hiyo huyu akija haina tija tutakuwa tumemwongeza mtoto mwingine hata kama alikuwa wa kambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia KADCO hii tunayoizungumza yaani iliweka mkataba wake ambao unaisha tarehe 16 yaani ilisema hivi, asitokee mtu yoyote hate yenyewe Serikali isijenge uwanja wa ndege wowote zaidi ya kilometra 240 kila upande kutoka KIA. Hii maana yake ni kwamba Arusha wasijenge uwanja wa ndege na watu wa Manyara wasijenge uwanja wa ndege. Mimi niombe Serikali kupitia hili irudishe KADCO iwe chini ya usimamizi wa TAA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante nakushukuru sana. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante nilimwita Mheshimiwa Tunza Issa Malapo. Wakati huo Mheshimiwa Engineer

Mwanaisha Ulenge pamoja na Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo ajiandae.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu. Naunga mkono hoja za kamati zote tatu ambazo zimewasilishwa na wenyeviti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kuchangia; mengi wenzangu wameyasema. Serikali kama ni ya kusikia itasikia lakini kama itafanya kama ilivyozoea miaka yote kwamba tunasema mwisho hatimaye yanayotendewa kazi ni machache basi wataendelea na utaratibu wao kwa sababu labda wanaona unafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti za CAG pesa zinapigwa kwelikweli, yaani watu wanatumia pesa kinyume cha utaratibu tena bila woga. Mimi nimejipa muda kidogo nikasoma. Ukiangalia ile ripoti ya Hesabu za Serikali za Mitaa, nakupa tu mfano wa maeneo manne halafu uone ni pesa kiasi gani ambazo zimeliwa na wajanja wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza CAG ile ripoti ya Serikali za Mitaa anasema matumizi yasiyo na manufaa, yaani kwamba yametumika tu, ukiuliza yamefanya nini hakuna manufaa yoyote ambayo yanaonekana kwa wananchi, milioni 664 na point, ukurasa wa 275, kasome utakuta kaeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine malipo ya bidhaa na huduma zisizopokelewa. Watu wameandika tutatoa huduma hii, tutaleta vifaa hivi lakini havikupokelewa, shilingi ngapi bilioni 8.44 watu wamekula

na mambo yako kimya. Malipo yaliyofanywa bila kudai risiti za *electronic*; tunaambiwa ukiuza toa risiti, ukinunua toa risiti; mimi mwananchi wa kawaida tu nikienda kwenye kituo cha mafuta, nkinunua chochote nadai. Lakini Serikali hiyo inayositisiza wanafanya manunuzi risiti hakuna, shilingi ngapi; bilioni 6.07. Hapa sizungumzii namba tu nazungumzia pesa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo Mheshimiwa Deo Utumishi simuoni Mheshimiwa Jenista mimi nahudumia Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI); kila siku za Mungu tunakuja kufundishwa mifumo, kwamba kuna e-government lakini mpaka leo ripoti ya CAG siyo maneno yangu mimi leo sisemi ya kwangu. CAG anasema hivi mpaka mwaka unaoishia Juni kuna wafanyakazi wamelipwa ambao hawako kazini. Mifumo ipo lakini waliostaifu wamelipwa milioni 343. Mifumo ipo inajua Tunza unastaifu lini lakini unalipwa. Watoro kazini wamelipwa milioni 81 mifumo ipo Mheshimiwa Deo. Waliofariki wamelipwa milioni 63 mifumo ipo, wengineo, yaani ambao hawaeleweki tu. Hawa ambao walistaifu, watoro, ambao hawako kazini ni wengineo, sasa sijui CAG alikuwa na maana gani; maana hawa walikuwa wanarandaranda, tu wamelipwa milioni 68, na mifumo ipo na kitengo cha mifumo kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahudumia Utawala na Serikali za Mitaa ambayo ndiyo kamati yangu. Tumekwenda kuangalia mifumo, wataalamu wa mifumo wapo kwa nini haya mambo yanatokea? Maana watu wanapiga tu, huku tunasifia mama anaupiga mwingi anapita kutafuta hela huku watu wanakula na siku zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Leo tunaambiwa Kariakoo ilipoungua moto na nyaraka zote za mapato na matumizi zimeungua, yaani hazijulikani. Shilingi ngapi sasa hizo tunazungumzia? tunazungumzia bilioni 3.562; ni hela nyingi. Tupo tuna mifumo na kuna watu wanalipwa lakini tunaambiwa Kariakoo ilipoungua moto na mambo yote yameungua. Kwakweli kama taifa hatupo serious. Kwa sababu, sasa hivi wewe ukiwa na simu yako ikaibiwa unaweza ku-recover data zako; sikwambii kitu ambacho kinaingiza mapato mengi hivi kwa nchi. Unaambiwa soko la Kariakoo ilipoungua moto basi kila kitu kimeungua. Haya si maneno yangu ni maneno ya CAG, someni ripoti mtaona. Wameshindwa kuleta udhibitisho hizi hela ziko wapi, hakuna, vimeungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na MSD. Watu wamechangia MSD mimi nikasema ngoja kwanza nikasome.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Naibu Waziri Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Deo Ndejembii.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpatia taarifa Mheshimiwa Tunza Malapo ambaye kweli Mheshimiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, ambayo inatusimamia sisi

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimtoe mashaka yeye na wewe Mwenyekiti na Bunge lako. Hiyo taarifa baada ya kuwa imetoka Serikali hii ya Awamu ya Sita, kwa kuwa ni Serikali makini sana, imehakikisha mfumo wa HCMIS, umetengenezwa kupitia Wakala wa Serikali Mtando (e-GA), na tayari mfumo huo umeanza kutumika Mei, mwaka jana. Hivi sasa kuna kitu kinaitwa *auto-termination*. Mtu akishafika umri wa miaka 60 automatically anatolewa nje ya mfumo. Wakati CAG anafanya ukaguzi wake mfumo huu ulikuwa bado haujaanza kufanya kazi; lakini kwa sasa mtu yoyote anayetoka nje ya utumishi wa umma tayari kuna *auto-termination*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii Mheshimiwa Tunza, iko makini sana chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, na yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais ametuelekeza kuhakikisha tunakwenda kwenye mifumo zaidi na Ofisi yake hii ya Utumishi, nawe ni shuhuda tumekuonesha hata huu mfumo wa HMIS namna unavyofanya kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Tunza Malapo, unapokea taarifa?

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa yaani ipo *half half*. Upande naweza kuipokea na upande siipokei. Siipokei kwa maana ipi? Hawa wanakuwa *wana-exit meeting*, yaani haya yote wangeelezana huko CAG asingeendelea kuyaleta.

Yaliwashinda wapi kumweleza? Kwa hiyo, hapa ndiyo maana nikasema, leo siongea maneno yangu, naongea kutoka kwenye ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hizi ni fedha za wananchi walipa kodi, kwa hiyo, ndiyo maana nasema, kwa upande mwingine kama mmeutengeneza mfumo, niwapongeze. Sina roho mbaya, nawapongeza mfanye vizuri, haya mambo yasijitokeze, kwa sababu hizi fedha zingeweza kusaidia mambo mengine. Hiyo ndiyo hoja yangu ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na MSD. Nimesoma ripoti ya CAG kuhusu MSD. Wenzangu wameongea vizuri tu. Sasa (*MSD - Medical Stores Department*), yaani Bohari Kuu ya Dawa Tanzania, maana yake Bohari, yaani ukisema tu neno bohari, ni kama godown, sehemu ambayo watu wanahifadhi au vitu vinahifadhiwa. Tunategemea nini? Tunategemea tukute wataalamu wa kumbukumbu, wataalamu wa kuhifadhi vitu. Kinachoingia mwanzo ndiyo inabidi kitoke mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ripoti ya CAG jambo la ajabu kabisa anasema hivi, halmashauri zinapelekewa dawa ambazo zimekaribia kwisha muda wake. Kwa nini zinapelekewa hivyo? Kwa sababu watu wa MSD hawana utaratibu mzuri wa kutoa dawa. Labda yeye ananunua huko anaponunua kwa wazalishaji, leo hii tunaongelea Novemba, dawa nyingine ananunua Januari, anaacha kutoa hii ya Novemba iende kwenye halmashauri, anaenda kutoa ya Januari. Kitu kama hicho ninyi mnaamini? Binafsi siamini. Ninachoona, kuna madili yanapigwa. Labda wanaenda kununua dawa huko za

bei nafuu ambazo zimekaribia ku-expire halafu wanafanya dampo halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakupa mifano michache, leo mimi nina ripoti tu ya CAG hapa na namba na kila kitu. Dawa zinazohitaji kuteketezwa mwaka huu ulioshia Juni, Shilingi bilioni 3.5. Bilioni! Nikaenda kusoma sasa, ni halmashauri gani hizo zinazoenda kuteketeza dawa? Katika hizo halmashauri 46, halmashauri nne zinatoka Mkoa wa Mtwara. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi dawa za Shilingi billion 188. Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Shilingi milioni 97, Hamashauri ya Mji wa Newala Shilingi milioni 119, Hamashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Shilingi milioni 76. Hizi ni fedha. Dawa zenyе thamani ya fedha hizi zinaenda kuteketezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaijiliza, hivi kweli Wamakonde wenzangu wanavyoumwa, wanakwenda hospitali wanaambiwa dawa hakuna, leo unasikia dawa za fedha zenyе thamani hiyo zinakwenda kuteketezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nia ya dhati kabisa, tuongeze azimio lingine kwenye maazio ya LAAC, tuseme hivi, hawa MSD wasipeleke dawa halmashauri ambayo labda bado miezi sita ku-expire, wapeleke dawa ambazo zina mwaka, zina miezi 24 kulingana na *shelf life* ya dawa. Wanachofanya MSD wakishaona hawajafanya utaratibu mzuri, dawa zinakaribia ku-expire ili lile bomu lisiwalipukie wao, wanachukua mzigo wanapeleka halmashauri. Kwa hiyo, kule wanafanya dampo. Sasa halmashauri tuongeze azimio. Halmashauri zisipokee dawa ambazo zimekaribia ku-expire, waziache hapo hapo bohari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mpaka moyo unauma. Unateketeza dawa za Shilingi bilioni saba! Mwaka 2018/2019 wameteketeza dawa za shilingi bilioni 7.3, mwaka 2019/2020 dawa za shilingi bilioni 1.5, hapo ilipungua, tunashukuru. Sasa maajabu na kweli mwaka 2020/2021 wanaenda kutekeza dawa za shilingi bilioni 3.5. *This is not fair.* Siyo sawa! Kwa hiyo, watu wa Bohari Kuu tunaamini ni wataalamu, kama ni wataalamu, wafanye mambo kitaalamu, hizi ni fedha za walipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaumwa, wewe mwenyewe ni shahidi, ukiwa kama Mbunge, hivi umewahi kuwachangia watu matibabu mara ngapi? Halafu leo uambiwe dawa za fedha zote hizi zinateketezwa. Huu ni uzembe wa hali gani? Tuweke azimio kuhusu MSD. Unajua watu wanatufanya sisi kama hatujielewi, lakini sisi tunajielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwenye Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inafanya mambo, kuna mengine nimejipa muda nimesoma. Kulingana na sheria yao, wao wanatakiwa wa-support wanafunzi wanaosoma shahada, lakini kuna maagizo yanatoka Wizarani. Wizara ya Elimu walipieni wanaosoma Diploma, hiyo ndiyo ripoti ya CAG inavyosema. Sasa hayo ni matatizo, lakini CAG pia anakwenda mbele anasema, kuna wanafunzi karibia 500 wana-drop kwa sababu ya kukosa ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mwanachuo kasoma mwaka wa kwanza, mwaka wa pili anakosa ada, ana-drop. Kwa hiyo, tunaposema kwamba shule za msingi na sekondari wana-drop na Vyuo wana-drop. Wizara ya Elimu inashindwa kusimamia Bodi ya Mikopo. Wamewaacha pale wakati wajibu wa kuwasimamai Bodi

3 NOVEMBA, 2022

ya Mikopo ni wa kwao, wasikwepe jukumu, wawasimamie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nilimwita Engineer Mwanaisha Ulenge, na wakati huo Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, anajiaandaa.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika mjadala huu unaoendelea. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kunisimamisha mahali hapa muda na wakati kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kuchangia katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali katika kipengele cha 9.2 cha Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba. Kwa mujibu wa CAG amesema kwamba Taasisi 16 zilinunua bidhaa na huduma zenyet thamani ya shilingi bilioni 77.62 bila kutumia mfumo wa TANePS

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa

mwaka 2016 imezitaka taasisi za Serikali zinazofanya manunuzi ya Umma kutumia mfumo huo wa TANePS. Pia Waraka Na. 4 wa Wizara ya Fedha umezitaka taasisi hizo kuanza haraka kufanya manunuzi ya Umma kuanzia tarehe 01 Januari, 2020. Kwa maana mpaka leo ni miaka miwili na ushei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhakika wa taarifa zilizopo ni kwamba mfumo wenyewe wa TANePS ni shida tupu. Ukiangalia maelezo ya CAG aliyoyatoa ukurasa wa 141 akielezea umuhimu wa mfumo wa TANePS amesema kwamba kushindwa kutumia mfumo wa TANePS katika manunuzi kunakwamisha jitihada za Serikali katika kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa manunuzi na kuboresha uwazi katika manunuzi ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mfumo huu bado una changamoto kubwa na kwa kiasi kikubwa hauleti uwazi uliokusudiwa, wala ufanisi uliotarajiwa. Nasema hivi kwa sababu gani? Katika mfumo huo wa TANePS kwanza mfumo wenyewe jinsi ambavyo umenunuliwa kutoka huko uliponunuliwa ni changamoto kubwa, ni aibu tupu kusema kwamba unanunua mfumo ambao haukupi *full access* ya kuutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *evaluation report*, nimefanya tathmini ya *tender* na mfumo huu lengo lake ilikuwa ni kufanya tathmini ya zabuni na kufanya usimamizi wa mradi, maana yake *contract administration* inafanyika ndani ya mfumo. Malipo yote unayowalipa Wazabuni uyanafanya ndani ya mfumo. Kadri unapolipa *certificate* namba moja, hivyo hivyo inapungua mpaka mradi wote unakamilika. Cha ajabu, mfumo huu bu hauipi PPRA wala taasisi inayofanya manunuzi ya Umma *full access* ya mfumo huu. Maana

3 NOVEMBA, 2022

yake mfumo huu so far ni kimeo na kama umenunuliwa, tumenunuliwa na tumezigwa. Haiwezekani ununue mfumo ambao haukupi full access (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Taarifa.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge kwamba mfumo huo ambao anauzungumza, TANePS ni kweli ulikuwa na changamoto lakini Serikali imeamua kujenga mfumo mpya unaoitwa NEST na upo Iringa na unajengwa na wazalendo kutokana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mfumo tulionao sasa utapunguza għarama na utakuwa ni wa uwazi na utakuwa unakamilisha zabuni zote kwa uhakika na kwa muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyeki, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge, unapokea taarifa?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa taarifa hiyo, lakini naomba kama Serikali tusirudie makosa hayo kila kukicha. Kwa nini

tununue mfumo kwa fedha nyingi halafu baadaye tuje tutafute mfumo mwingine kwa ndani, zile pesa *value for money* yake tunaisemaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vizuri umetoa taarifa hiyo kaka yangu Mheshimiwa Naibu Waziri Chande, nimeipokea vizuri kabisa, lakini je, tumefanya tathmini ya kina ya kuangalia ni hasara kiasi gani tumeingia? Mfumo unaokuja mtuhakikishe kwamba utakwenda kutatua changamoto zifuatazo: Mfumo huu wa TANePS kwanza kabisa ukimaliza *evaluation report* ulikuwa hautoi *full detailed evaluation report*; ulikuwa unatoa taarifa ambayo inatoka kama mtindo wa excel. Wakati tulipokuwa tukifanya manunuzi na zile zabuni, tulikuwa tunapata taarifa kamili (*full detail*) ya mchakato mzima wa zabuni, lakini mfumo huu wa TANePS umekuwa haufanyi hivyo. Hata baada ya hapo, unapoingia tena ukitaka kufanya mwendelezo wa mradi kwa maana ya usimamizi, haukupi *access* kwa maana ya mpaka ulipe tena fedha. Kwa nini tumeingia kwenye mifumo ya aina hii? Ina maana kweli hatuna weledi wa kutosha wa kujua mifumo inakuaje? Kwa nini tupewe mifumo ambayo haitupi *full access*? Kwa nini huwezi ku-edit *report* baada ya kuingiza katika TANePS? Hii siyo sawa, tunafanya makosa yanayojirudia kila siku. Ina maana ndiyo Tanzania kweli ni kichwa cha wenda wazimu? Kwa nini tuje na mifumo ya aina hii? Tumesema lengo ni kupata ufanisi na uwazi lakini TANePS hautoi ufanisi na uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa hatua ambazo mmezichukua. Tunawapongeza sana na hili, lakini ukweli lazima tuuseme kwamba kuna hasara tumeingia ili jambo hili tulichukulie very serious, manunuzi ya Umma ni suala kubwa kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichangie sura ya tisa kwa maana ya ukurasa wa 139 unaozungumzia hasara ya Shilingi bilioni 68.73 zimepatikana kwa Serikali kulipa riba kwa wakandarasi. Naomba nisirudie sana, kaka yangu Mheshimiwa Ndulane amezungumza vizuri, amekuwa kwenye utendaji huko TANROADS, ameelezea vizuri kabisa jinsi malipo yanavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba CAG ameonesha kidole kwa mtu ambaye siyo stahiki. Kama kweli tunatafuta *solution*, kama kweli tunataka kuondoa changamoto hizi, CAG anyooshe kidole kwa mtu anayestahili. Kumbuka TANROADS kama ndiyo chanzo cha riba hizi au upotevu huu, nafikiri kuna shida, sielewi labda utendaji wa CAG ukoje? Kwa sababu namwini CAG katika uzoefu wake wa usimamiaji wa miradi, lakini anaponyoosha kidole kwa mtu asiyestahili sifikiri kama ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndulane amezungumza vizuri sana, kule Wizara ya Fedha na Mipango unapeleka *certificate* ya malipo, watu 10 wote wale ni wa nini? Halafu hawaendi site, wanakaa nazo tu ofisini. *Certificate* inakutaka uende site ukafanya measurement ya kazi iliyofanyika. Mnakaazo kule siku 10 nzima Wizara ya Fedha na Mipango, zinafanya nini? (Makofii)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa wapi? Mheshimiwa Mtemvu.

3 NOVEMBA, 2022

TAARIFA

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Engineer Mwanaisha ya kwamba CAG, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anachokifanya, akienda kwa *implementer* wa mradi anamhoji juu ya kutokamilika kwa mradi husika bila kuangalia alitakiwa kupokea hiyo hela kwa nani? Pia ana jukumu la kwenda kwenye Wizara ya Fedha chini ya fedha ambazo zinatokea kwenye GoT - Government of Tanzania; na kule pia mtoaji fedha anahojiwa vilevile, mbona wewe una jukumu la kutoa fedha kwenye taasisi kadhaa na hujazitoa kwa wakati? Kwa hiyo, nilitaka kumwambia, hiyo ndiyo kazi ya CAG, ameifanya sahihi kwa yule anaye-*implement* mradi na pia kwa mtoaji wa fedha. Ahsante. (Makofij)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge, unapokea taarifa?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa elimu, lakini nimkumbushe kaka yangu Mheshimiwa Issa Mtemvu, kwamba yeye ni mhasibu kweli, lakini hapa hasimami kwa CAG. Hapa tunatafuta *solution*, kwa nini miradi inaleta riba nyingi? Kwa hiyo, sisi kama tunataka kutoa maazimio na kuishauri Serikali, inabidi kuangalia mambo *in wide perspective*, hatusimami upande wa CAG. Kama Wizara ya Fedha haijapeleka pesa kwa wakati, miradi yote ya DEVO ni kimeo nchini humu. Mkandarasi yejote akipata mradi wa DEVO, siku zote sisi tunajua atapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miradi ya *mantainance* pekee ambayo inatokana na fedha za *fuel levy* ndiyo

yenye uhakika wa malipo. Miradi ya development hailipwi kwa wakati yote. Chanzo cha fedha cha miradi ya DEVO ni Serikali, fedha zinatoka Hazina.kwa hiyo, ni lazima tuyaseme haya ili tuije na mapendekezo sahihi na maelekezo sahihi kwa Serikali. Sasa hapa Mheshimiwa Mtemvu, uzoefu wako kwenye auditing na uhasibu lakini wewe sio CAG hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Shilingi bilioni 68.73 kwa uhakika ni kwamba ni riba peke yake, lakini hasara ni kubwa zaidi ya hii. Kwa maana gani? Hapa bado hatujaingiza fedha. Kama una Mwandisi Mshauri kwa mfano, anasimamia mradi huu, unapochelewa kumlipa mkandarasi, maana yake unaongeza na muda wa usimamizi wa mradi. Kwa hiyo, na mwandishi mshauri naye anaongeza malipo yake. Kwa hiyo, cost and time over run nazo ni thamani kubwa katika mradi. Achia wafanyakazi ambao ni client ambao wana supervised miradi kila siku na kufuatilia kila siku kule site.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni fedha nyingi sana kiukweli za Watanzania walalahoi zinapotea. Tangu nimekaa kwenye Serikali zaidi ya miaka kumi kabla ya kuja huku, miradi yote ya DEVO pesa haziji kwa wakati, haziji at all, shida ni nini?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ulenge, kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe mnapochangia, basi mwasiliane na Kiti, nikikupa ishara kwamba muda tayari, iwe rahisi zaidi kuweza kumwita mwingine.

Nilimwita Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, wakati huo Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza wanajiandaa.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. Naomba nichangie kwenye taarifa zetu mbili hasa hii taarifa ya LAAC. Nikiwa sehemu ya Madiwani kule kule ninapotoka, nianze na eneo moja la Mwenendo wa Bajeti na Kiwango cha Utiegemezi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, nitambue ukweli kwamba halmashauri nyingi nchini kwa kweli zinajitahidi sana kukusanya mapato kwa kuzingatia makadirio ambayo imejivekea.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia huu mwaka wa fedha ambao CAG ameufanyia audit, 2020/2021, Halmashauri zilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 822.38 na zimekusanya bilioni 799.42, sawa na asilimia 94. Kwa hiyo, zinafanya vizuri na kwa nini? Uki-bench mark na Serikali Kuu TRA ilipanga kukusanya trilioni 20.326 ikakusanya trilioni 17.599 sawa na asilimia 86.6. Kwa hivyo, tukilinganisha kiufanisi na kitakwimu halmashauri zetu zilifanya vizuri kuliko Serikali Kuu. Hili ni

vizuri tukaliona kwa sababu huwa tunaona tu ule upande wa udhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukweli ni kwamba, changamoto za halmashauri zetu sio uwezo wa kukusanya, changamoto kubwa ni ufinyu wa vyanzo vya mapato, hii ndio changamoto kubwa ambayo inatukabili. Ndio maana katika shilingi trilioni zaidi ya 34 kwenye bajeti ambayo tunaijadili, halmashauri zote ukikusanya kwa pamoja hata trilioni moja haziwezi kukusanya, kwa hiyo, ni changamoto kubwa. Tunategemea tu leseni za biashara, service levy, leseni za vileo, vibali vya ujenzi na vibali vya sherehe kwa wale wanaokaa kwenye manispaa na mijini, ukienda vijijini huko wanategemea ushuru wa mazao na kadhalika. Sasa hivi vyanzo ni vidogo ni vifinyu, haviwezi kuifanya halmashauri itekeleze jukumu lake sawasawa kama ambavyo imewekwa katika Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chanzo kingine tunafahamu ruzuku, lakini CAG anasema nini kuhusu ruzuku ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri? Mambo matatu; moja kuna halmashauri kama 19 ambazo zenyewe zimepokea ruzuku zaidi ya bajeti yao, kiwango cha shilingi 47.19 na ipo kwenye taarifa ya Kamati yetu. Pili, kuna halmashauri 163 zenyewe zimepokea ruzuku chini ya bajeti yao, yaani imepungua kwa shilingi bilioni 312, lakini tunazo halmashauri 144 ambazo zenyewe hazikupokea kabisa ruzuku ya matumizi ya kawaida. Hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ruzuku kimsingi ni hisani, hakuna formula inayotoka Hazina inayotumika kugawa ruzuku, inategemea pengine bidii ya Mkurugenzi mwenyewe, inategemea Meya anaongea vipi na

Hazina, ndio maelezo pekee, lakini kwa nini tuwe na variable ya ugawaji wa ruzuku? Hii ni hisani. Je, ni sahihi sisi kama Bunge hili tuendelee kutegemea hisani ya ruzuku? Au tuweke utaratibu mzuri ambao kuna formula inaeleweka na nchi nyingi zimeshaweka, nchi nyingi zimeweka vizuri kabisa kwamba, kila jimbo linapata shilingi ngapi kwa utaratibu upi? Wamefanya hiyo South Africa, wamefanya hivyo Nigeria, wamefanya hivyo juzi wenzetu Kenya kupitia Sera yao ya Devolution. Kwa hiyo nataka niiweke hiyo *observation* ambayo nadhani ni muhimu sana sisi kama Bunge tukaelewa na tukaizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipayendekeze kutatua hili tatizo kwa sababu tuko kwenye kikao hiki cha hili Bunge hili na hapa hatuishauri Serikali, tunataka kuweka maazimio ili tukasimamie utekelezaji. Naomba nipayendekeze mambo matatu na naomba Mwenyekiti wa Kamati kama itampendeza achukue haya mapendekezo, kama ninavyosoma kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Halmashauri zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa fedha, mapato kwa ajili ya uendeshaji na miradi ya maendeleo;

Na kwa kuwa ruzuku kutoka Serikali Kuu imekuwa haiendani na bajeti za halmashauri na mara nyingi haipatikani kwa muda muafaka.

Na kwa kuwa vyanzo vingi vya mapato vya kodi viro kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii niifafanue, vyanzo vingi vya mapato katika halmashauri vilienda TRA. Tulikuwa tunategemea sana *property tax* ilienda na juzijuzi tumenyang'anywa ushuru wa mabango na

wenyewe hatukusanyi tena na haieleweki sasa hivi anakusanya TANROADS au TRA, lakini halmashauri zimenyang'anywa kukusanya hiyo.

Na kwa kuwa kwa hali hii imekuwa ikiathiri uwezo wa halmashauri katika kutekeleza wajibu wake wa kisheria na Kikatiba;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kuwa:-

- (1) Bunge liweke utaratibu wa kisheria na kikanuni wa kugawana mapato ili kwamba, sehemu ya mapato ya kodi yarudi katika halmashauri. Kama Serikali Kuu tumekubali kwamba, TRA ndio *Professional Tax Collectors*, lakini TRA hawezi kufanya makusanyo ya *property tax* bila kushirikisha halmashauri, hivyo tukubaliane kwamba, sehemu ya kodi hiyo irudi halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika halmashauri ili utaratibu wa kupata hizi fedha uwe ni wa haki, ni wa kisheria kuliko kusubiri hisani ya Hazina.
- (2) Kwa kuanzia katika mwaka wa fedha ujao, asilimia 40 ya mapato ya kodi ya majengo na ushuru wa mabango irudi kwenye halmashauri husika; na
- (3) Serikali iweke utaratibu na vigezo vya wazi vinavyotumika katika kugawa ruzuku kwa halmashauri ambazo hazina vyanzo vya uhakika vya mapato kwa ajili ya uendeshaji na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mapendekezo matatu ambayo nayatoa katika kuboresha jambo hili ili halmashauri zetu ziwe na uhakika wa mapato na kwamba, utolewaji wa ruzuku ufanyike kwa mujibu wa sheria kuliko ilivyo sasa ambapo tunaona kabisa halmashauri hii inapata na nyingine haipati. Hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo limeibuka kwenye Taarifa ya CAG na bahati mbaya sijaliona kwenye Kamati zetu ni suala la mfumo wa udhibiti wa ndani. Usimamizi wa vihatarishi na mfumo wa utawala bora. CAG katika ripoti yake ameibua jambo kubwa sana, ukurasa wa 8-13 anasema, changamoto za mfumo wa uendeshaji wa Serikali za Mitaa amehoji kile ambacho wanaita mwingiliano kati ya Madiwani na mamlaka za utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amebainisha kwamba, Madiwani wamekuwa wakishiriki katika shughuli za kiutendaji za mamlaka ikiwemo kwa mfano Wenyeviti na mameya kusaini mikataba na ameona hili jambo sio zuri. Sasa hili tumrejeshe CAG kwenye Ibara ya 145 na Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumrejeshe CAG kwenye sera ya ugatuaji *decentralization by devolution* ambayo tuliipitisha mwaka 1996. Tumrejeshe pia kwenye Sheria mbili ambazo zinaongoza Local Government Authority.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Serikali kamili na zipo chini ya Madiwani. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu likaeleweka na Waheshimiwa Wabunge hapa sisi ni Madiwani na zile lawama zote ambazo tunazitupa halmashauri ni za kwetu. Sisi ndio wasimamizi, sio tu wasimamizi, sisi ni waendeshaji wa

halmashauri tofauti na Serikali hapa, tunaweza tukalaumu Serikali Kuu hapa kwa sababu sisi ni washauri tu, lakini sisi ndio waendeshaji na wasimamizi wa halmashauri kisheria. Sasa kiuhalisa hiyo tutajadili siku nyingine kwamba, kweli sisi tuna nafasi kiasi gani? Hivi kati ya DC na Mkurugenzi, Mkurugenzi akiagizwa akipewa maelekezo na DC anafuata ya nani? Hili tulijadili siku nyingine, lakini kwa sasa tuseme kwamba, Waheshimiwa Wabunge sisi ni Madiwani zile halmashauri zipo chini yetu na kwa jambo hili CAG sio sahihi. Kwa hiyo, azimio hapa liwe ni kwamba:

“Serikali iongeze kasi katika utekelezaji wa sera ya ugatuaji na kuwajenyea uwezo wa kutosha Madiwani. Na kwamba, irudishe mamlaka ya Madiwani dhidi ya watumishi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi kwa sababu, sasa hivi Madiwani kwa kweli mamlaka dhidi ya watumisi ni madogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa sababu ya muda nilisikia kengele hapo. Hili ni la wananchi wa Ubungo kule.

MWENYEKITI: Nimekuongeza dakika mbili Profesa.

MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ubarikiwe. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, tunao Mradi wa DART Dar-es-Salaam, mradi muhimu na unatusaidia sana na tunaupenda, lakini naomba katika suala la kutwaa maeneo ya wananchi wazingatie sheria ya fidia wala

wasifanye vinginevyo. Zoezi hili liwe la wazi, liwe shirikishi kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna mgogoro pale Ubungo Kisiwani kaya 91 zinataka kuondolewa. Uthamini ulifanyika katika utaratibu ambao haueleweki, wananchi wamelalamika, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 7.8 kwa ajili ya fidia, lakini watu wa DART wameshindwa kusimamia utaratibu mzuri wa kuweka utaratibu pale kwa ajili ya fidia. Mheshimiwa Waziri tumelizungumza hili naomba alifuatilie ili wananchi wale watendewe haki, wapishe mradi, fidia ilipwe kwa mujibu wa sheria. Hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika moja iliyobaki nichukue nafasi hii kuzipongeza sana Kamati zetu mbili kwa kazi kubwa, ripoti zao ni nzuri sana. Tupongeze vilevile halmashauri zetu kwa sababu, kwa mara ya kwanza wamepata hati inayoridhisha asilimia 96. Ukiangalia kwa miaka mitano hiyo record haijawahi kuvunjwa, kwa hiyo, ni jambo jema, halmashauri zetu zinafanya kazi katika mazingira magumu, tuwatie moyo, tuwasimamie wafanye vizuri zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale wanapofanya vizuri tuweze kuwatia moyo, kwa hiyo, hili ni jambo zuri ambalo nadhani kwamba, ni muhimu likazungumzwa. Hii ni sawa na waliopata kwenye upande wa Serikali Kuu, lakini la mwisho, bahati mbaya mapendelekezo mengi hayatekelezwi yale ya CAG na CAG analalamika kwamba, mapendelekezo mengi yamekaa bila kutekelezwa. Azimio moja tupendekeze hapa ni kwamba, pengine kuanzia mwaka ujao wa fedha pale ambapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa au Mamlaka ya Serikali Kuu haijatekeleza angalau asilimia 50 ya

mapendekezo ya CAG, watu hawa waitwe kwenye Kamati yetu ya Haki na Maadili wajieleze na hatua stahiki zichukuliwe ili tuokoe fedha za wananchi wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya malalamiko mengi ambayo tunayatoa hapa CAG ametoa mapendekezo namna ya kuyashughulikia, watu hawatekelezi. Bahati mbaya hawajachukuliwa hatua yoyote *criminal* kwa sababu, CAG *report* sio *criminal document* ni jambo nadhani kwamba, sisi kama Bunge tutake watu hawa waitwe. Kama mtu anaweza akaitwa kwenye Kamati kwa kosa dogo, kama amefuja fedha za wananchi aitwe kwenye Kamati yetu ya Haki na Maadili ili ajieleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Bonaventura Kiswaga.

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi uliyonipatia, lakini nianze kuunga hoja taarifa hizi tatu ambazo zimeletwa na Kamati zetu hapa Bungeni. Sisi tunaamini kwamba, Kamati ya PAC, PIC na LAAC, CAG ndiye jicho letu, maana yake ndiye jicho la Bunge. Kwa hiyo, tunapokuwa humu ndani sasa hivi leo, tunafanya kazi sisi wenyewe kama CAG. Kwa hiyo, tunapoona kuna watu wanateteatetea haya mambo tunajiuliza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana mchangiaji wa mwisho hapa, Profesa Kitila, amesema CAG ameshaleta mapendekezo mengi, lakini hayafanyiwi kazi. Hayafanyiwi kazi kwa sababu, sisi wenyewe humu tena tunawateteatetea hawa ambao wamesemwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge ni kutunga sheria. Tunapotunga sheria miongoni mwetu humu kuna Mawaziri wanakwenda kutunga kanuni ili kuiwezesha sheria kufanya kazi. Wanapokwenda kufanya kazi tumepitisha bajeti hapa ya miradi, wao ndio wanaoandaa *Bill of Quantity*, makadirio ya mradi. Wao ndio wanaoandaa taasisi hiyo, inaandaa mikataba; ikiandaa mikataba inaweka vigezo mbalimbali. (Makofi)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Taasisi ya TANROADS...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumpa Taarifa mchangiaji. Kwa kweli, wanaojaribu kuteteatetea kuhusiana na hii ripoti, nataka nimwongezee tu mchangiaji, yeye atiririke tu asiwe na wasiwasi tutafikia hitimisho na nawaandika hapa wale wanaotetea, tutakuja kumalizana mwishoni. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga unapokea Taarifa?

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na miradi ya bilioni 664 ya ujenzi wa barabara. Bilioni 600 hizi wakandarasi walicheleweshewa kulipwa na kufanya Serikali kuingia

hasara ya jumla ya bilioni 68.7. Huu ni udhaifu wa usimamizi wa mikataba. Kama ambavyo nilisema sisi ndio tunaandaa makadirio, sisi ndio tunaandaa mikataba, halafu tunashindwa kusimamia mikataba, kulipa kwa wakati mkandarasi akiwa amemaliza kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halikubaliki kwenye dunia hii. Hatuwezi kukubaliana na jambo hili. Nchi hii ni tajiri, lakini inataka kufilisiwa na watu ambao kimsingi wanaangalia maslahi yao. Inaingiaje akilini kwamba, tuliweka sheria ya siku 28, tukaweka sheria ya siku 56 ili mkandarasi awe ameshamaliza kulipwa, jumla ni siku themanini na ngapi? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie, tuwafuate mmoja mmoja ambaye amesababisha hasara hizi, kwamba, mkandarasi alipo-raise certificate ilikaa kwake siku ngapi ili tumwone nani ameingiza hasara hizi. Haya yamekuwa ni mazoea, huu ni mradi mmoja tu wa taasisi moja ya TANROADS; miradi mingi ya Serikali yote ina riba, kwa nini tuwe na riba? Kwa nini tuwe na riba wakati kuna wataalam waliobobe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewapa ofisi nzuri, tumewapa magari, tumewapa kila linalowezekana ili wafanye kazi hizi, haiwezekani hata siku moja. Kwa hiyo, Bunge tuangalie ni nani aliyesababisha hasara hizi, awe ni mtoto wa shangazi, awe ni mjomba, awe ni mke wangu, wote wachukuliwe hatua. Haiwezekani nchi hii watu wakatengeneza kichaka cha kupigia kwenye miradi na sisi tupo, haiwezekani. Tumekuja hapa Bungeni kufanya kazi gani? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tulikuwa tunajadili kuleta Muswada hapa wa bima na Wabunge

tunalalamika kwamba, wananchi hawana uwezo wa kuchangia, kumbe fedha ambazo zingeweza kulipa zimekwenda kulipa riba na sisi tupo, haiwezekani! (Makofi)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma, Taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampa taarifa mzungumzaji kwamba, hata hizi riba ambazo zimelipwa bilioni 68 hazikulipwa kwa wakandarasi wazawa, zimelipwa kwa kampuni za nje. Hakuna mkandarasi mzawa anayedai fidia kwenye Serikali, maana yake riba na mimi nikiwemo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiswaga unapokea Taarifa?

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo maana yake nini? Ni kwamba, hawa wataalam wetu walioko ofisini wanakaa wanazungumza na hizi kampuni, tukucheleweshee certificate, tukulipe riba, halafu na mimi uje unipe cha kwangu, ndivyo inavyoonekana. Halafu Serikali imeshindwa kuweka utaratibu wa kisheria wa kuteua bodi, Executive Board, inateua bodi ya ushauri ilimradi iwe na mkono wake na yenyeche au kuna namna gani humo ndani, Serikali watueleze haya maneno haya? Kwa hiyo, Bunge tuchukue hatua kikamilifu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nakwenda kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Imezungumzwa hapa, bahati nzuri Mheshimiwa Songe jana alizungumza kwamba, kuna watu wanapewa mikopo ambao hawana sifa, ni zaidi ya bilioni mbili, ngoja niangalie hapa. Ni zaidi ya bilioni 2.5 hivi, bilioni 2.255, hawana sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wataalam wamebobea wako kule ofisini wanatoa kwa watu ambao hawana vigezo, watoto wa walalahoi wanakosa hela hizi. Nilimsikia Mheshimiwa Spika, jana anasema hawa wataitwa, hivi bado wapo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Elimu alipouona huu uozo akateua Kamati, Kamati ikaenda kukwamishwa maana yake nini? Unajua Sheria haina mbadala na sisi ndiyo watunga Sheria, akikwamishwa Waziri Kamati yake maana yake Serikali imekwamishwa kufanya kazi, hao bado wapo? Waziri, tena Profesa mbona tunataka kuchelewa nchi hii, hao hawana mjadala, hao anzeni kuchukua hatua mara moja. Haiwezekani Serikali inakwamishwa na taasisi ambayo imeiweka yenyewe, halafu Bunge tuko hapa, CAG leo sasa anafanya kazi yake lazima tuamue, haiwezekani! Tuliomba Ubunge ili tuwasaidie wananchi, Hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine mmetupa Kamati ngumu kweli! Kamati ya PAC ya kuangalia wezi, usiku na mchana wezi! tena Kamati hii inamaliza vikao kila siku usiku Saa Mbili, hizi Kamati ni nzito kweli halafu tuache hawa, tumeumia migongo hawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio letu tuchukue hatua iwezekanavyo hawa hawapaswi hata kukawia kama ni

Jumamosi wangeitwa, sijui waitwe lini, sijui kesho asubuhi ili kwanza Kamati iwanyonge, halafu sasa azimio letu nalo Jumamosi tukamalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, PAC ilipendekeza Bodi za Wakurugenzi kwamba zikimaliza muda wake ziendelee, hili nalo siyo sawa kwa sababu inafahamika bodi hii inamaliza muda wake lini, kama inafahamika wale wanaopendekeza majina kwenda kwa mamlaka ya uteuzi wanaweza wakawa wanachelewesha, kwa sababu yupo mtoto wa Shangazi, Mjomba, yupo mate wangu, wanachelewesha hata kama bodi hii haitoi matokeo chanya, Hapana! Wale wanaopendekeza majina kama tutabaini wanachelewesha kupeleka kwa mamlaka ya uteuzi tuchukue hatua. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu, Bodi hizi..... samahani niongeze muda kidogo. (*Makofij*)

MWENYEKITI: Haya dakika moja hitimisha hoja yako.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bodi siyo mahala pakwenda kupumzikia. Kuna utaratibu wa kuchagua watu ambao wanaelekea kustaafu sikatai, lakini kuna wengine ukiwaona wakitoka PAC wengine PIC pale, unaona wamechoka, unaweza kutafakari sijui wanaomba msaada huyo au namna gani! Lakini nataka niwaeleze Bodi hizi ni za kwenda kuweka akili ili Shirika au Taasisi iendelee. Haiwezekani tunao vijana wazuri wa miaka 30 au 45 wanashindwa kuteuliwa kwenye Bodi tunateua watu ambao kimsingi wanapaswa kupumzika, tusifanye hisani kwenye Mashirika yetu na Taasisi zetu tupelekeni akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Boniventura Kiswaga. Nilimuita Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, wakati huo Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu wanajiandaa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo kuhusu taarifa ya Kamati za PAC, PIC na LAAC. Nianze kwa kuunga mkono hoja ya taarifa hizi, nami ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC nashukuru Wajumbe wamechangia, nami naweza kuongeza kidogo kwa sababu tumesikiliza namna gani mnavyounga mkono kazi yetu tulioifanya na inafurahisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kiswaga ameuliza swali bado wapo? Bado wapo kwa sababu nchi hii imelea mfumo wa wizi! Narudia nchi hii imelea mfumo wa wizi, tumelea kizazi sisi wenyewe! Mfumo huu umebadilika sasa umekuwa utamaduni, tumeuchukua kama sehemu ya maisha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo tu ndani ya Halmashauri ya Longido, wengine wanasema mambo ya Serikali Kuu ngoja sisi turudi huku chini, msije mkafikiri kwamba uchafu huu mnaousema Serikali Kuu, kwa sababu ni mahela makubwa, ngoja niwapeleke Longido mjue kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la TANESCO walilipa pesa za fidia kwa Halmashauri ya Longido 341,820,000 na walikuwa wanalipa vijiji ile njia iliyopitisha umeme kutoka

Longido kwenda mpaka kuvuka kwenda Kenya. Pesa hizo, ziliwekwa katika Halmashauri ya Longido. Afisa Masuuli alichukua 251,320,000 akapeleka kwenye akaunti ya Vijiji, alikuwa anapeleka asubuhi pesa zinatolewa baada ya masaa mawili kama zile za *EPA*. Alivyoona afanye nini akachukua milioni 90 akampa Mkuu wa Wilaya ili kumkata ngebe! Yaani Mkuu wa Wilaya anafungwa zipu mdomoni! nafikiri alimuona kwamba ana maneno maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi zilichukuliwa zikapotea na Afisa Masuuli huyo akasema zilikwenda kwenye uchaguzi. CAG alipokwenda kufuatilia Tume ya Uchaguzi ikasema haijui hizo pesa. Pesa hizi zimepotea na hazijawahi kupatikana na hazina kielelezo. Afisa Masuuli huyu yupo kazini! Mkuu wa Wilaya yupo kazini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo mtiririko wa malalamiko ya Waheshimwa Wabunge, kwamba mtu anafanya kitu cha namna hii bado anaendelea kukaa kazini, huu ni mfumo tumeulea unapendeza sana! Je, tutawezaje kuurekebisha? Kama wote tunaheshimiana na tunahurumiana? Tunaona kwamba hakuna sababu ya kusemana, yaani mtu anabeба fedha zote hizo viongozi wapo wanaona, kinachofanyika kwa watu kama hawa wanahamishwa anatoka kwenye Halmashauri moja kwenda nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukagazi wetu kama LAAC tumegundua hilo, wakipewa taarifa kwamba Kamati ya LAAC itakuita kwenye Halmashauri wanamhamisha *the next day*, unapata Mkurugenzi ambaye amekaa kwenye Halmashauri mwezi mmoja atajibu nini, wakati manyanga yalifanywa na Mkurugenzi ambaye alihamishwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba sana, jambo hili tusichukulie mzaha hii nchi inapoteza pesa nyingi na wapigaji kama nilivyosema ni wengi na wanaoshiriki pia. Mimi najiuliza Je, huu mfumo tumeulea unaanza wapi, ukatiririka wapi mpaka kwenye Kijiji? *there is something wrong somewhere!* Naomba niishie hapo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuhusu ukosefu wa Watumishi katika Halmashauri. Halmashauri zetu na hasa zile za pembezoni hazina watumishi kabisa. Majuzi ni kweli tumepitishwa na TAMISEMI katika mfumo wa TAUSI na wameenda mbali wameonesha watakavyoweza kutoa mikopo ile ya asilimia Kumi kwa njia ya kielektroniki. Sasa nikajiuliza hawa wamefanya hapa TAMISEMI je, wapo wataalam huku chini? Hakuna wataalam wa TEHAMA katika Halmashauri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Maendeleo ya Jamii hawawezi hiki kitu, zipo Halmashauri ambazo zina pesa nyingi kama Maafisa Maendeleo wangeweza kusimamia mikopo hii lakini hawana magari, hawana hata pesa. Tuliuliza kwa nini Mkurugenzi hatoi pesa za usimamizi wa mikopo hii? TAMISEMI wakatuambia kwamba wanapanga kwamba kwenye mikopo humohumo kutoke na pesa ya kusimamia mikopo, hatukukubaliana na jambo hilo. Tulisema Mkurugenzi maana yake mikopo hii Waheshimiwa Wabunge haina riba hairudishwi na haina riba. Sasa kama hakuna riba na siamini kwamba huo mfuko uko *too political*. Hata kama ungekuwa wa kisiasa hauna riba? Yule anayekusanya mikopo anatumia nyenzo gani kuweza kufuatilia hiyo mikopo? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ndani ya Halmashauri kuna upungufu mkubwa wa *Engineers* tumesema hapa tena kwenye miradi ile ya *force account*, wasiwasi wangu nafikiria kwamba kule mbele tutakuwa na *crisis* ya miradi hii ambayo inayo pesa kubwa lakani haina msimamizi. Darasa linajengwa leo kesho nyufa! Nani anasimamia? Tumetoa ushauri kwamba kwa sisi ambao ni vijana wa zamani tulimwona Rais Hayati Mwalimu Nyerere wakati ule anahangaika na Walimu ali-introduce kitu kinaitwa *Universal Primary Education* aka-train Walimu kwa misingi aliyooiona yeye. Ni kwa nini Halmashauri, TAMISEMI, VETA na sehemu nyingine msikae kwa pamoja mkatengeneza technician? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana wengi ambao wamemaliza Form Six na Halmashauri inaweza kusomesha watu hawa. Halmashauri kusomesha mtoto VETA akawa *technichian* wa ujenzi ni gharama ndogo sana, ni lazima Serikali mtoke ndani ya box, lazima Serikali iyaone haya, kama tunakosa *Engineers* basi tutengeneze watu hapa ambao watasimamia ujenzi, tutengeneze sisi wenyewe watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zinaweza kabisa kusomesha watoto mafunzo ya TEHAMA vijana wapo, Halmashauri wanaweza kusomesha *Technicians* kama siyo *Engineers* ambao wanaweza kwenda kule vijiji ni wakasimamia ujenzi kwa sababu hii miradi imechukua pesa nyingi lakini haikujengwa imara. Inawezekana baada ya miaka fulani miradi hii yote madarasa yakaanguka, japo wengine wanajitahidi, lakini iliyomingi haitekelezwi kwenye viwango vinavyotakiwa. Kwa hiyo, naomba Serikali, TAMISEMI na Halmashauri tuje na idea ya kusomesha Watoto. Wanao uwezo Halmashauri kama wanapoteza pesa namna hiyo, mtu

anampa Mkuu wa Wilaya anamfunga mdomo kwamba usiseme chukua Ninety Million na wewe uweke hapa halafu ukae kushoto! Kwa nini pesa kama hizo zisiende kusomesha watoto na Halmashauri ikawawekea mikataba fanyaeni hapa miaka mitatu mtusaidie hiki, hiki na hiki halafu baadae uondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo kuhusu kupeleka bajeti kubwa na ndogo katika miradi ya maendeleo katika Halmashauri. Aliongea vizuri Mheshimiwa Kitila lakini wasiwasi wangu ni kwamba, haya mambo ya kupeleka pesa pungufu yanaumiza Halmashauri maskini. Hebu fikiria Halmashauri kama ya Bumbuli ina mapato yasiyozidi Milioni 800 kwa mwaka. Kama Halmashauri inakusanya Milioni Mia Saba au Milioni 800 what do you expect? Hivi hawa wanaweza kuchangia nini hata hiyo 40 percent ya maendeleo, watachangia alafu hamupeleki hela, mnawapelekea 33, 34 percent na ukitazama Halmashauri zote za Tanga huko zimecaa mkao huo, sijui mafikiria nini, sijui mna agenda gani huko, hakuna pesa zinazokwenda kwenye Halmashauri zote Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili mlitazame kwa maana kuna Halmashauri ambazo uwezo wake ni mdogo. Halmashauri ya Bumbuli ilikuwa na Kiwanda kimoja tu cha Chai na sasa hakifanyi kazi miaka mingapi, sijui wanatoza ushuru kwa nani? Zipo nyingine ambazo hata kutoka kwenye Halmashauri kwenda kununua mafuta kama ile ya Momba unatembea karibu Kilometra mia moja na kitu, sasa Mkurugenzi anakwenda kununua mafuta Kilometra mia moja halafu akirudi mafuta yameisha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho CAG anakagua siyo tu mambo ya pesa peke yake, ametuambia kuhusu elimu kwamba kuna drop out kubwa sana kwa watoto ambao wako darasa la....

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Naona muda wake ulikuwa umeisha na kengele ilishapigwa lakini kwa sababu ulisimama Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, ninaoma nikupe fursa ya kutoa taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Conchesta kwamba, pamoja na mchango wake mzuri lakini nimejaribu kutafakari hapa amezungumza moja ya hoja ambayo kwenye taarifa ya CAG haipo, ame-generalize kwamba Wakuu wa Wilaya wanaweza kulambishwa tu hela kadhaa, amezungumzia general *not in a specific case*.

Pili, kwa kufanya hivyo kama Mkuu wa Wilaya hiyo kuna ushahidi kwamba alipewa fedha hizo, kuna mamlaka na hatua za kuchukua na zipo kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, nilitaka kuweka kumbukumbu sahihi kwamba kwa nafasi ya Wakuu wa Wilaya ni nafasi ya Kikatiba na wanaapa viapo vya utii wa utekelezaji wa majukumu yao na wanayo Sheria ya Tawala za Mikoa ambayo inaelekeza majukumu na wajibu wa Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunavyo vyombo pia PCCB na mamlaka nyingine zipo na zimetoa utaratibu kama tuhuma za rushwa au ufujaji wa fedha, Serikali inautaratibu wake. Kwa hiyo, nilitaka kwa kweli pamoja na mchango mzuri, namshukuru sana Mama yangu lakini kuweka sawa isiende rekodi vibaya kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya ambao wanafanya kazi kubwa na nzuri sana kwa nchi hii. Ahsante. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Conchesta unapokea taarifa?

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siipokei hiyo

MWENYEKITI: Hebu ngoja kwanza tuelewane vizuri, keti kwanza. Hoja ya Naibu Waziri anasema umetaja Milioni Tisini on General term na siyo mtu hata hukumtaja jina, sasa kama umezungumzia Wakuu wa Wilaya wanafanya hivyo hiyo lazima ufute kauli, otherwise utuambie uthibitishe. Hoja yako kama ingekuwa specific, hapo sawa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijataja jina la mtu hapa, sijawa specific, lakini jambo hili liko kwenye taarifa ya CAG. Taarifa ya CAG ndiyo alimetuonesha haya siyo mimi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru.

MWENYEKITI: Ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri, bado sijakuruhusu, naomba uketi kwanza. Umemamaliza hoja yako, taarifa unapokea au hupokei.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, aah mimi sijapokea kwa sababu mimi sija-*identify* mtu, nimesema Mkuu wa Wilaya alipewa Ninety Milioni na hii....

MWENYEKITI: Hebu labda tuende kwenye ukurasa ni sehemu ipi, hebu tuende kirahisi zaidi ili kumrahisishia Mheshimiwa Naibu Waziri.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Nitakuletea kwenye briefing maana tunapewa kwenye briefing za CAG, kwa hiyo....

MWENYEKITI: Ngoja, kumrahisishia, amesema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba unaongea ambayo hayapo kwenye ripoti ya CAG, sasa wewe uthibitishe unachokiongea ni cha CAG basi mpitishé kwenye ukurasa ni kazi nyepesi tu.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya kazi na briefing za CAG, kwenye briefing ya CAG aliyotuonesha ipo hii.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, taarifa.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuniona. Nataka nieleze jambo moja ili Mwenyekiti na mtoa hoja aelewe. Taarifa ya CAG

kwa mujibu wa maneno yako ni kwamba kuna Mkuu wa Wilaya aliyetajwa *specific*, huyo ndiye tunaetaka tumsikie hapa akitajwa, lakini kusema kwamba Wakuu wa Wilaya wote wanachukua fedha hilo jambo halipo, kwa bahati mbaya zaidi msemaji hujasema ni nani? Mtaje huyo Mkuu wa Wilaya lakini usije ukasema kwamba Wakuu wa Wilaya wanachua fedha, hilo jambo halipo.

MWENYEKITI: Hebu tuelewane vizuri, ngoja kwanza tuelewane vizuri, tunachangia taarifa ya CAG, kwa hiyo ukisimama hapa ndiyo *reference* yetu na ndipo unajenga hoja, kwamba kuna hili na hili. Hoja iliyopo ingekuwa *general* ilitakiwa ufute, lakini kwa sababu umesema ni *specific*, kwamba kuna mkuu wa wilaya alichukua fedha na ametajwa kwenye taarifa ya CAG. Sasa tunataka utusaidie ni ukurasa wa ngapi au ni kwenye kitaku kipi? Umenielewa?

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya kazi *briefing* ya CAG, na hiyo *briefing* anakuwa ameitoa kutoka kwenye ukaguzi wake. Kwa hiyo yeye anakuwa ametuonesha ili atupe kuifanya kazi kwa hiyo kuisema hapa hakuna makosa.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

TAARIFA

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokuwa anazungumza Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC ni

jambo sahihi na la ukweli. Hoja ya nani, wakati anatoa maelezo yake amesema Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya. Kwa hiyo kutaja tu Wilaya ya Longido, na huu ni ukaguzi wa 2021, maana yake ameshataja nani muhusika, bila kusema jina.

Mheshimiwa Mwenyekiri, nafikiri ichukuliwe tu hivyo.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Conchesta endelea. Kwa kuwa muda wako uliisha nakuongeza dakika moja uhitimishe hoja yako.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwanza meza yako imenilinda, pia namshukuru makamu mwenyekiti, jambo nililosema ni sahihi. *Mimi I am so carefully nimekuwa kwenye kamati hii zaidi ya miaka saba kwa hiyo siwezi kuropoka hapa, lazima niseme ambacho kiko sahihi.* Ahsante sana kwa nafasi hii uliyonipa.

MWENYEKITI: Haya. Nilimwita Mheshimiwa Ali Mohammed Kasinge wakati huo mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu anajiandaa.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili nami jioni ya leo nichangie hoja zilipo mezani. Pia kwa upekee wake nitajikita zaidi kwenye hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kama ambavyo imebainisha na taarifa ya CAG kwa hesabu za kuishia Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya leo nitakuwa na hoja kubwa mbili tu. Hoja ya kwanza ni uwezo wa halmashauri zetu katika utekelezaji wa miradi ya

maendeleo. Kwa mujibu wa taarifa ya CAG kumekuwa na changaomoto katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, na kwa ridhaa yako naomba nitoe mifano michache;

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Halmashauri ya Mji wa Newala, sekta ya elimu peke yake Shule ya Msingi Lidumbe mradi wa nyumba ya mwalimu umetelekezwa tangu mwaka 2015. Shule ya Msingi Mnaida, mradi wa nyumba ya mwalimu umetelekezwa tangu mwaka 2012. Shule ya Msingi Mcholimbili, mradi wa nyumba ya mwalimu tangu mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, madarasa 25 yametelekezwa, nyumba za walimu 37 zimetelekezwa, maabara 26, zahanati 12 na mabwalo ya chakula mawili. Halmashauri ya Kasulu miradi 34 ambayo imeanzishwa na jamii imetelekezwa, haikuweza kukamilishwa. Nimalizie kwa mifano michache na halmashauri ya Kigoma Ujiji, kati ya miaka mitatu hadi kumi na moja, miradi yenyeye thamani ya shilingi 1,251,000,000/= imetelekezwa bila kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake hapa? Maana yake ni kwamba, fedha za Watanzania walipa kodi zimeangamizwa bila kuleta tija yoyote. Jambo kama hili, sisi kama wabunge, wawakilishi wa wananchi ambaa ndio walipa kodi haipaswi kulinyamazia. Hapa tumezungumzia fedha ambazo zimeingizwa kwenye miradi hii ya muda mrefu ambayo haikukamilika na haitumiki. Maana yake ni kwamba fedha za Watanzania zimekwenda bila kuleta tija. Hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kikubwa ni kwamba halmashauri zetu hatujazijengea uwezo katika maeneo

mawili; eneo la kwanza ambayo ni usimamizi na eneo la kutoa ruzuku kwa halmashauri zetu katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Baadhi ya Wabunge hapa wamechambua, kwamba kumekuwa na uwiano usioridhisha wa kutoa ruzuku za miradi ya maendeleo katika halimashauri zetu. Zipo halmashauri ambazo zimepata ruzuku zaidi ya asilimia 100 na zipo ambazo zimepata ruzuku chini ya asilimia 40, kwa mujibu wa taarifa ya CAG. Hii imesababisha ndio matokeo ya miradi zaidi ya miaka minane, imetelekezwa na haina tija yoyote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni matokeo ya haya ni usimamizi usioridhisha wa mamlaka zetu za Serikali za mitaa kwenye vyombo vyake vya usimamizi. Hapa kwa upekee kabisa niseme, *regional secretariat* (Sekretarieti za mikoa). Kimsingi, kwa utendaji usioridhisha wa halmashauri zetu, mtu wa karibu kabisa ambaye ndiye mkono wa karibu wa ofisi ya Rais, TAMISEMI wa kusimamia ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa chini ya Sekretarieti ya mkoa. Lakini, ni kiwango gani sekretarieti zetu za mikoa tumeziweshesha kusimamia halmashauri? Ni kwa kiwango gani watendaji pamoja na maafisa waliopo pale kwenye sekretarieti za mikoa wamejengewa uwezo wa kusimamia Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.? Ni kwa kiwango gani mamalaka zetu za sekretarieti za mikoa watendaji wake wamekuwa na uzoefu wa kutosha wa usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hili ni janga na ni jukumu la Serikali kuliangalia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili mahsus ambalo ningependa kulitolea uchambuzi katika taarifa hii ni mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Halmashauri 46, kwa mujibu wa taarifa ya CAG zenye POS 1,355 hazikuwa katika mfumo wa kukusanaya mapato mpaka ripoti hii

inatolewa. Pia halmashauri nane zilipoteza POS 34 na halmashauri 27 zilifanya marekebisho ya ankara kiasi cha shilingi bilioni moja milioni mia sita na ushee, bila kiambatisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kulikuwa na utaratibu katika halmashauri zetu, watendaji wasio na nia njema ya nchi hii kuiba fedha za wananchi wakati tukitumia mifumo wa stakabdhi za kuandika kwa mikono maarufu kama HW5. Kulikuwa na utaratibu wa kupoteza vitabu kwa makusudi wakati tayari fedha zimekusanywa, halafu watendaji wasio na nia njema walikuwa wanapiga hizo fedha. Tulipoleta mifumo hii ya ukusanyaji wa fedha kwa njia za kielektroniki tulidhani utakuwa ndio mwarobaini wa kurekebisha mapungufu haya. Badala yake watendaji hao hao wasiokuwa na nia njema na nchi yetu, wamekuwa wakitumia mifumo hii hii ya kielektroniki, kwa maana ya mashine za kukusanya mapato lakini bado wanapiga kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoambiwa kwamba halmashauri nane zilipoteza POS maana yake ni kwamba walikusanya halafu fedha za Watanzania zikaenda mifukoni mwa watu binafsi halafu baadaye wanasema POS zimepotea. Hili ni jambo ambalo haliwezi likakubalika. Pia tunaambiwa kwamba katika halmashauri ambazo zimakaguliwa na CAG kwa taarifa ya kuishia Juni, 2021 kiasi cha shilingi bilioni 17 za mapato zilikusanywa na POS lakini hazikupelekwa benki. Maana yake ni kwamba zilibaki kama fedha mbichi na zilitumika zikiwa fedha mbichi bila kupelekwa benki. Sasa haya mambo ni msiba mkubwa sana katika taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu hiyo nilikuwa na mapendekeo yafaatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, kama nilivyosema, kwamba haya yote ni matokeo ya mifumo ya usimamizi istoridhisha. Kwa hiyo jukumu la kwanza kabisa ni kuimarisha mfumo wetu wa usimamizi hususani kuimarisha eneo lile la *regional secretariat* ili Ofisi ya Rais TAMISEMI isipate shida sana, kwamba Maafisa wa TAMISEMI kuhangaika kuwa wanashuka kwenye halmashauri. Tuna halmashauri 184 nchi nzima, watumishi au maafisa wa Wizara hawatoweza kutosheleza kuzunguka kwenye halmashauri 184 kwaajili kutoa au kujenga uwezo kwa watendaji wetu au kusimamia miradi. Jukumu la *regional secretariat* ni kuisaidia Ofisi ya Rais TAMISEMI, kwa maana ya Wizara, kwa niaba yake, kuzisimamia hizi halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uwezo wa kiutendaji na wa kiuzoefu wa maafisa waliopo kwenye *regional secretariat* zetu unakuwa si kwenye kiwango ambacho wangeweza kuzisimamia halmashauri hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona ni changamoto na nipayendekeze hapa ni muundo wenyewe uliopo kati ya watendaji wa halmashauri na muundo wa *regional secretariat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Ofisi ya Rais TAMISEMI ilipitisha muundo ambao ulinakwenda kutekelezwa na watendaji wetu wa halmashauri lakini muundo huu kimsingi si muundo ambao ulikuwa shirikishi. Sisi kama Madiwani, Wabunge hatukushirikishwa katika kupayendekeza muundo huu. Hata hapa Bungeni sidhani kama kulikuwa na semina ya kuonesha kwamba tunaenda kutekelezwa nuundo huu. Sasa tunapaktekelezwa muundo ambao umetoka juu na kushuka tu kutekelezwa

kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kuhusisha wadau wakaingiza *inputs* zao matokeo yake ndiyo haya ambayo CAG anakuja kuyaibua. Utaratibu huu wa mapungufu ya kiutendaji na usimamizi yataendelea kuwa ni mwiba katika nchi hii mpaka pale ambapo muundo wa usimamizi utakapokuwa umekaa vizuri.

Mhehimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ali Mohammed Kasige kwa kutumia muda vizuri zaidi. Nilimwita Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na kisha Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye ripoti hizi ambazo zimewasilishwa ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitasema kidogo kwenye ripoti ya PAC katika eneo ni moja tu la usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamejadili katika eneo hili kwa kugusia jinsi gani mikataba kwenye nchi yetu haiheshimiwi; jinsi gani mikataba ambayo imefungwa vizuri pasiposhaka na wataalamu wetu, kwa maana ya wanasheria wabobezi (*land lawyers*) ikija katika usimamizi wake inaleta shida katika nchi yetu. Mifano iko mingi, michache tutaisema lakini mingine imesemwa na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti ya CAG ametoa mifano mingi sana ya jinsi mikataba ilivyoshindwa

kusimamiwa vizuri mpaka fedha za umma zimepotea nyingi sana. Nitasema mifano kama miwili;

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mikopo mingi sana ambayo imekuwa inakuja baada ya makubaliano ya nchi yetu na mashirika ya kimataifa. Pamekuwa na mradi mikubwa ambao ulikuwa unaendeshwa chini ya TANROAD, Mradi wa Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni huzuni sana, fedha tunazikopa nje, nyingi sana. Kama ambavyo tunaendelea kukopa fedha nyingi, na mimi nakubaliana kabisa na taratibu za kukopa, na hasa hii mikopo ambayo Mama Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa awamu ya sita ambaye tunaenenda naye. Mikopo mizuri yenye tija na isiyo na riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masharti ya kimkataba ambayo pale ambapo tunakubaliana kuchukua mikopo mikubwa kwa ajili ya kufanya miradi hasa ya barabara ambayo imetolewa na CAG; katika mradi huu niliotamka, Mradi wa Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi Kusini mwa Afrika, palitokea malipo ya ada isiyo na tija ya ada ya huduma ya kifedha ya zaidi ya dola za kimarekani laki moja na ishirini na tisa mia tisa na sitini na nane. Hizi ni takriban milioni mia tatu na hamsini, zilipotea tu, na tulifikia tukalizilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tulizilipa? Tulipewa mkopo fulani mkubwa ambao ulituambia mpaka kufikia tarehe 30 Julai, 2013, miaka kadhaa, zaidi ya kumi ilitakiwa tuwe tumekamilisha miradi husika. Lakini kwa sababu ambazo, inawezekana *design* ya mradi ilikuwa na changamoto, na sababu zingine ambazo hazina

mantiki kabisa tunashindwa ku-meet yale masharti ya kimkataba. Matokeo yake nini; hii ilitokea, bakaa ya fedha ambayo imekopwa; katika bakaa yoyote ambayo ulitakiwa uitumie kwa kipindi fulani na ukashindwa kukitumia makubaliano ya mkataba ni kwamba utakatwa robo ya tatu ya asilimia moja ya kiasi ulichoshindwa kutumia. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikabaki Dola za kimarekani milioni kumi na saba laki tatu ishirini na tisa mia moja themanini na nne na nukta kama ishirini, na taarifa ya Kamati inatuambia hivyo. Ukitafuta robo tatu ya aslimia moja ya fedha hizo dola milioni 17 unapata dola 129,698.90, zaidi ya milioni mia tatu na hamsini; na tukazilipa, tunalipa tu halafu tumetulia. Aliyesababisha damage hii kama nchi hakuna chochote alichofanyiwa na hakuna lolote lililoendelea, *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu; mfano mwingine CAG anatuambia wa kushindwa kusimamia mikataba yetu ambayo wenyewe tumeiingia, kulikuwa kuna ongezeko la gharama za fidia ya kiasi cha shilingi bilioni 22.35, na hii ni kutokana na kutolipwa kwa kaya 1,125.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 Wizara iliyokuwa ya Uchukuzi na Mawasiliano Iliingia na Mkandarasi Mshauri kuhusu jinsi gani ya kuongeza *Airport* yetu Julius Nyerere *International Airport*. Katika ule mchakato wa kuongeza kulikuwa na kaya nyingi sana zilitakiwa zilipwe mabilioni. Kiukweli niishukuru Serikali yangu Sikivu, kwa kiasi fulani ilifanikiwa kulipa.

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli pia katika mwaka ule kwa sababu za kibajeti hatukufanikiwa kuwalipa wote

au kulipa fidia zote, tukabakiza wananchi 1,125, ripoti ya CAG inatuambia hivyo. Wale wananchi walitakiwa kulipwa bilioni saba za Kitanzania; lakini tangu mwaka huo hadi tathimini ya mwisho inafanyika mwaka 2020 unaweza ukaona hakuna chochote kilicholipwa wakati wote. Msimamizi wa mkataba hayupo na hajui kama kuna watu aliwaacha pending hajamalizana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 13 (3) ya Kanuni za Ardhi, Uhakiki na Thamani ya Fidia na Ardhi ilibidi wajielekeze kwenye kufanya tathimini upya ili kujua bilioni saba zimeongezeka kiasi gani, zile za wale watu wetu 1,125 ambalo ni jambo jema, ni takwa la kikanuni. Tulipoenda wakasema riba ni asilimia sita, tangu mwaka 1997 hadi mwaka 2019, lakini ilibidi riba iongezeke, ikatupeleka mpaka wakafanya uthamini wa mara kwa mara. Ilikuwa jambo jema sana ili wananchi wetu wasionewe, ikatufikisha kwenye 29,768.029,951 zaidi ya bilioni 22; nataka kusema jambo hapo. Si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tumefika wakati tunasema tuna mradi X tunataka kuutekeleza kama nchi, huu wa kufungua *airport* yetu wakati huo tulifikiri ni jambo jema. Maana yake mhandisi mshauri alishasema pana idadi ya watu hawa, tunajua maeneo ya pale, lakini hawa watu wanatakiwa walipwe kiasi hiki. Kama tunakwenda maana yake tuko tayari kwa fedha za ndani na fedha za nje. Sasa kama tumekaa kutoka bilioni saba hadi bilioni 29, tunaambiwa na CAG, bilioni ishirini na mbili nukta kadhaa ni deni mpaka sasa tunavyoongea, sio sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamesema hapa, hii ni kiashiria kibaya sana. Wataalamu wetu wanakaa wanajua kuwa wanatakiwa wasimamie

mikataba ile lakini hawaisimamii kwa wakati lakini wanaacha. Je, wanaacha kusudi ili riba iongezeke? Au wanakuwa na sababu zipi? Sasa tumetoka billion saba hadi bilioni 29. Bilioni 22 linakuwa deni.

Mheshimiwa mwenyekiti, hii sio sawa; fedha za Watanzania zinapotea. Bilioni 22 tungezipeleka kwenye Jimbo la Kibamba. Leo mimi ninalia maji hayatimii, barabara hazipo chini ya kilomita tano za TARURA na TANROAD hakuna. Huduma nyingine ni changamoto sana. nimpongeze sana Mama Samia anatusaidia sana, tunaona huduma nyingine za afya na elimu zinakuja, lakini tunashida kubwa bado. Maji hatuyaoni maeneo mengi, na ninasema kila siku, barabara bado sana, idadi ya watu Dar es salaam ni zaidi ya milioni nne na nusu. Sasa, hivi tunafanyaje? Sio sawa, lazima tuiseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nilikuongeza dakika kwa sababu muda wako ulikuwa umeisha.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hizo sababu mbili za kushindwa kusimamia mikataba ya nchi yetu vizuri. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda, aweze kuchangia.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa heshima hii, nami niweze kuchangia

uwasilishaji wa taarifa za kamati tatu za oversite. Nami nichukue nafasi hii kuanza kuzipongeza hizi Kamati zimefanya kazi zake vizuri kwa mujibu wa taarifa ambazo wamewaslisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kulizungumza, kabla ya kuanza kujadili taarifa ya CAG mimi binafsi nilikuwa natamani kamati zetu zingejadili taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa siku ya tarehe 30/03/2022 alipopokea taarifa ya CAG na taarifa ya TAKUKURU. Mheshimiwa Rais baada ya kupokea taarifa hizo, alibainisha na kutoa maagizo na maelekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza alisema, kupitia ripoti hizo mbili, kwamba kuna udhaifu katika uratibu wa Serikali kwa ujumla (*Government coordination*) ikiwemo kuchelewa kutoa maamuzi hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kutokana na tatizo hilo, akaelekeza Katibu Mkuu Kiongozi achukue hatua mahususi kurekebisha udhaifu huo. Kwa hiyo, nilitegemea wapate taarifa ya utekelezaji kwa hii miezi tangu agizo hili litolewe. Hali ya utekelezaji wa agizo hili ikoje Serikalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Rais alisema, kuna udhaifu kwenye ufuatiliaji wa tathmini ikiwemo utaalamu hafifu na nyenzo hafifu. Akaagiza Taasisi ya Uongozi (*Uongozi Institute*) ifanye uchambuzi na kuishauri Serikali ipasavyo. Kwa hiyo, nilitegema Kamati zetu nazo zifuatilie status ya utekelezaji wa agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Mheshimiwa Rais akasema, kuna udhaifu Serikalini wa kuwa na mifumo mingi sana ya utoaji wa taarifa ambapo mifumo hiyo haiwasiliani, yaani haiongei. Akaagiza mifumo yote ya

mawasiliano Serikalini na kupeana taarifa iangaliwe ili ikiwezekana kuwe na mfumo mkubwa mmoja unaoongea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea kwa sababu haya ni mambo ya msingi ambayo kama yatarekebishwa, yataweza kuondoa yale matatizo ambayo yanaonekana kwenye taarifa za CAG angalau kwa robo tatu yake. Sasa haya mambo ni muhimu sana. Nilikuwa napendelea sana hata kama hawakuyajadili, basi siku zijazo waweze kukaa na kupata *status* ya utekelezaji kwa sababu haya yalikuwa ni maelekezo ya kisera ambayo yana umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye taarifa ya CAG. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 143 (1)(a) na (b) inampa mamlaka mdhibiti au CAG afanye kazi ya kudhibiti. Udhibiti (*control*); yaani *controller* anapewa mamlaka na hivyo vipengele viwili, (a) na (b). Sasa katika taarifa ya CAG mimi sijaiona taarifa ya CAG inayoelezea jinsi alivyotimiza jukumu lake la udhibiti kwenye taarifa hiyo. Nilitegemea aeleze. Tatizo ni nini? Tatizo kuu, usimamizi wa jukumu hilo umewekwa kwenye Mahakama, ndiyo maana amekuwa hatoi taarifa kuhusu udhibiti kwa Bunge au hata kwa Rais kwa sababu usimamizi wake umewekwa kwenye Mahakama, kupitia kipengele gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 143 (6), nanukuu, inasema hivi: "Katika kutekeleza madaraka yake, kwa mujibu wa ibara ndogo za (2), (3) na (4) za ibara hii, CAG hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo haya ya ibara hii ndogo hayataizua Mahakama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili kuchunguza kama CAG

ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au sivyo." Mwisho wa kunukuu. Kwa hiyo, kama usimamizi wake umewekwa kwenye Mahakama, kwa hiyo, inategemea malalamiko. Ni nani alalamike Mahakamani ili CAG aweze kusimamia ipasavyo katika utelezaji wa jukumu hili la control?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia CAG atueleze kwamba katika mwaka wa fedha huu alioukagua, yeye katika jukumu lake la udhibiti, tarehe fulani alitoa approval Serikali itumie kiasi kadhaa; tarehe nyingine akatoa approval Serikali itumie kiasi kadhaa; na tarehe nyingine akatoa approval Serikali itumie kiasi kadhaa. Hilo ni jukumu lake ambalo ni *not delegated*, yaani haliwezi kuwa delegated kwa mtu mwingine yeote isipokuwa tu ni CAG mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu taarifa hizi huwa hatoi, nilikuwa napendekeza, utakapofika wakati wa kurekebisha Katiba, tuzingatie kwamba lazima CAG apewe chombo ambacho kitamsimamia kwenye jukumu hili la control kama siyo Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la tatu ambalo ningependa kulizungumzia kwa mujibu wa taarifa yake, huyu CAG amejipambanua kutekeleza vizuri sana jukumu lake la pili ambalo ni ukaguzi. Kafanya ukaguzi vizuri na taarifa yake imeeleza kwa asilimia 100 kuhusu jukumu lake hila la ukaguzi wa mahesabu. Amekagua vizuri na taarifa ziko vizuri. Tatizo lipo kwenye hatua za kuchukua baada ya taarifa zake. Hatua za kuchukua zimekuwa ndogo ndogo sana na kuoneana aibu, labda na kuheshimiana, vitu kama hivyo. Ndiyo maana kila mwaka amekuwa analeta kwenye taarifa zake matatizo yale yale yanayofanana, kwa sababu hatua hazichukuliwi.

Matatizo gani ambayo yamekuwa yanaonekana kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kutokupatikana kwa nyaraka za mapato na matumizi ili azikague kwa wakati; la pili, nyaraka kutokuwa halali; la tatu, kutokutekelezwa kwa mikataba kwa wakati na mapungufu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokutekelezwa kwa mikataba ni tatizo kuu la msingi katika utekelezaji wa miradi. Kwa sababu utekelezaji wa mikatana ili uwe mzuri, kuna mambo mawili; sheria ya ununuzi imeelekeza kwamba kila Afisa Masuuli kule ambako mradi unatekelezwa, anatakiwa atue wataalamu wawili, watatu au zaidi kadri atakavyoona yeye inafaa, wa kusimamia mradi siku kwa siku. Kwa hiyo, kila idara ya Serikali, kila Wizara, kila halmashauri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako ulikuwa umekwisha.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nimetumia kama dakika tano hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila taasisi inatakiwa itekeleze hili jukumu, lakini wamekuwa wanalifanya nusunusu na ndiyo maana kunakuwa na matatizo. Sehemu nyingine hata hao wasimamizi hawateuliwi na hatua hazichukuliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu lingine ili mradi utekelezwe vizuri, lazima kuwe na maafisa mahususi kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Nao vile vile wamekuwa hawatekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo limeonekana, ni kutokutekelezwa kwa ushauri na mapendekezo ya CAG kwa wakati. Hilo nalo ni tatizo. Sheria imeweka muda maalumu kwamba taarifa ya CAG baada ya kutoka, anatakiwa Afisa Masuuli aandae program au mpango mkakati wa namna atakavyotekeleza mapendekezo ya CAG. Wamekuwa hawafanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mapendekezo yamekuwa yakijitokeza miaka yote na maafisa wetu wa Serikali wala hawaogopi chochote kwa sababu hatua zimekuwa hazichukuliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri katika maeneo kama mawili au matatu hivi. La kwanza, sheria zipo na zinajitosheleza na zinaweza kutumika kuwachukulia hatua watu ambao wanakosea, lakini zimekuwa hazitumiki. Hawa watu siyo kwamba hawazijui sheria, wanazijua. Wanajua sheria ya ununuzi, wanajua Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma, wanazijua vizuri, lakini makosa mengi yanafanyika kwa makusudi. Naomba sana hatua zile zinazoeleweka ziwe zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Kamati za Oversight naomba ziongeze ukali wa mapendekezo yao, ikiwa ni pamoja na kulishauri Bunge kuhusu maazimio ya kuchukua. Nimemsikia Mheshimiwa aliyekuwa anatoa

3 NOVEMBA, 2022

mapendekezo ya maazimio ya Bunge, yeye mwenyewe, lakini yeye mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri kule kwenye kamati ndiyo wangeshauri Bunge kwamba Bunge kwamba tunaazimia, ili Bunge liazimie kuchukua hatua moja, mbili, tatu. Hiyo ingelisaidia Bunge kufanya maazimio ambayo yangeisaidia Serikali kuweza kurekebisha maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naona muda umekwisha, naomba niishie hapo. Naomba sana tujipambanue katika utekelezaji wetu.

MWENYEKITI: Umesema una mapendekezo manne, malizia tu.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Naam!

MWENYEKITI: Au ni hayo mawili tu! Basi sawa, ahsante.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wetu jioni hii imekamilika. Hivyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho tarehe 4 Novemba, 2022 saa tatu asubuhi.

(Saa 1.49 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 4 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)